**UNIVERSITY OF EMBU**

**ELIZABETH WANJIRU WAITHAKA**

**MA**

**2025**

# UNYANYASIKAJI WA WANAUME KATIKA DIWANI ZA TUMBO LISILOSHIBA NA MASKINI MILIONEA NA HADITHI NYINGINE

**ELIZABETH WANJIRU WAITHAKA**

**TASNIFU HII YA UTAFITI IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHLI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA EMBU**

**AGOSTI, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ya utafiti ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa mahali pengine popote kwa ajili ya shahada au tuzo nyingine yoyote.

Sahihi……..................................................……Tarehe……………………………

Elizabeth Wanjiru Waithaka
Idara ya Masomo na Jamii
E556/1455/2020

Tasnifu hii ya utafiti imewasilishwa kwa ajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo.

Sahihi……..................................................……Tarehe……………………………

Dkt. John Khaisie Wanyama
Idara ya Masomo na Jamii
Chuo Kikuu Cha Embu

Sahihi……..................................................……Tarehe……………………………

Dkt.Timothy Kinoti M’Ngaruthi
Idara ya Masomo na Jamii
Chuo Kikuu Cha Embu.

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu  Baba James Waithaka na Mama Esther Muthoni kwa kunilea, kunisomesha na kunipa motisha kila wakati. Mungu azidi kuwaneemesha na kuwaongezea miaka mingi duniani. Kwa mume wangu John Njeru kwa kuwa mwombezi wangu na wanangu Patience Mwende, David Macharia, Daniel Waithaka na Emmanuel Murimi kwa kuwa nguzo muhimu kwangu.

## SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa umbali huu amenifikisha. Neema zake na kibali zimekuwa kwa wingi.

Pia, nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu ambao pia ni wahadhiri wangu katika kiwango hiki, Dkt. John Khaisie Wanyama na Dkt.Timothy Kinoti kwa msaada wao wa kuhakikisha kazi hii imefika kiwango hiki na kwa kujitolea kutufundisha katika kiwango cha uzamili. Uongozi wenu wa busara na ushauri wenu wenye uvumilivu ulinifaa katika utafiti huu. Nawashukuru kwa kunivumilia kuanzia mwanzo hadi nikafikia tamati mwa kazi hii.

Kwa njia ya kipekee nashukuru usimamizi wa Chuo Kikuu cha Embu kwa kunipa nafasi ya kuendeleza masomo yangu. Shukrani kwa wahadhiri wote wa Idara ya Masomo ya Jamii katika Chuo Kikuu Cha Embu kwa kunielekeza katika masomo yangu na pia kunipa mwongozo nilipokuwa nikitetea pendekezo la utafiti huu na kwa kutoa maoni ya kuboresha kazi hii, Mungu awabariki sana.

Shukrani zingine ni kwa wazazi wangu James na Esther, dada na kaka zangu, Mercy Nyambura, Alice Wanjiku, Mary Mugechi, Monika Wairimu, Patrick Gitau, Paul Kamanja, Cecilia Wanjiku na Esther  Wanjiru kwa kusimama nami kila wakati kwa hali na mali. Mungu awabariki na awalinde kila wakati.

Kwa wanafunzi wenzangu, Faith Mbithe, Caroline Kathure na Martha Moraa, asanteni kwa kunipa motisha katika masomo na kushirikiana nami katika mijadala yote ambayo kwa kweli ilinijenga na kupanua akili yangu. Safari hii ilikuwa ndefu lakini kwa ushauri wenu nimeweza kuikamilisha salama.

Mwisho, namshukuru mume wangu mpendwa John Njeru na watoto wangu, Patience Mwende, AlvinDavid Macharia, Daniel  Waithaka na Emmanuel Murimi kwa kunifaa kwa hali na mali wakati wa masomo yangu. Mmekuwa waombezi wangu wa kila siku. Mungu azidi kuwalinda.

## YALIYOMO


**UNGAMO** .......... **ii**

**TABARUKU** .......... **iii**

**SHUKRANI** .......... **iv**

**UFAFANUZI WA ISTILAHI** .......... **viii**

**ABSTRACT** .......... **ix**

**IKISIRI** .......... **x**

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**UTANGULIZI** .......... **1**

1.1. Usuli wa Mada .......... 1

1.2. Suala la Utafiti .......... 3

1.3. Madhumuni ya Utafiti .......... 3

1.4. Maswali ya Utafiti .......... 4

1.5. Sababu za Kuchagua Mada .......... 4

1.6. Umuhimu wa Utafiti .......... 5

1.7. Upeo na Mipaka .......... 5

**SURA YA PILI** .......... **7**

**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA** .......... **7**

2.1. Utangulizi .......... 7

2.2. Dhana ya Jinsia .......... 7

2.3. Unyanyasikaji wa Wanaume .......... 7

2.4.1. Utafiti wa Awali Kuhusu Namna Wanaume Hunyanyasika .......... 8

2.4.2. Athari za Unyanyasikaji wa Wanaume .......... 11

2.4.3. Mbinu Wanazotumia Wanaume Kupambana Dhidi ya Unyanyasikaji ... 13

2.5. Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho .......... 15

2.6 Hitimisho .......... 18

**SURA YA TATU** .......... **19**

**MBINU ZA UTAFITI** .......... **19**

3.1. Utangulizi .......... 19

3.2. Mkabala wa Utafiti .......... 19

3.3. Eneo la Utafiti .......... 19

3.4. Walengwa .......... 19

3.5. Uteuzi wa Sampuli .......... 20

3.6. Ukusanyaji wa Data .......... 20

3.7. Uchanganuzi wa Data ........ 21
3.8. Maadili ya Utafiti ........ 21
3.9 Hitimisho ........ 22
**SURA YA NNE ........ 23**
**MATOKEO YA UTAFITI ........ 23**
4.1. Utangulizi ........ 23
4.2. Muundo wa Uchanganuzi ........ 23
4.3. Namna Wanaume Hunyanyasika ........ 23
4.3.1. Wake Kushiriki Mapenzi Nje ya Ndoa ........ 23
4.3.2. Kutenganishwa na familia ........ 27
4.3.3. Kukataliwa Uchumba ........ 30
4.3.4. Kutukanwa ........ 32
4.3.5. Kunyimwa Chakula ........ 34
4.3.6. Kuchapwa ........ 36
4.3.7. Kufanyishwa Kazi za Nyumba ........ 38
4.4. Athari za Unyanyasikaji wa Wanaume ........ 40
4.4.1. Majuto ........ 41
4.4.2. Kukata Tamaa ........ 44
4.4.3. Ukosefu wa Amani ........ 46
4.4.4. Majeraha ya Mwili ........ 49
4.4.5. Upweke ........ 52
4.4.6. Kusambaratika kwa Asasi ya Ndoa ........ 55
4.4.7. Msongo wa Mawazo ........ 57
4.5. Mbinu Wanazotumia Wanaume Kupambana Dhidi ya Unyanyasikaji ........ 60
4.5.1. Kuvumilia au Ustoa ........ 60
4.5.2. Kuchunguza na Kuchukua Hatua Hatari ........ 63
4.5.3. Kujipa Matumaini na Kuomba kuwa Hali Itabadilika ........ 65
4.5.4. Kunyamaza au kutojali ........ 67
4.5.5. Hatua ya Kujisaka na Kutafuta Suluhu ........ 70
4.6 Hitimisho ........ 72
**SURA YA TANO ........ 73**
**MAJADILIANO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 73**
5.1. Utangulizi ........ 73
5.2. Majadiliano ........ 73
5.2.1. Namna Wanaume Hunyanyasika ........ 73

5.2.2. Athari za Unyanyasikaji wa Wanaume .................................................... 74
5.2.3. Mbinu Wanazotumia Wanaume Kupambana Dhidi ya Unyanyasikaji ... 75
5.3. Hitimisho ......................................................................................... 75
5.4. Mapendekezo ..................................................................................... 76
5.5. Hitimisho la sura ................................................................................ 77
**MAREJELEO ........................................................................................ 78**
**KIAMBATISHO ..................................................................................... 85**

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| **Dhalilisha** | Kumfanya mwanamume awe duni, mnyonge au kumdharau. |
| **Dhuluma** | Kitendo cha kumnyima mwanamume haki au stahiki yake. |
| **Jinsia** | Namna mke au mume hutambulika katika jamii. |
| **Kufasiri** | Kitendo cha kuchunguza na kueleza maana ya mwandishi au maana ya kazi ya fasihi. |
| **Unyanyasikaji** | Ni kuteseka kunakotokana na hali ya kuwa mwanamume katika jamii iliyomwekea mtoto wa kiume shinikizo za aina tofauti. Mateso haya yanatokana na hali anuwai za kimaisha. |
| **Mtagusano** | Hali ya kuingiliana kwa kitu na kingine au watu na wengine. Katika kazi hii mtagusano unarejelea mwingiliano wa vipengele vya utambulisho vya nadharia. |
| **Vitambulisho** | Vipengele vinavyotambulisha kunyanyasika kwa mwanamume kama vile: uchumi, jinsia, utabaka, matarajio ya kijamii na kadhalika. |
| **Ustoa** | Hali ya kukubali mambo ambayo hatuwezi kuyabadilisha. Ni hatua ya kwanza ya kupata amani ya akili. |
| **Shinikizo** | Hali ya wanaume kubanwa na matarajio ya kijamii. |
| **Ubabedume** | Ni hali ya kumkweza mwanamume katika jamii |

## ABSTRACT

Literature as a mirror of the society uses language very effectively to give us a true picture of what is happening in the society. This research focused on the suffering of men in the selected literary works. The research investigated the issue of the violation of rights of men as depicted in selected Kiswahili literary works, that is, selected stories in *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (2016*) edited by Alifa Chokocho and Dumu Kayanda, and *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine (2012)* edited by Ken Walibora. This research evaluated ways in which men suffer, effects of this suffering and the methods they use to free themselves. This research was guided by Intersectionality Theory. Purposeful sampling technique was used to get the samples. The research data was collected through reading the selected Kiswahili literary works and analysing it through descriptive method guided by the objectives of the research. The findings of the study indicate that men experience various forms of suffering, including extramarital infidelity, family break-ups, break- up of engagement, abuse, deprivation of food, carrying out domestic chores, and physical violence. The factors contributing to the perpetration of male suffering encompass economic status, gender, social class, and societal expectations. The effects of suffering manifested in several profound ways, including feelings of regret, hopelessness, disrupted peace of mind, experiences of physical assault, social isolation, family break-ups, and depression. The study further revealed that men fight against these adversities through mechanisms such as perseverance or stoicism, investigating ant taking risky actions, cultivating hope and optimism, intentional silence and indifference, and introspection and seeking solutions. Although men often employ these mechanisms to cope with their suffering, these methods prove to be inadequate. Consequently, it is important that they seek assistance from appropriate professionals. This study offers valuable insights for literary scholars by showing various dimensions of male suffering and its effects. Furthermore, it holds significance for male activists by underscoring the pivotal role of Kiswahili literature in addressing and articulating the experiences of male suffering both within Kenya and in a global context.

## IKISIRI

Fasihi kama kioo cha jamii hutumia lugha kwa ufanifu mkubwa kutuchorea taswira kamili ya yale yanayotendeka katika jamii. Utafiti huu uliangazia unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Utafiti ulichunguza suala la ukiukaji wa haki za wanaume kama ilivyosawiriwa katika hadithi fupi teule katika diwani za *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (2016)* iliyohaririwa na Alifa Chokocho na Dumu Kayanda na *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine (2012)* iliyohaririwa na Ken Walibora. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa; kubainisha namna wanaume hunyanyasika katika hadithi fupi za Kiswahili, kutathmini athari za unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi fupi za Kiswahili na kubainisha mbinu wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi. Data ya utafiti huu ilitokana na kusoma hadithi fupi teule za Kiswahili na kuzichanganua kimaelezo kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa mwanamume hunyanyasika kwa namna nyingi kama vile: wake kushiriki kimapenzi nje ya ndoa, utengano wa kijamaa, kukataliwa uchumba, upyaro, kunyimwa chakula, kuchapwa na kufanyishwa kazi za nyumba. Vipengele vya utambulisho vinavyoshirikiana na kusababisha unyanyasikaji wa wanaume ni: uchumi, jinsia, tabaka na matarajio ya kijamii. Athari za unyanyasikaji wa wanaume zilizojitokeza ni kama vile majuto, kukata tamaa, ukosefu wa amani, majeraha ya mwili, upweke, kuvunjika kwa ndoa na msongo wa mawazo. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wanaume hupambana dhidi ya unyanyasikaji kupitia mbinu za uvumilivu au ustoa, kuchunguza na kuchukua hatua hatari, kujipa tumaini na kuomba kuwa hali itabadilika, kunyamaza au kutojali, hatua ya kujisaka na kutafuta suluhu. Hata ingawa wanaume hutumia mbinu hizi kupigana dhidi ya unyanyasikaji, zilibainika kuwa pungufu. Hivyo, wanapaswa kutafuta msaada kutoka kwa wataalamu husika. Utafiti huu una umuhimu kwa waandishi wa fasihi kwa kuwawezesha kutambua namna wanaume hunyanyasika pamoja na athari zake. Pia, utafiti huu unatoa mchango kwa wanaharakati wa haki za wanaume kuhusu mchango wa fasihi ya Kiswahili katika kuangazia suala la unyanyasikaji wa wanaume nchini Kenya na kote ulimwenguni.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1. Usuli wa Mada

Fasihi kama kioo cha jamii hutumia lugha kwa ufanifu mkubwa kutuchorea taswira kamili ya yale yanayotendeka katika jamii. Hadithi fupi kama utanzu wa fasihi huwasilishwa ili kupitisha ujumbe kutoka kwa mwandishi hadi kwa msomaji au msikilizaji. Hadithi fupi huwa na kipengele cha maudhui. Maudhui haya hujumuisha masuala yanayotendeka katika jamii. Utafiti huu ulichunguza unyanyasikaji wa wanaume katika diwani za *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (2016*) na *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine (2012).*

Kulingana na Crouse (1998), unyanyasikaji ni ukandamizaji wa kimfumo unaodhihirika kwa mtu binafsi, baina ya kundi moja na kundi jingine au jamii kwa jumla. Hivyo, unyanyasikaji ni kinyume cha haki na usawa. Ni kuteseka kunakotokana na hali tofauti. Unyanyasikaji katika jamii umekuwa jambo la kawaida ambalo limekuwa likiendelea. Unyanyasikaji hasa katika familia ni ukatili unaotokea mara kwa mara na huathiri wanawake, wanaume na watoto.

Kwa mujibu wa Crouse (1998), wanaume huchukuliwa kama watu wenye ujeuri kiasili na hawaruhusiwi kubadilika kihali wanapopitia changamoto. Kwa sababu hii wanaume wanapokumbwa na changamoto hupendelea kujieleza kwa wanaume wenzao kuliko kutafuta msaada kutoka kwa wahudumu wa afya kama vile wanasaikolojia (Vogel et al., 2014). Mara nyingi mwanamume anapoomba msaada huonekana dhaifu kulingana na matarajio ya kijamii. Hali hii huwafanya wanaume kunyanyasika kana kwamba hawahisi maumivu au kuathirika kihisia kama wanawake. Vilevile kazi za kuhatarisha hutengewa wanaume. Hata wanapoumia kazini, wanatarajiwa kunyamaza na kuendelea kana kwamba hakuna kilichotokea. Kazi huchukuliwa muhimu kuliko hisia zao, jambo ambalo huchangia kunyanyasika kwao na ukiukaji wa haki zao (Samritha, 2025).

Katika ngazi za kimataifa, unyanyasikaji wa wanaume hudhihirika. Kwa mfano katika nchi ya Mexico, wanaume hupata mateso mbalimbali kwa sababu ya kuwa wanaume. Mateso haya husababisha madhara mengi kama vile: kuathirika kiakili, kuzua

mawazo ya tanzia, kusababisha hali ya kujidunisha na kujitenga na wengine (Ortiz-Hernadez na Mendoza-Perez, 2021). Ili kukabiliana na changamoto hizi kuna hitaji la uvunjaji wa unyanyapaa, ujenzi wa mazingira salama ambapo wanaume wanaweza wakaomba msaada kwa ujasiri na kukuza uelewa wa kihisia.

Kulingana na ripoti iliyotolewa na *Canadian Men's Health Foundation (2025)* wanaume zaidi ya asilimia hamsini (50%) hawapati msaada wa kutosha kutoka kwa jamii hasa katika masuala yanayowahusu kama wanaume. Hali hii huzidi kuwa mbaya kadri wanaume wanavyokua kwa kuwa mahusiano ya kirafiki hupungua kutokana na majukumu ya kazi, wajibu wa kifamilia, na mitazamo ya kijamii inayokataza wanaume kuonyesha hisia zao kwa uwazi. Hali hii husababisha kunyanyasika kwao.

Nchini Uganda, wanaume huteseka kimyakimya kutokana na changamoto za afya ya akili ambazo mara nyingi hazishugulikiwi (Okiror, 2023). Ingawa matatizo haya hudhihirika wazi miongoni mwa wanaume hasa katika maeneo ya vijijini, ni wachache wanaotafuta msaada rasmi. Hali hii huchochewa na unyanyapaa uliojengeka katika jamii na tamaduni zinazowakataza wanaume kuonyesha udhaifu au kuomba msaada. Kwa sababu hiyo wanaume wengi hujizuia kuonyesha maumivu yao ya kihisia na badala yake kunyamaza huku wakishiriki katika ulevi kama njia ya kukabiliana na matatizo yao. Hali hiyo ya ukimya huongeza mateso yao na kusababisha kudorora kwa afya ya akili, kuzua migogoro ya kifamilia na hata wengine kupata fikira za kutaka kujitia kitanzi.

Kwa mujibu wa Shirika la Takwimu la Kitaifa la Kenya (KNBS, 2022) wanaume nchini Kenya wanabeba mzigo mkubwa wa matatizo ya afya ya akili. Kulingana na takwimu zilizotolewa na shirika hilo, asilimia hamsini na sita nukta tisa (56.9%) ya wanaume huwa na matatizo ya afya ya akili ikilinganishwa na asilimia arubaini na tatu nukta moja (43.1%) ya wanawake. Tofauti hii inaonyesha kuwa matarajio ya kijamii kama vile ya kuwataka wanaume kujitegemea, huwafanya wanaume wengi kushindwa kutambua matatizo yao ya kihisia, kukosa kutafuta msaada kwa wengine kwa wakati au kutokabiliana ipasavyo na changamoto zao. Kwa hivyo, changamoto zinazowakumba baadhi ya wanaume huwa hazitambuliwi mapema na kutibiwa kwa wakati. Hali hii husababisha uraibu wa pombe, kuvunjika kwa mahusiano na hata wengine kujidhuru.

Unyanyasikaji wa wanaume ni tatizo linalojitokeza ulimwenguni kote. Baadhi ya waandishi wa kazi za fasihi wanawasilisha matatizo yanayoikumba jamii kupitia fasihi andishi ya Kiswahili. Kulingana na King'ei (2002), suala la udhalilishaji wa wanawake limepewa uzito wa kutosha katika utafiti wa Kiswahili hadi sasa. Kulingana na Matei (2017) mwanamume hudhalilishwa katika jamii na wakati mwingine nafasi yake kutotambulika. Jambo hili linahalalisha haja ya kuangalia upande mwingine wa sarafu kwa kuzingatia unyanyasikaji wa wanaume katika jamii. Hili lilichochea mshawasha wa kutaka kuchunguza iwapo wanaume wamedhihirishwa kunyanyasika katika utanzu wa hadithi fupi za Kiswahili. Kwa sababu hii, utafiti huu ulilenga kuchunguza unyanyasikaji wa wanaume katika Diwani za *Tumbo Lisiloshiba* na *Masikini Milionea na Hadithi Nyingine.*

## 1.2. Suala la Utafiti

Unyanyasikaji wa wanaume ni suala linalotatiza wanajamii wengi. Haki za wanaume zimeanza kuvutia hisia mseto kutoka kwa wadau mbalimbali. Sababu kuu ni kuwa jamii imeegemea katika kutetea ukombozi wa wanawake kwa muda mrefu na kupuzilia mbali unyanyasikaji wa mtoto wa kiume. Utafiti huu ulilenga kuangazia dhuluma dhidi ya wanaume katika fasihi ya Kiswahili kwa kuchunguza diwani teule za hadithi fupi. Licha ya kuwepo tafiti za unyanyasikaji wa wanaume katika riwaya za Kiswahili, suala hili halijachunguzwa kwa kina katika utanzu wa hadithi fupi. Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza suala la unyanyasikaji wa wanaume kama linavyodhihirika katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine* na *Maskini Milionea na Hadithi nyingine*.

## 1.3. Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

1. Kubainisha namna wanaume wananyanyasika katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

2. Kutathmini athari za unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

3. Kufafanua mbinu wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji wao katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

### 1.4. Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

1. Unyanyasikaji wa wanaume umedhihirishwaje katika hadithi fupi teule za Kiswahili?
2. Athari zipi za unyanyasikaji wa wanaume zinabainika katika hadithi fupi teule za Kiswahili?
3. Mbinu zipi wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji wao katika hadithi fupi teule za Kiswahili?

### 1.5. Sababu za Kuchagua Mada

Mada hii ilichaguliwa kwa kuzingatia ukweli kwamba wanaume ni wahusika muhimu katika jamii yoyote. Ni vyema kuelewa kuwa ingawa wanaume huchorwa kama viumbe walio na nguvu na ukakamavu, pia wao hukabiliwa na changamoto kama vile kudhalilishwa, kudhulumiwa na kushushwa hadhi.

Utafiti wa Ruto (2015) ulipendekeza uchunguzi ufanywe ili kuangalia upande wa pili wa masuala ya uana kwa kuwa mengi yametafitiwa juu ya masuala yanayohusiana na jinsia ya kike. Hivyo, mapendekezo haya yalikuwa kichocheo cha utafiti huu kufanywa ili kueleza kwa kina namna wanaume hunyanyasika, kutathmini athari za unyanyasikaji na namna ambavyo wanaume hupambana dhidi ya unyanyasikaji. Ijapokuwa hili ni suala linalowaathiri wanaume katika jamii, halijaweza kuchunguzwa kwa kina katika tafiti za awali. Kwa kuwa fasihi huwasilisha mambo halisi yanayotendeka katika jamii, mtafiti aliteua mada iliyojikita katika utanzu wa hadithi fupi. Katika hadithi teule, waandishi husika walimsawiri mwanamume kwa njia mbalimbali zilizodhihirisha unyanyasikaji wake na kuchochea uchunguzi wa suala hili katika utafiti huu.

### 1.6. Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu katika kuhamasisha umma kuhusu unyanyasikaji wa wanaume na athari za unyanyasikaji huo. Jamii itapata uelewa zaidi kuhusu kunyanyasika kwa jinsia ya kiume. Itafahamu zaidi kuwa wanaume hunyanyasika na kuathirika kisaikolojia, kihisia na hata kimwili kama ilivyo kwa jinsia ya kike.

Vilevile, waandishi wa fasihi watanufaika na utafiti huu kwa kuwawezesha kutambua aina mbalimbali za unyanyasikaji wa wanaume. Waandishi hawa watahamasishwa pia kuhusu nafasi ya fasihi kama chombo cha kuyafichua maovu yanayoiathiri jamii na kupendekeza suluhu.

Pia, utakuwa wenye manufaa kwa wanaharakati wa haki za wanaume nchini na kimataifa kwa kuwasaidia kuelewa mchango wa fasihi ya Kiswahili katika kuangazia suala la unyanyasikaji wa wanaume.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yatasaidia tafiti za baadaye. Utafiti mwingine kuhusu unyanyasikaji wa wanaume unaweza kufanywa katika utanzu wa tamthilia na ushairi, hivyo, utafiti huu unaibua pengo la utafiti wa baadaye.

### 1.7. Upeo na Mipaka

Utafiti huu uliangazia suala la unyanyasikaji wa wanaume katika diwani teule za fasihi ya Kiswahili. Ulijikita katika diwani mbili ambazo ni: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016) iliyo na hadithi kumi na tatu (13) na *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine* (2012) iliyo na hadithi kumi na moja (11). Kati ya hadithi hizi kumi na tatu za *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, hadithi tano ziliteuliwa ambazo ni: Mapenzi ya Kifaurongo, Masharti ya Kisasa, Ndoto ya Mashaka, Tulipokutana Tena na Nizikeni Papa Hapa. Katika *Diwani ya Maskini Milionea*, hadithi mbili ziliteuliwa ambazo ni: Haramu Tamu na Tafrija Kambini. Mtafiti aliteua hadithi hizi mbili kwa kuwa waandishi wake walimsawiri mwanamume akiwa katika hali ya kunyanyasika hivyo kuwa faafu kwa utafiti huu**.** Vilevile alichagua diwani hizi kwa kuwa suala hili halijatafitiwa katika utanzu wa hadithi fupi ambao ni utanzu wa hivi karibuni na falsafa na msimamo wa waandishi wake ulikuwa unashadidia yaliyopo katika jamii ya leo kuhusu unyanyasikaji wa wanaume. Mtafiti alijikita tu kwa maudhui ya unyanyasikaji wa wanaume wala si mengine kwa sababu ni njia moja dhabiti ya

kuwakilisha kundi linalosahaulika mara nyingi na kukuza tafakari ya kina kuhusu dhana ya unyanyasikaji.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1. Utangulizi

Sehemu hii ilishughulikia maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Mtafiti ameyaeleza yafuatayo katika sura hii: dhana ya jinsia, na unyanyasikaji wa wanaume. Mtafiti pia ameeleza tafiti za awali kuhusu namna wanaume hunyanyasika, athari za unyanyasikaji wa wanaume na mbinu wanazotumia kupambana dhidi ya unyanyasikaji. Nadharia ya utafiti pia imefafanuliwa.

## 2.2. Dhana ya Jinsia

Jinsia ni dhana ya kijamii na kitamaduni inayobainisha majukumu, tabia, matarajio na utambulisho unaoonekana kufaa kwa mtu kulingana na jinsi anavyoonekana kama mwanamume au mwanamke. Jinsia huundwa na jamii, utamaduni na historia na inaweza kubadilika kutegemea muda na mazingira UNESCO (2023). Tofauti na jinsia ya kibayolojia, jinsia huundwa kupitia desturi za kitamaduni na taasisi za jamii (Haslanger, 2024).

## 2.3. Unyanyasikaji wa Wanaume

Kwa mujibu wa Bahemu (2021), unyanyasikaji wa kijinsia unapozungumziwa wengi huuwaza kwa upande mmoja, kwamba ni dhidi ya mwanamke. Hata hivyo, uhalisia ni tofauti kwani hata wanaume hunyanyasika isipokuwa si wepesi wa kuzungumza. Maelezo ya Bahemu yalitolewa wakati wa kongamano la kupinga ukatili wa kijinsia lililoandaliwa na Norwegian Church Aid (NCA) mkoani Manyara. Alisema haya wakati wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia. Kongamano hilo lilihudhuriwa na viongozi wa dini, mwakilishi wa kamanda wa polisi, wanaharakati, wazee na viongozi wa serikali. Katika kongamano hilo mwakilishi wa kamanda wa polisi alisema kuwa wanaume hunyanyasika isipokuwa baadhi yao huwa hawasemi. Vilevile alieleza kuwa katika kupambana na unyanyasikaji wa kijinsia, jeshi la polisi lilianzisha vituo vya huduma vya kijinsia. Aliendelea kufafanua kuwa wanapotafakari kuhusu jambo hili la unyanyasikaji, wasifikiri ni la watoto na wanawake tu; hata miongoni mwa wanaume, wapo wanaoogopa kujieleza kutokana na waliyoyashuhudia kwenye hivyo vituo vya kijinsia. Hivyo, hili lilimchochea kushauri kuwa wasiangazie upande mmoja tu.

Kulingana na Alberta (2011), unyanyasikaji hudhihirika katika ndoa ambapo mpenzi mmoja hutawala, kuonea au kudhalilisha mwingine. Unyanyasikaji wa kihisia ni kuvunja mtu moyo, kudhibiti fedha, kumtenga mpenzi na kuzuia uhuru wake wa kibinafsi. Unyanyasikaji wa kimwili ni pamoja na shughuli yoyote ambayo inaweza kusababisha maumivu ya kimwili au majeruhi. Unyanyasikaji wa kijinsia ni pamoja na kutumia nguvu ili kumpata mpenzi kwa njia zisizo za haki, kukejeli au kukosoa utendaji wake na kumnyima mapenzi. Kutumia vitisho pia ni aina ya unyanyasaji ambapo mpenzi hutumia maneno au matendo kumtishia mwenzake kama vile: kuharibu mali na kumtia mtu hofu.

### 2.4.1. Utafiti wa Awali Kuhusu Namna Wanaume Hunyanyasika

Kama anavyosema Amadiume (1987), mwanasosholojia kutoka Nigeria, alitafiti kuhusu jinsia katika jamii ya Kiafrika. Alichunguza miundo ambayo iliwawezesha wanawake kupata nguvu na akaonyesha kuwa majukumu hayakusemekana kuwa ya kike au kiume. Utafiti wake ulilenga jamii ya Igbo nchini Nigeria na uligawanywa katika vipindi vitatu: kipindi cha kabla ya ukoloni ambapo mifumo ya jadi ilitenda kazi, kipindi cha ukoloni ambapo Waingereza walitawala nchi ya Nigeria na kipindi cha baada ya ukoloni wakati nchi hiyo ilipata uhuru. Alisema kuwa wanawake walitekeleza majukumu ambayo, kwa kawaida, husemwa kuwa ni ya wanaume. Hivyo basi, wanawake wakaitwa 'wanaume'. Hili liliwezeshwa na hoja kuwa wanawake hawa walijitegemea kiuchumi na pia kulikuwepo na dini iliyowaangazia wanawake. Kujitegemea huku kwa kiasi fulani kulisababisha kunyanyaswa kwa wanaume. Suala la utafiti wake lilishabihiana na la huu kwa kuwa uliangazia jinsia na kudokeza jinsi unyanyapaa hudhihirika. Utafiti huu ulikuwa na manufaa katika kuelewa majukumu yanayosababisha kunyanyasika kwa wanaume. Hata hivyo, ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa huu uliangazia unyanyasikaji katika diwani za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wa Kenya. Hivyo, unyanyasaji uliodhihirika uliwakilisha hali halisi iliyo katika nchi ya Kenya kinyume na utafiti wa Amadiume uliofanyika kule Nigeria ambalo ni eneo tofauti la kijiografia. Utafiti wake uliangazia jamii ya Igbo kinyume na utafiti huu ulioshughulikia suala la unyanyasikaji wa wanaume kwa kurejelea wahusika mbalimbali katika kazi ya fasihi andishi.

Utafiti uliofanywa na Chaterji (2004), kuhusu mabadiliko katika mfumo wa kuumeni akizingatia jamii ya Wahindi ulibainisha kuwa majukumu ya wanawake katika jamii hiyo yamebadilika mfululizo katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Hapo awali, jambo hili halikupewa kipaumbele. Pia anatoa mifano ya mabadiliko ya majukumu ya wanawake na wanaume. Anaeleza kisa cha wanawake watano waliodaiwa kumwua jambazi sugu. Vilevile, mtu aitwaye Yadau alidungwa kisu na kupigwa kwa mawe na kundi la wanawake. Aidha, Chaterji anaonyesha athari ya mabadiliko ya kiuana hasa katika mahusiano kama ndoa yaliyosababishwa na maendeleo ya wanawake katika masuala ya kijamii, kiuchumi, kimawazo na kisiasa duniani kote. Wanaume huona vigumu kuishi na wanawake wa sampuli hiyo kwa kuwa wanawanyanyasa. Utafiti wa Chaterji unahusiana na utafiti huu kwani ulishughulikia masuala ya kijinsia kama ilivyochunguzwa katika utafiti huu. Utafiti wake ulichangia huu kwa kudokeza namna mabadiliko ya kimajukumu husababisha kunyanyasika kwa mwanaume. Utafiti wake ulitofautiana na huu kwa kuwa wake uliangazia mabadiliko ya mfumo wa kuumeni kwa kuzingatia jamii ya wahindi. Kinyume na utafiti wake, utafiti huu uliangazia unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi fupi zilizoandikwa na waandishi wa Kenya.

Utafiti uliofanywa na Gitau (2011) kuhusu unyanyasaji dhidi ya wanaume katika fasihi ya Kiswahili ulibainisha kuwa wanaume hukabiliwa na unyanyasaji wa kutukanwa na wake zao, wanawake wengine au wanaume wengine. Mara nyingi matusi haya hutokana na yale majukumu aliyopewa mwanamume na jamii kama mtoa riziki wa familia. Alisema pia wanaume hukabiliwa na unyanyasaji wa kutengwa na familia zao. Katika tamadumi za Kiafrika, watoto ni muhimu kwa sababu huendeleza uhai wa jamii husika. Mwanamume hupewa jukumu la kukidhi mahitaji wa familia, kuwatunza wazazi na wanajamii wengine ambao ni wa aila yao. Jambo hili huleta mafarakano kati ya mume na mke kwani mke haoni kwa nini mumewe akidhi mahitaji ya aila yake na hali ana familia yake mwenyewe. Vilevile hunyanyasika kutokana na kudharauliwa na wake zao au wanajamii wengine hasa wanaposhindwa kutekeleza wajibu wao. Unyanyasaji huu huumiza wanaume kwa kuhisi kuwa wao si wanaume kamili kama wanaume wengine. Utafiti huu ulikuwa na manufaa mengi kwa kuwa ulisaidia kuelewa namna wanaume hunyanyasika katika jamii. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa uliangazia unyanyasaji wa wanaume kwa kuelekezwa na nadharia ya Umuundo-Utekelezaji ilhali utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mtagusano wa

Vitambulisho. Gitau alishughulikia fasihi ya Kiswahili kwa jumla ilhali huu ulijikita katika utanzu wa hadithi fupi pekee.

Matokeo ya utafiti uliofanywa na Laititi (2005) kuhusu unyanyasaji wa wanaume waliostaafishwa mapema ulibainisha kuwa visa vya wanawake kuwanyanyasa wanaume wao viliongezeka. Alibainisha kuwa baadhi ya wanaume waliofutwa kazi walitumikishwa na wake zao ambao walichukulia kuwa mwanamume asiye na uwezo kiuchumi hana hadhi katika familia. Baadhi ya wanawake hawa waliwaachia wanaume wao kazi za nyumbani na wengine hukataa kuandamana nao katika kumbi za starehe na badala yake kuandamana na wanaume wengine walio na hadhi ya juu kama wao. Ingawa utafiti huu si wa kifasihi, ulichangia katika kuielewa mada hii na kuelewa changamoto wanazokumbana nazo wanaume. Utafiti wake ulitofautiana na huu kwa kuwa wake ulilenga wanaume waliostaafishwa mapema ilhali huu uliangazia kwa upana unyanyasikaji jinsia ya kiume, kuanzia watoto hadi watu wazima. Isitoshe, utafiti huu ulijikita katika kazi ya fasihi, hasa utanzu wa hadithi fupi kinyume na utafiti wake ulioangazia unyanyasaji wa wanaume kwa kurejelea wajamii halisi.

Ruto (2005), alifanya utafiti juu ya matatizo ya mwanamke katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea na Nguzo za Mama*. Alisema kuwa jamii nyingi za Kiafrika huchukulia mwanamke kama kitega uchumi. Kabla ya kuolewa ni lazima mahari ilipwe kama dhamana na hili husababisha wasichana kuozwa mapema hivyo kunyanyaswa kwa kudharauliwa. Mwanamke ana haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa kwani anachangia katika maendeleo na kuchuma mali katika jamii. Dharau inajitokeza pale ambapo mke anakosa kuthaminiwa, kuvunjiwa heshima na kuaibishwa kupitia vitendo kama vile kubakwa, kutawishwa na kuelekezewa lugha isiyo ya heshima. Kutawisha ni hali ya kufungia mtu ndani ya nyumba ili asitoke nje kuingiliana na wanajamii wengine. Utafiti wake unahusiana na huu kwani ulishushughulikia suala la kijinsia na kudhihirisha namna jinsia ya kike hunyanyasika. Hata ingawa utafiti wake ulichangia huu, unatofautiana kwa kuwa huu uliangazia upande mwingine wa kijinsia. Ruto alijikita zaidi kwa jinsia ya kike ilhali huu ulijifunga katika kuchunguza unyanyasikaji wa jinsia ya kiume kwa kuelekezwa na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho.

Kwa mujibu wa Kausi (2021) kuhusu dhuluma za kitabaka katika riwaya ya Kiswahili ambapo wahusika wa tabaka la juu ambao ni waajiri huwadhulumu waajiriwa wa tabaka la chini. Dhuluma hizi ni kama vile: kudunishwa, kutukanwa, kupigwa kikatili, kudhulumiwa kimapenzi na kisaikolojia na kubaguliwa kwa misingi ya rangi kama ilivyokuwa wakati wa mkoloni. Mifumo yote ya kisiasa, kiuchumi na kijamii iliongozwa na ubaguzi. Hali hii imechangia migogoro ya kimawazo miongoni mwa wahusika wanyonge. Utafiti huu ulikuwa na manufaa kwani ulisaidia kuelewa aina mbalimbali za dhuluma zinazoelekezewa watu wa tabaka la chini. Utafiti wake una uhusiano na huu kwa kuwa ulibainisha dhuluma za kitabaka zinazoleta hali ya unyanyasikaji katika jamii. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na hii kwa kuwa hii iliangazia unyanyasikaji wa wanaume katika utanzu wa hadithi fupi ilhali yake ilichunguza kuhusu dhuluma za kitabaka katika katika riwaya ya Kiswahili.

### 2.4.2. Athari za Unyanyasikaji wa Wanaume

Kulingana na APA (1892), unyanyasaji wa wanaume ni suala linaloweza kuwa na athari mbaya kwa watu binafsi na jamii kwa ujumla. Baadhi ya athari za unyanyasaji wa wanaume ni kama zifuatazo: madhara ya kihisia, majeraha, kifo, madhara ya kijamii na kisaikolojia. Madhara haya huathiri ujasiri wao na mtazamo wao wa maisha kwa ujumla. Kazi hii ina manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa ilisaidia kuelewa namna wanaume hunyanyasika na wanavyopigana dhidi yake Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa huu uliangazia unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi fupi teule. Nadharia iliyokuwa kielelezo cha uchunguzi uliofanywa na wanasaikolojia hao ni nadharia ya Majukumu ya Kijinsia. Katika utafiti huu, nadharia tofauti ilitumika ambayo ni nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho.

Utafiti uliofanywa na Gitau (2005) kuhusu unyanyasaji wa wanaume katika riwaya za Kiswahili ulieleza athari za unyanyasaji wa wanaume. Utafiti wake ulibainsha kuwa wanaume wanaathirika kwa njia kama vile: kuvumilia mateso na kunyamaza, kuzua vita, kutoroka nyumbani kwao, kukimbilia dini na kutumia razini. Wanapokumbana na unyanyasaji kutoka kwa wanawake, huwa wanatumia maneno ili kuwafanya wanawake waelewe msimamo wao juu ya jambo fulani. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa makubwa kwa kuwa ulieleza kwa kina jinsi wanaume wanavyoathirika kupitia unyanyasaji. Tofati iliyodhihirika ni kuwa utafiti wake uliangazia athari za unyanyasaji wa wanaume katika riwaya na tamthilia za Kiswahili ilhali huu uliangazia

athari za unyanyasikaji wa wanaume katika utanzu wa hadithi fupi. Pia, Gitau alitumia nadharia ya umuundo-utekelezi ilhali utafiti huu ulielekezwa na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho.

Kwa mujibu wa Mwangi (2018), mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya za Said Mohamed *Utengano (1980)* na *Dunia Yao (2006)* huwa na athari kwa mwanamume. Alieleza athari hizi kama kudorora kwa maadili. Alisema kutokana na mabadiliko ya kijamii hasa ujio wa utandawazi, tamaduni na maadili ya kigeni yaliingizwa katika bara la Afrika. Maadili yaliyokuwa yakihimizwa katika jamii za kiafrika tangu zama za mababu yametokomea na kutupwa katika kaburi la sahau. Kukosa maadili kunasababisha watoto kutoheshimu wazazi wao, kushiriki usherati na kutumia dawa za kulevya. Alieleza athari zingine kama vile: ukosefu wa kazi na athari zake, kukata tamaa maishani, kukita mizizi kwa ukoloni mamboleo na malezi. Utafiti huu ulikuwa na faida kwa kuwa ulisaidia kupata uelewa zaidi kuhusu athari za unyanyasikaji wa wanaume. Hata hivyo ulitofautiana na huu kwa kuwa wake uliangazia athari hizi katika riwaya za Kiswahili ilhali huu uliangazia athari hizi katika diwani teule za Kiswahili.

Nzonga (2020) alitafiti kuhusu mgao mpya wa kazi za wanaume katika hadithi fupi za Kiswahili. Alieleza kuwa athari za mgao mpya wa kazi za wanaume kwa kuziweka katika makundi yenye sifa zinazofanana. Alieleza hadithi zilizodhihirisha athari mahususi kwa wanaume katika utekelezaji wa mgao mpya wa kazi za mwanamume. Alisema mgao mpya wa kazi za wanaume huleta athari kama vile: kuongeza mapenzi, kuleta ushirikiano baina ya mwanamume na mwanamke, kusababisha utoshelevu wa moyoni, kuleta ufanisi katika maisha ya mwanamume, kumfanya mwanamume kujiona wa maana katika familia yake na wakati mwingine kusababisha mikinzano. Kazi hii ina manufaa kwa kuwa ilisaidia kuelewa athari za mgao wa kazi kwa mwanamume ambazo hudokeza kunyanyasika kwake. Hata hivyo kazi yake inatofautiana na hii kwa kuwa hii iliangazia unyanyasikaji wa wanaume katika diwani teule za Kiswahili ilhali wake ulishughulikia mgao mpya wa kazi za wanaume bila kuweka wazi na kwa kina suala ya unyanyasikaji.

### 2.4.3. Mbinu Wanazotumia Wanaume Kupambana Dhidi ya Unyanyasikaji

Kelvin (2019) alielezea kwa nini wanaume hukaa kimya wanapofanyiwa unyanyasaji. Alisema kuwa kiongozi mmoja aliyewahi kufanyiwa unyanyasaji wa kingono alikuwa akiwasikiliza wanaume ambao walipitia unyanyasaji wa aina hiyo wakitaka suala lao liangaliwe kwa ukaribu. Kiongozi huyo alisema kuwa wanaume walioathirika na unyanyasaji wa kijinsia wakiwa watoto katika jamii ya watu weusi wamekuwa wakirudishwa nyuma na serikali. Aliendelea kusema kuwa mhusika mmoja aliyenyanyaswa alisema kuwa alijaribu kusahau aliyotendewa akashindwa. Vilevile alijaribu kuendelea na maisha yake lakini kitendo hicho kilisalia akilini mwake. Kazi hii ina manufaa kwa kuwa ilisaidia katika kuelewa kuwa pia wanaume hunyanyasika katika jamii. Ilidokeza baadhi ya mbinu wanazotumia wanaume kupigana dhidi ya unyanyasikaji kama kunyamaza na kuvumilia. Hata hivyo kazi yake ni tofauti na hii kwa kuwa hii iliangalia unyanyasikaji wa wanaume kwa jumla kwa kuzingatia utanzu wa hadithi fupi ilhali wa Kelvin ulichunguza suala la unyanyasaji, hasa wa kingono.

Utafiti uliofanywa na Kausi (2021) ulibainisha mbinu wanazotumia wanyonge dhidi ya dhuluma za kitabaka. Mbinu hizi zilizoangazia namna wahusika wanyonge wanavyojikomboa ni kama vile: kufanya maandamano na migomo ya wafanyikazi, kuelimisha wahusika wanyonge, kuanzisha biashara ili kujikimu kimapato na uandishi wa vitabu vya fasihi kama vile tamthilia. Hili hufanywa ili kuwazindua wanajamii kwa kumulika dhuluma zinazowakumba wahusika wa tabaka la chini. Utafiti huo ulikuwa na manufaa kwa kuwa ulisaidia kuelewa mbinu zilizotumiwa na wanyonge waliponyanyaswa. Hata hivyo utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa huu ulitumia nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho ilhali wake ulirejelea nadharia ya Uhakiki ya Ki- Marx. Isitoshe, vyanzo vya data vilitofautiana kwani kwa utafiti wa Kausi, riwaya ilitumika ilhali kwa kwa utafiti huu hadithi fupi zilitumika.

Matokeo ya utafiti uliofanywa na Mwangi (2022) kuhusu changamoto zilizowakumba vijana katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ulibainisha mbinu walizotumia vijana kujikomboa. Licha ya kuwa vijana wengi wanakumbwa na changamoto chungu nzima katika tamthilia hii, wanaibuka na mbinu anuwai za kukabiliana na matatizo kama vile: kushikilia msimamo wao, kudhihirisha ukakamavu, kutoa vitisho na kuzinduka na kufutilia mbali mila kandamizi. Kwanza

vijana wanaushikilia msimamo wao wa kuoa wanaowapenda na kukataa kata kata shinikizo la wazazi wao kuwachagulia wapenzi wa kuoa. Kutokana na msimamo dhabiti wao, wazazi wao hulegeza msimamo wao kuhusu uhuru wa kujichagulia wachumba. Vijana wanadhihirisha ukakamavu kutokana na jinsi wanavyojaribu kuwashawishi wazazi wao kuitikia uamuzi wao. Utafiti huu ulikuwa na manufaa kwa kuwa ulisaidia kuelewa mbinu zinazotumiwa na vijana katika kukabiliana na unyanyasaji. Hata hivyo, ni tofauti na huu kwa kuwa huu uliangazia mbinu zinazotumiwa na wanaume kupigana dhidi ya unyanyasikaji bali si vijana tu.

Karinge (2013) alitafiti kuhusu usawiri wa ndoa katika riwaya ya *Unaitwa nani?* iliyoandikwa na K.W.Wamitila (2008). Katika utafiti wake, alieleza mikakati ya kuiokoa asasi ya ndoa. Alieleza kuwa ingawa asasi ya ndoa inakabiliwa na changamoto zinazotishia kuisambaratisha, baadhi ya mikakati inayotumiwa au kutajwa na wahusika inaweza kuchangia kwa njia chanya kuiokoa asasi hii. Mbinu hizi ni kama vile: uwazi wa mawasiliano, ushauri nasaha, matibabu yanayofaa, msamaha, uvumilivu, uelewano na ushirikiano, Utafiti huu ulifaidi pakubwa kwa kuwa uliwezesha utambuzi wa mbinu zaidi zilizotumiwa kuiokoa asasi ya ndoa. Hata hivyo, ulitofautiana na huu kwa kuwa wake ulitumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ilhali huu ulitumia nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho. Isitoshe, Karinge aliangazia riwaya ilhali huu ulijikita katika utanzu wa hadithi fupi.

Kulingana na John na Brown (2018), mbinu za kujitafakari na kujifunza mikakati ya kukabiliana na msongo wa mawazo ni muhimu sana kwa wanaume wanaopitia unyanyasaji. Mbinu hizi husaidia wanaume kuelewa hisia zao, kupunguza kuvurugika kwa moyo na kuimarisha ustawi wa kisaikolojia. Kupitia mbinu hizi, wanaume hujenga nguvu za kukabiliana na changamoto hizo. Hali hii inawezesha kujijenga upya kiakili na kihisia baada ya uzoefu mgumu wa unyanyasaji. Utafiti wa John na Brown unahusiana na huu kwani ulitambua mbinu mbili za kujinasua kutokana na unyanyasaji wa wanaume. Mbinu hizi zilidokeza hoja kuhusu namna wanaume hupigana dhidi ya unyanyasikaji kama ilivyochunguzwa na utafiti huu. Tofauti na utafiti wake uliochunguza mbinu hizi kwa jumla, utafiti huu ulitafiti mbinu walizotumia wanaume kupigana dhidi ya unyanyasikaji katika hadithi fupi teule za *Diwani za Masikini Milionea* na *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.* Mwongozo wa nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho ulitumika.

## 2.5. Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho iliyoasisiwa na Kimberle Crenshaw (1989). Ni mojawapo ya nadharia za kijinsia. Nadharia ya kijinsia haihusu tu kutetea haki za wanawake. Inaweza kufaa kwa kuchanganua unyanyasikaji wa wanaume hasa wakati uchanganuzi unahusu matarajio ya kijinsia na mifumo ya mamlaka. Nadharia hii ni mfumo unaochunguza jinsi mamlaka, majukumu ya kijinsia na miundo ya kijamii inavyounda uzoefu kwa jinsia zote. Mitazamo mingi ya kijinsia kama vile Mtagusano wa Vitambulisho na ufeministi wa baada ya muundo hukagua jinsi ubabedume hudhuru kila mtu katika jamii.

Kimberlé Crenshaw ni mwanasheria na msomi wa masuala ya haki za kiraia. Aliitambulisha nadharia hii rasmi mnamo 1989 katika makala yake, *the Intersection of Race and Sex*, ambapo alieleza jinsi wanawake weusi walivyokumbwa na aina tofauti za ubaguzi ambazo haziwezi kueleweka kwa kutumia mtazamo mmoja tu wa jinsia au mbari.

Crenshaw alianzisha nadharia hii ili kueleza jinsi mifumo ya ukandamizaji inavyoshirikiana na kuathiri watu kwa njia mbalimbali. Alieleza kwamba, sheria na harakati za kijamii zilikuwa zinashughulikia ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kijinsia kama mambo tofauti bila kuzingatia jinsi mtu anavyoweza kukumbwa na aina zote mbili za ubaguzi kwa wakati mmoja. Alitoa mfano kuwa, wanawake Waafrika walikuwa wakikumbwa na changamoto ambazo zilikuwa tofauti na zile zinazowakumba wanawake wa rangi nyingine au wanaume weusi. Hivyo, Crenshaw alisisitiza kwamba ukandamizaji hauwezi kuchambuliwa kwa kutenganisha vipengele vya utambulisho wa mtu bali kwa kuzingatia jinsi vinavyoshirikiana na kuathiriana. Nadharia hii hutumika katika jamii za kisasa kwa njia mbalimbali, hasa katika masuala ya haki za kijamii, sera za umma, na harakati za kijamii.

Patricia Hill Collins (1990) alichangia nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho kupitia kitabu chake cha *Black Feminist Thought*. Katika kitabu hiki, alianzisha dhana ya matriki ya utawala ambayo inaeleza jinsi vipengele vya utambulisho kama jinsia, rangi, na tabaka vinavyoathiriana na kuunda mifumo ya ukandamizaji. Collins alipanua nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho kwa kuonyesha jinsi wanawake weusi wanavyokabili ukandamizaji wa kimfumo kwa njia tofauti na wanawake wa

jamii nyingine. Alisisitiza umuhimu wa kuzingatia mwingiliano wa vipengele vya utambulisho katika uchambuzi wa kijamii.

Lorde (1984) alichangia nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho hasa kupitia maandiko yake ya kifeministi na kijamii. Ingawa hakutumia neno mtagusano moja kwa moja, alizungumza kwa kina kuhusu maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi na jinsi vinavyoathiri uzoefu wa ukandamizaji au ukosefu wa haki. Kazi yake muhimu, *Sister Outsider: Essays and Speeches* (1984), ilichangia katika kuelewa jinsi vipengele vya utambulisho kama vile jinsia na rangi vinavyoathiriana na kuunda ukandamizaji.

Katika maandiko yake, Lorde alisisitiza kuwa ukandamizaji hauwezi kuchunguzwa kwa mtazamo mmoja tu, bali unapaswa kuzingatia mwingiliano wa vipengele vyote vya utambulisho wa mtu. Kauli yake maarufu, *"The master's tools will never dismantle the master's house,"* ilihimiza harakati za kijamii kutambua na kushughulikia mifumo ya ukandamizaji kwa mtazamo mpana.

Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho ina mihimili kadhaa inayosaidia kuelewa jinsi vipengele mbalimbali vya utambulisho wa mtu vinavyoshirikiana na kuathiri jamii. Mihimili hii ni msingi wa uchambuzi wa ukandamizaji na upendeleo katika jamii.

1. Mwingiliano wa vipengele vya utambulisho: nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho inasisitiza kwamba mtu anaweza kuwa na utambulisho zaidi ya mmoja, kama vile jinsia, rangi, hadhi, mwelekeo wa kijinsia, na ulemavu. Vipengele hivi vinaposhirikiana vinaweza kuathiri jinsi mtu anavyoelekezewa upendeleo au ukandamizaji katika jamii. Mhimili huu ulitumiwa kuonyesha kuwa wanaume hunyanyasika kwa sababu ya kipengele cha jinsia na mwelekeo wa kijamii.
2. Ukandamizaji wa Kimuundo. Nadharia hii inaeleza jinsi mifumo ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi inavyoweza kuendeleza ukandamizaji kwa watu wenye utambulisho tofauti. Mfumo wa sheria, elimu, na ajira unaweza kuwa na upendeleo unaoathiri makundi fulani kwa njia tofauti. Mhimili huu ulitumiwa kuonyesha kuwa sababu za kiuchumi husababisha wanaume kunyanyasika.
3. Uzoefu wa Kipekee wa Ukandamizaji. Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho inaonyesha kuwa watu wenye utambulisho tofauti

wanakumbwa na changamoto za kipekee ambazo haziwezi kueleweka kwa kutumia mtazamo mmoja tu wa ukandamizaji. Kwa mfano, mwanamke mweusi anaweza kukumbwa na changamoto ambazo ni tofauti na zile zinazowakumba wanawake wa rangi nyingine au wanaume weusi.

4. Uwakilishi na Sauti ya Makundi ya Kijamii. Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kuwapa nafasi watu kutoka makundi yaliyotengwa ili waweze kueleza uzoefu wao wenyewe. Uwakilishi katika vyombo vya habari, siasa, na elimu unapaswa kuzingatia mwingiliano wa vipengele vya utambulisho.
5. Mabadiliko ya Kijamii na Haki. Mtagusano wa Vitambulisho unahimiza mabadiliko ya kijamii kwa kuhakikisha kwamba sera na sheria zinazingatia mahitaji ya watu wenye utambulisho tofauti. Harakati za kijamii zinapaswa kujumuisha mtazamo wa Mtagusano wa Vitambulisho ili kuhakikisha kwamba zinawakilisha makundi yote kwa usawa.

Nadharia hii inahusu jinsi mifumo ya mamlaka inavyoingiliana ili kuunda uzoefu. Ingawa ilitokana na nadharia ya ufeministi na uhakiki wa kushughulikia utengano wa wanawake wa rangi tofauti, haikomei tu katika kuchanganua uzoefu wa wanawake pekee. Inaweza kutumika kueleza jinsi vipengele tofauti vya utambulisho kama vile rangi, tabaka, jinsia, uwezo, dini, au hali ya uhamiaji vinaathiri wanaume pia.

Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho inawahusu wanaume kwa namna zifuatazo**:**

1) Wanaume weusi na idara ya usalama: wanaume weusi wanaweza kukabiliwa na vurugu kutokana na utambulisho wa rangi na jinsia. Kwa mfano, dhana potofu za uhalifu na uume kupita kiasi.
2) Mashoga wanaweza kukumbana na shinikizo la kijamii linalowataka kufuata dhana za uanaume za kitamaduni, huku wakikabiliwa na ubaguzi wa kijinsia na mwelekeo wa kimapenzi.
3) Wanaume maskini: daraja lao linaingiliana na jinsia ili kuunda masuala kama vile: ukosefu wa ajira, upatikanaji wa elimu na huduma ya afya. Wanaume wa tabaka la chini wanaweza kunyanyaswa au kupuuzwa katika mijadala fulani ya sera za umma.
4) Wanaume wenye ulemavu: wanaweza kukumbana na ubaguzi tofauti na wanawake walemavu kutokana na matarajio ya kijamii kuhusu uanaume, uhuru, na tija.

5) Wanaume wahamiaji au wakimbizi wanaweza kuwa waathirika wa unyanyapaa, kutengwa, au matarajio yasiyowezekana kutokana na mikutano ya vitambulisho vyao mbalimbali. Hivyo basi, si kila mwanaume aliye mamlaka katika jamii. Wengine ni waathirika wa mfumo kandamizi.

### 2.6 Hitimisho

Sehemu hii imeangazia dhana ya jinsia. Vilevile, unyanyasikaji wa wanaume kulingana na tafiti za awali umeelezwa. Utafiti umehakiki kazi za awali kuhusu namna wanaume hunyanyaswa, athari zake na mbinu wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji huo. Mwishowe, nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho imefafanuliwa kwa kurejelea waasisi wake, mihimili, na matumizi yake katika uhakiki wa fasihi.

# SURA YA TATU
# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1. Utangulizi

Sura hii imefafanua vipengele vifuatavyo: mbinu za utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na maadili ya utafiti.

## 3.2. Mkabala wa Utafiti

Muundo uliotumiwa katika utafiti huu ni wa kimaelezo. Kothari (2004) anasema utafiti wa kimaelezo ni mtazamo ambao huchunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa. Nia yake huwa kuchunguza jinsi mambo yalivyo katika mazingira. Lengo kuu katika muundo huu ni kukusanya data na kueleza uhusiano wa vipengele mbalimbali vya data hiyo. Kulingana na Derry-Vick (2023), muundo huu hulenga zaidi kufafanua, kueleza, na kupima jambo au tajiriba. Kwa mujibu wa Khaisie na wenzake (2018), kueleza na kufafanua huku hutegemea data inayopatikana. Hivyo, muundo huu ulitumika kueleza hali halisi ya unyayasikaji wa wanaume kwa kutumia data iliyopatikana kwenye hadithi za diwani teule.

## 3.3. Eneo la Utafiti

Kulingana na Creswell (2014), eneo la utafiti ni mahali mahususi, muktadha, au taaluma ambayo mtafiti hufanyia uchunguzi wa kimfumo ili kushughulikia tatizo fulani. Utafiti huu ulifanyika katika maktaba Chuo Kikuu cha Embu, Chuka na Kenyatta ambapo mtafiti alichambua kwa kina Diwani mbili za Kiswahili ambazo ni: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* na *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine.* Kupitia usomaji wa kina wa hadithi katika diwani hizi, mtafiti alipata data ya utafiti huu. Isitoshe, katika maktaba hii, mtafiti alisoma mitandaoni makala yanayohusiana na mada na nadharia iliyoongoza utafiti huu.

## 3.4. Walengwa

Utafiti ulilenga utanzu wa hadithi fupi. Mtafiti alichanganua hadithi tano katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* na hadithi mbili katika *Diwani ya Maskini Milionea na Hadithi Nyingine*. Mtafiti aliteua utanzu wa hadithi fupi kwa

misingi kuwa suala la unyanyasikaji wa wanaume halikuwa limechunguzwa katika utanzu huu. Vilevile utanzu huu uliafiki madhumuni ya utafiti ambayo yalikuwa kubainisha suala la unyanyasikaji, kutathmini athari za unyanyasikaji huu na kufafanua mbinu wanazotumia kupambana na unyanyasikaji huu. Isitoshe utanzu wa hadithi fupi ni utanzu wa hivi karibuni unaoangazia masuala nyeti na ibuka katika jamii. Msimamo wa waandishi wake ulikuwa unashadidia yaliyopo katika jamii ya leo kuhusu unyanyasikaji wa wanaume hivyo kuwezesha kupata data faafu.

### 3.5. Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi. Mugenda (2013) anasema kuwa uteuzi wa sampuli kimakusudi ni mbinu ambayo humruhusu mtafiti kuchagua sampuli itakayompa data anayohitaji kulingana na malengo ya utafiti wake. Sampuli iliyochaguliwa ni hadithi zilizoangazia suala la unyanyasikaji wa wanaume. Utafiti huu ulilenga vitabu mahususi ambavyo vina vipengele muhimu vya unyanyasikaji. Vitabu hivi ni Diwani za *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016) na *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine* (2012). Mtafiti aliteua diwani hizi mbili ili aweze kupata data ya kutosha. Mtafiti alisoma hadithi hizi na kuteua data ambayo ilihusiana na maswali na madhumuni ya utafiti. Hadithi mbili zilizoteuliwa katika *Diwani ya Masikini Milionea* ni: Haramu Tamu na Tafrija Kambini. Katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba,* hadithi tano ziliteuliwa ambazo ni: Mapenzi ya Kifaurongo, Masharti ya Kisasa, Ndoto ya Mashaka, Tulipokutana Tena na Nizikeni Papa Hapa. Sababu ya kuteua hadithi hizi ni kuwa zilidhihirisha suala la unyanyasikaji wa mwanamume na kuafikiana na madhumuni ya utafiti.

### 3.6. Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alisoma kwa kina hadithi fupi teule za *Diwani za Tumbo Lisiloshiba* na *Maskini Milionea*. Baada ya usomaji, mtafiti alikusanya data ya msingi kutoka kwenye maandishi na kuyanakili katika daftari**.** Data hii ilikuwa nukuu halisi za maneno, virai, vishazi na aya kutoka kwenye hadithi. Nukuu hizi zilitumika kama ushahidi wa kuchambua tatizo la utafiti. Kati ya zilizonakiliwa, mtafiti aliteua dondoo zilizodhihirisha unyanyasikaji wa wanaume na kuzipiga chapa kwenye kipakatalishi. Dondoo hizi alizipanga katika kategoria tatu. Kategoria ya kwanza ilihusu namna wanaume hunyanyasika katika hadithi fupi teule. Pili, alionyesha athari za

unyanyasikaji wa wanaume na tatu zilidhihirisha mbinu wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji. Isitoshe, mtafiti alitumia vitambulishi vya kipekee ili kusimba data. Nukuu/dondoo zilizotoka katika *Diwani ya Tumbo Lisioshiba na Hadithi nyingine* aliziita **TL** na za *Masikini Milionea na Hadithi Nyingine* zikatambulishwa kama **MM** ili kurahisisha uchanganuzi wa data.

### 3.7. Uchanganuzi wa Data

Baada ya kukusanya data iliyohusu unyanyasikaji wa wanaume na athari zake, mtafiti alichanganua data kulingana na madhumuni na maswali ya utafiti. Mtafiti alijadili unyanyasikaji wa wanaume na athari zake akiongozwa na mihimili ya nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini. Kulingana na Carney (1969) uchanganuzi matini ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti hupanga data kulingana na mada fulani ya utafiti. Mada hizi hujumuisha mambo ambayo yamo ndani ya matini na ambayo mtafiti anaweza kubainisha maana yake kutokana na matini inayoshughulikiwa. Mtafiti hugawa mada katika vijisehemu vinavyoweza kufasiriwa kwa urahisi. Baada ya kukusanya data na kuichanganua kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini, iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yalizingatia ufafanuzi wa unyanyasikaji wa wanaume katika diwani teule.

### 3.8. Maadili ya Utafiti

Mchakato mzima wa utafiti huu ulizingatia masuala ya kimaadili. Baada ya kupata kibali cha kukusanya data kutoka kwa Chuo Kikuu Cha Embu, mtafiti alipata idhini kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi-NACOSTI (NACOSTI/P/25/4175862). Mtafiti alizingatia maadili ya utafiti kwa kuhakikisha kuwa vyanzo vyote vya taarifa vimetambuliwa na kunukuliwa ipasavyo kwa kutumia mtindo wa APA. Kwa kuzingatia maadili ya utafiti, mtafiti alikiri mchango wa waandishi wa awali kwenye marejeleo, hivyo kuepuka wizi wa maarifa. Data iliyotumika ilitokana na vyanzo vya kuaminika vya kitaaluma. Hivyo, mchakato mzima ulidhihirisha ukweli, uwazi, na uaminifu wa kitaaluma bila kupotosha maana ya maandishi yaliyotumika. Kama alivyoeleza Zhaksylyk (2023), maadili huwawezesha wanasayansi kuaminiana wao kwa wao, kuthibitisha uaminifu wa

matokeo ya utafiti, na pia hutumika kama msingi wa imani ya umma kwa ushahidi wa kisayansi.

### 3.9 Hitimisho

Sehemu hii imeangazia muundo uliozingatiwa katika utafiti huu. Isitoshe, imefafanua kuhusu eneo la utafiti na kuweka wazi diwani zilizolengwa kuchambuliwa katika utafiti huu. Vilevile mtafiti ameeleza walengwa wa utafiti. Usampulishaji wa kimakusudi umeelezwa kulingana na namna ambavyo ulitumika katika utafiti huu. Pia, uwazi umewekwa kuhusu namna ambavyo ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake ulifanywa. Mwishowe, maadili yaliyozingatiwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa utafiti yameelezwa.

# SURA YA NNE
# MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1. Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu suala la unyanyasikaji wa wanaume na uchanganuzi wake kwa kuelekezwa na mihimili ya nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho.

## 4.2. Muundo wa Uchanganuzi

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuelekezwa na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho na kupangwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Mtafiti alidondoa maneno, virai, vishazi, sentensi na aya zilizodhihirisha unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi teule. Isitoshe, utathmini wa athari za unyanyasikaji wa wanaume ulifanyika katika hadithi teule. Pamoja na hayo, utafiti ulichambua mbinu mbalimbali ambazo wanaume hutumia ili kupigana dhidi ya unyanyasikaji huo. Vitambulishi vya kipekee vilitumika kuainisha dondoo. Kwa mfano, **MM** iliwakilisha *Maskini milionea*, **TL** ilisimamia *Tumbo Lisiloshiba* kisha **uk.** iliwakilisha ukurasa ambao dondoo hilo lilitolewa. Hadithi zilizochanganuliwa ni: *Mapenzi ya Kifaurongo, Masharti ya Kisasa*, *Ndoto ya Mashaka*, *Tulipokutana Tena*, *Nizikeni Papa Hapa, Haramu Tamu* na *Tafrija Kambini.*

## 4.3. Namna Wanaume Hunyanyasika

Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa wanaume hunyanyasika kwa njia zifuatazo:

### 4.3.1. Wake Kushiriki Mapenzi Nje ya Ndoa

Unyanyasikaji wa kwanza unaopitiwa na wanaume ni ule wa wake zao kutokuwa waaminifu na kushiriki mapenzi nje ya ndoa. Uaminifu ni mojawapo ya misingi muhimu sana katika maisha ya binadamu hasa katika mahusiano ya kijamii, kibiashara na kikazi. Ni msingi wa kuaminika, kutegemewa, na kujenga uhusiano wa kudumu wenye manufaa. Minja (2025) anasema kuwa uaminifu katika ndoa huwa na manufaa. Vilevile anasema uaminifu unapokosekana mikinzano hutokea. Kulingana naye, faida za uaminifu ni kama vile kujenga mahusiano imara, kuleta utulivu wa akili na furaha, kuaminika na kutegemewa na watu wengine, kupunguza migogoro na mivutano na kujenga mazingira bora ya kufanyia kazi. Uaminifu ni nguzo ya mahusiano yenye afya na thabiti, iwe ni katika familia, urafiki au mahusiano ya kimapenzi.

Mwandishi wa hadithi ya 'Haramu Tamu' katika *Diwani ya Maskini Milionea* amedhihirisha kuwa mwanamume ananyanyasika pale ambapo anaendewa kinyume na mkewe kama ifuatavyo.

> Kama alivyobashiri, alijibu na wakakubaliana kukutana katika mkahawa alioupendekeza Chaurembo mwenyewe viungani mwa mji. Alitambua kuwa alikuwa mke wa mtu, ndio sababu akataka wakutane katika mkahawa wa faragha, mbali na upeo wa macho ya wateja wengine (MM, uk. 84)

Sentensi, *Alitambua yeye ni mke wa mtu, ndio sababu akataka wakutane katika mkahawa wenye sehemu za faragha mbali na upeo wa macho ya wateja wengine*, inadhihirisha kuwa Chaurembo alishiriki mapenzi nje ya ndoa. Chaurembo hakutaka kuonekana na mwanamume asiyekuwa mumewe kwani wengi walifahamu kuwa alikuwa mke wa mtu. Hili linamfanya apendekeze wakutane katika hoteli ambapo hakuna yeyote angemfahamu. Kama Chaurembo hangekuwa na lolote la kuficha, hangeogopa kukaa katika hoteli ambapo watu wangemwona. Hivyo, ni wazi kuwa alikuwa akishiriki mapenzi nje ya ndoa na aliogopa kuonekana akiwa na mpenzi wake wa kando.

Mwandishi anaonyesha Karisa akinyanyasika kwa kukosa usingizi na amani kwa sababu ya mkewe kurejea usiku. Anasema:

> Moyo ulimpapa Chaurembo alipojipenyeza nyumbani mwake jioni hiyo. Kulikuwa na kimya kikuu. Isipokuwa taa za nje, ndani mlikuwa giza. Chaurembo akaamini Karisa mumewe alikuwa usingizini. "Umechelewa, mpenzi. Itakubidi upunguze kazi. Huu mji siku hizi usiku una wenyewe". (MM, uk. 86)

Sentensi *Umechelewa, mpenzi. Itakubidi upunguze kazi.* inaashiria kuwa Karisa alikuwa ananyanyasika kwa kuwa mkewe Chaurembo alikuwa akirejea nyumbani usiku wa manane. Karisa alinyanyasika kwa kuwa mwanamume. Unyanyasikaji huu ulitokana na yeye kutambua kuwa mkewe alikuwa akishiriki mapenzi ya nje ya ndoa.

Karisa hakuweza kupata usingizi kwa kuwa alihofia usalama wa mkewe. Alinyanyasika pia kwa kukosa amani na utulivu. Alimweleza mkewe kuwa, *Huu mji siku hizi usiku una wenyewe* kumaanisha kuwa kulikuwa na wahuni na ilikuwa hatari

yeye kutembea usiku. Alihofia kuwa jambo mbaya lingemtendekea mkewe. Hivyo, akamwonya dhidi ya kutembea usiku. Hili linaonyesha kuwa Karisa hakuwa na amani na alinyanyasika.

Kwa mujibu wa Crenshaw (1989), vipengele vya uchumi, jinsia, matarajio ya kijamii, utamaduni wa Kiafrika na ubabedume vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Karisa. Karisa anampa mkewe uhuru wa kufanya kazi ili kuchangia katika uchumi. Mkewe Chaurembo anaitumia nafasi hii vibaya na kuwa na mapenzi nje ya ndoa. Anaanza kurejea nyumbani akiwa amechelewa. Akiulizwa na mumewe kwa nini kachelewa anasema kuwa mikutano kazini ilikuwa mingi ilhali alikuwa na mpenzi wake wa kando wakichupa kutoka hoteli moja hadi nyingine. Kuchelewa huku kunamfanya Karisa kunyanyasika Jambo hili ni kinyume na matarajio ya kijamii kwani mke hafai kutembea usiku. Pia kulingana na utamadumi wa Kiafrika mwanamume hafai kurejea nyumbani kabla ya mkewe. Hali ya ubabedume pia inachangia kunyanyasika kwake kwani mkewe ana madaraka kumzidi. Mwanamume ndiye anafaa kurejea nyumbani kama amechelewa kwa kuwa ukwezi wao wa kijinsia unamrumhusu ila katika muktadha huu hali inayodhihirika ni kinyume chake.

Katika hadithi ya ‘Masharti ya Kisasa’ katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, tunamwona Dadi akinyanyasika kwa kudhani kuwa mkewe ana mpango wa kando. Mwandishi anasema:

> Lazima niache kazi maana mume wangu haniamini… Anadhani kwamba mimi na kwenda na… ananifikiria nina “mpango wa kando’’ (TL, uk. 68*)*

Tunamwona Kidawa akiamua kujiuzulu kutoka kwa kazi ya umetroni kwa sababu mumewe Dadi alidhani kuwa ana mpango wa kando ingawa Kidawa hakuwa nao. Mumewe Dadi anakuwa na wasiwasi mwingi kuwa mke wake ana jicho la nje. Anaamua kumfuata ili kwenda kuchunguza. Anamfuata Kidawa mpaka kazini. Aliamua kupanda paipu iliyoko karibu na dirisha la mwalimu mkuu. Alijiambia lazima apande paipu ili achungulie na kujionea vituko vinavyoendelea baina ya mkewe na mwalimu mkuu.

Mwandishi anaonyesha Dadi akinyanyasika kwa kupata majeraha anapomfuata mkewe kazini kuthibitisha iwapo ana mapenzi nje ya ndoa.

> Alikuwa kalala chini kwenye kokoto na kupoteza fahamu. Kidawa alipopiga tochi alimkuta mumewe Dadi damu imemwenea kichwani. Mwalimu mkuu hakusita hapo kamwe. Haraka alikwenda kupiga simu kuita ambulensi. (TL, uk. 68)

Maneno *alikuwa kalala chini kwenye kokoto na kupoteza fahamu* na *damu imemwenea kichwani*. yanaonyesha jinsi Dadi alinyanyasika kwa kumshuku mkewe kuwa na mpenzi wa kando. Dadi alishindwa kutulia kwa kuwa wanakijiji walimsimanga kuwa amedhibitiwa na mkewe. Haya yalimkera Dadi mpaka akaamua kumfuata mkewe. Baadaye anaumia sana na kupelekwa hospitali. Hakuna jambo linaloweza kumkera mwanamume zaidi kuliko kujua kuwa mkewe anafanya mapenzi nje ya ndoa. Jambo hili husababisha hata wenzi kuwatoa nyoyo wapenzi wao wanapogundua kuwa wanaendewa kinyume. Dadi anachora taswira ya kiwango cha athari ambayo mwanamume hupitia akigundua kuwa mkewe ana mpango wa kando. Kulingana na nadharia, Dadi ananyanyasika kwa sababu ya mtagusano wa vipengele vya uchumi, jamii, ubabedume na utamaduni. Mateso haya yanatokana na mkewe Kidawa kwenda kufanya kazi ya umetroni usiku. Ubabedume unamfanya kuwa na imani kuwa mwanamke hawezi kuwa na ukuruba na mwanamume kikazi tu bila kuwa na mahusiano ya kimapenzi. Kidawa anaonekana kwenda kinyume na matarajio ya kijamii kwa kufanya kazi usiku. Hili linasababisha jamii kumsimanga kama anayedhibitiwa na mkewe. Kidawa anachorwa kama anayekiuka tamaduni za jamii jambo linalomfanya Dadi kunyanyasika zaidi.

Mtafiti ana msimamo kuwa wanawake wanapopata nafasi ya kufanya kazi, wanafaa kuwa waaminifu kwa wapenzi wao. Si kutenda kama Chaurembo alivyofanya. Vilevile wanaume hawafai kuwashuku wake zao kuwa na mipango ya kando wanapoenda kazini kwani tunaona vile Dadi alinyanyasika kwa kumshuku mkewe. Aliishia hospitali na majeraha mabaya sana. Jinsia zote mbili zinapaswa kulaumiwa hapa kwani wanawake wanawaendea kinyume waume zao nao wanaume wanawashuku wake zao kuwa na mapenzi nje ya ndoa. Wanandoa wanafaa kuelimishwa umuhimu wa kuwa waaminifu katika ndoa na madhara ya kuwashuku wengine na kutokuwa waaminifu katika ndoa. Haya yanaingililiana na maoni ya Allen na wenzake (2025) waliogundua kuwa wanandoa wanapoaminiana na kushirikiana hufaidika kwa ndoa zao kunawiri na kudumu.

### 4.3.2. Kutenganishwa na familia

Kulingana na Mbiti (1989), binadamu katika jamii za Kiafrika hawezi kuishi peke yake. Katika jamii hizi mtoto alishirikishwa katika jamii yake kikamilifu, akafundishwa umuhimu wa ushirikiano kwa sababu ni kupitia kwa watu wengine ndipo mtu huweza kuhisi nafsi yake, madaraka yake na majukumu yake mwenyewe na majukumu yake kwa mwingine. Wanaume hukabiliwa na unyanyasikaji wa kutenganishwa na familia walimokulia na watu wanaohusiana nao kidamu.

Katika hadithi ya 'Ndoto ya Mashaka' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, mhusika Mashaka ananyanyasika anapotenganishwa na familia yake. Anasema kuwa siku moja alishangaa ya kushangaa aliporudi nyumbani kutoka kazini akampata mkewe Waridi na watoto wake wametoroka. Anasema aliwasuburi ila hawakurudi. Akazidi kuwatafuta lakini juhudi zake zikagonga mwamba. Mwandishi anasema:

> Hali hii ya utengano ilizidi kunipa unyonge na kuninyong'onyeza. Ningeishije? Sikuona thamani ya maisha tena. Nikawaza ya laiti ningekuwa na maisha mazuri. Mke wangu angeniheshimu. Asingekuwa na wazo la kunikimbia na kuniachia ukiwa nilio nao leo (TL1, uk.77)

Sentensi *Hali hii ya utengano ilizidi kunipa unyonge na kuninyong'onyeza* na *sikuona thamani ya maisha tena* inaonyesha Mashaka akinyanyasika kwa sababu ya kuachwa na mkewe Waridi na wanawe. Mashaka alihuzunika. Kutengana na familia yake kulimfanya mnyonge. Hakuona haja ya kuishi tena bila familia. Alikuwa maskini, hivyo hakuweza kuwatimizia mahitaji yao, wakamtoroka. Anawaza mengi na kusema kuwa angekuwa na fedha angeweza kumfurahisha mkewe na watoto wake na hawangemtoroka. Ananyanyasika kwa ukiwa alioachiwa.

Kulingana na nadharia, vipengele vya uchumi, tabaka, ubabedume, na matarajio ya kijamii vimetagusana kumnyanyasa Mashaka. Ananyanyasika kwa kukosa hela za kuikidhi aila yake na baadaye inamtoroka. Vilevile ananyanyasika kwa sababu jamii haingemheshimu kwa kuwa alitorokwa na mke. Isitoshe, ubabedume unamsababisha Mashaka kujiona kuwa yeye si mume kamili kwa kukosa mke hivyo kunyanyasika zaidi. Pia ananyanyasika kwa kuwa anajiona kushindwa kutekeleza majukumu yake kama mume kamili.

Katika hadithi ya 'Tulipokutana Tena' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, Bogoa anaonekana kunyanyasika kwa kutenganishwa na familia yake.

> Hapo hapo nilianza kutokwa na machozi, maana sikutaka kutenganishwa na mama, baba, ndugu kaka na dada zangu. Nililia sana na kutoa kwenzi. Nikaendelea kulia na kupiga kelele lakini baba alinishikia mkwaju kutishia kunichapa. (TL2, uk.114)

Sentensi *Hapo hapo nilianza kutokwa na machozi, maana sikutaka kutenganishwa na mama, baba, ndugu kaka na dada zangu* inaonyesha Bogoa akinyanyasika kwa kutenganishwa na familia yake. Hali ya umaskini na kuwa na watoto wengi ambao hawangeweza kuwalea vizuri ilichangia Bogoa kutenganishwa na familia yake. Bogoa alilia na kukataa kwenda kwa kuwa hakutaka kutenganishwa na wao. Alipokataa kwenda, babake alitishia kumchapa. Bogoa akaenda shingo upande. Wao kuwa wengi hayakuwa makosa yake. Wazazi wake wangepanga uzazi ili wajue idadi ya watoto ambao wangepata na wale wangeweza kuwalea na kuwatunza. Huu ni ukatili waliomtendea Bogoa wa kumnyima haki ya kuishi na familia yake. Bogoa alifanyiwa hili kwa kuwa alikuwa mtoto wa kiume. Alikuwa na dada ambao wangeenda badala yake. Hili linaonyesha kuwa mtoto wa kiume huanza kunyanyasika akiwa mchanga. Haki za mtoto wa kiume zinapuuzwa huku mtoto wa kike akizidi kutukuzwa. Jambo hili linafaa kumulikwa zaidi katika jamii.

Audre (1984) alizungumza kwa kina kuhusu maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii. Kulingana naye, kipengele cha uchumi na jinsia vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Bogoa. Bogoa anatenganishwa na familia yake kwa kuwa wazazi wake ni wa tabaka la chini. Waliamua kupunguza mzigo wa ulezi kwa kumpeana Bogoa kwa Bi Sinai alikoteswa. Wazazi wake walimchagua Bogoa kwa kuwa alikuwa wa jinsia ya kiume. Pia kuna suala la jamii kuamini kuwa mtoto wa kiume anaweza kuteseka bila kulalamika. Hili linapelekea wazazi na jamii kumkinga mtoto wa kike huku wakimtelekeza mtoto wa kiume alivyofanywa Bogoa. Kule kwa Bi Sinai alinyanyasika kwa kupitia mateso mengi kama vile kuchomwa, kupigwa na kunyimwa chakula.

Katika hadithi ya ‘Tafrija Kambini’ katika *Diwani ya Maskini Milionea* tunamwona babake Nangima akitenganishwa na familia yake. Mamake Nangima anamwambia:

> Usilete ngebe zako hapa. Babako na nduguyo hujui waliko. Hujui kakako kalalia maji au mate. Wewe unawazia karatasi tu. Mtoto una kichaa wewe? (MM, uk. 40)

Ni wazi babake Nangima alikuwa ametenganishwa na familia yake. Hii ni baada ya wao kukimbilia usalama wao majumba yao yalipochomwa na watu wasiojulikana.

Kulingana na nadharia, babake Nangima ananyanyasika kwa sababu ya muingiliano wa kipengele cha mifumo ya kijamii tabaka na ubaguzi. Watu wasiojulikana wanachoma makao hivyo kusababisha kila mtu kutorokea usalama wake, hivyo anatengana na familia yake. Waliowachomea nyumba walitoa cheche za maneno ya kutisha wakisema wakata wakatwe, fukuza wasikwao, chinja! Kumaanisha walio katika tabaka la chini wauawe. Kila mtu alikimbilia usalama wake na hili likasababisha babake kutengana na familia yake. Walipoungana tena, alisimulia familia yake yale yaliyowafika kumaanisha kuwa alipatana na mengi. Hapa kipengele cha mifumo ya kijamii na tabaka vilishirikiana katika kunyanyasika kwa babake Nangima. Nangima anaashiria vile wanaume huteseka na kuuawa wakati wa vita. Wapiganaji huwauwa wanaume ila wanawake na watoto husazwa. Kulingana na City News (2025), Gachagua alilinganisha matukio ya sasa ya serikali na ukandamizaji wa enzi za ukoloni. Katika taarifa aliyoitoa, alilaani madai ya serikali kuwalenga vijana wa kiume wakati wa maandamano ya kizazi cha Gen-Z, na akarejelea historia ya Wakenya kupinga utawala wa kikoloni. Kauli yake inadhihirisha kuwa wanaume hulengwa wakati wa vita jambo ambalo huchangia kunyanyasika kwao.

Mtafiti anapendekeza kuwa aliye na uwezo katika familia anafaa kulisha familia kwa kuwa yeye ndiye Mungu amefungulia milango ya fanaka. Jamii inafaa kulaumiwa kwa kutenga majukumu kwa misingi ya kijinsia kwani aliye na uwezo katika familia anaweza kusimamia mahitaji ya nyumbani awe mwanamke au mwanamume. Haya yanalingana na maoni ya Palomino-Suárez na Aparicio (2025) waliosema kuwa jamii haifai kuwa na majukumu bainifu ya kijinsia kwani huleta utosawa. Utafiti unapendekeza kuwa jamii inafaa kuelimishwa kuwa yeyote yule aliyebarikiwa na ajira katika familia anafaa kukimu mahitaji ya familia.

### 4.3.3. Kukataliwa Uchumba

Mapenzi huwa kati ya wawili wapendanao. Ni suala la kiasilia mtu wa kike na wa kiume kupendana. Hata hivyo, tofauti za kitabaka husababisha wanaume kukataliwa uchumba na wazazi wa msichana. Huu ni udunishaji wa hali ya juu kwani hakuna anayependa kuwa maskini. Pia kuwa maskini katika kipindi fulani si kumaanisha kuwa mtu ataishi katika hali hiyo.

Katika hadithi ya 'Mapenzi ya kifaurongo' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Penina akimwambia Dennis maneno haya:

> Nilikupenda nikidhani utapata kazi, kumbe wewe ni kiumbe asiye na maana yoyote. Nimemkosea mama na babangu mno. Walikuwa wamenionya dhidi ya kuchumbiwa nawe. Nikawapuuza. Sasa nimekuja kujua walichomaanisha. Maneno yao yamenisibu. (TL 1, uk. 26)

Wazazi wake Penina walikuwa wamekataa uchumba wake na Dennis kwa kuwa Dennis alikuwa maskini. Penina anasema aliwapuuza lakini amekuja kujua walichokimaanisha. Hivyo anamfukuza Dennis. Uchumba wao unasambaratika kwa sababu ya tofauti zao za kiuchumi. Penina anayetoka tabaka la juu hataki kuolewa na mwanamume asiye na kazi na mshahara mkubwa au aliyetoka katika tabaka la chini. Hivyo anauvunja uchumba wao.

Mwandishi wa hadithi anaonyesha Dennis akinyanyasika anapoambiwa maneno haya. Msimulizi anasema:

> Ninanyanyuka kutoka kochini kama mwenye kichaa. Nina hasira si hasira. Nimekerwa mpaka mwisho wa kukerwa. Ninafululiza moja kwa moja mpaka chumbani. Ninachukua nguo zangu na kuzitia katika mkoba. Ninatoka nje na kuuburura mkoba wangu wenye vigurudumu (TL 2, uk. 27)

Dondoo hili linaonyesha kuwa Dennis ananyanyasika. Anasema kuwa anapatwa na hasira si hasira na kukereka. Kinachosababisha Dennis kukataliwa uchumba na wazazi wa Penina ni kuwa yeye ni maskini. Patricia (1990) anaonyesha vile kipengele cha uchumi, tabaka na matarajio ya kijamii vinashirikiana katika kunyanyasika kwa Dennis. Dennis hakuwa na ajira hivyo alikuwa wa tabaka la chini. Wazazi wa Penina

walitoka tabaka la juu hivyo wakaikataa posa ya Dennis kwa kuwa alikuwa maskini. Jamii huchukulia kuwa mume ana jukumu la kuilisha familia yake. Wazazi wa Penina waliona kuwa Dennis ni maskini kwa hivyo hangeweza kumtimizia mkewe mahitaji yake hivyo wazazi wake wakamwonya dhidi ya ndoa hiyo. Utamaduni na jamii hutarajia mtoto wa kiume kuoa mke, kulipa mahari na kuilisha familia yake. Kutokana na uchochole wa Dennis, angeshindwa kuyatimiza haya na ndiyo maana anakataliwa na Penina. Hali hizi zote zinatagusana kumdhulumu mtoto wa kiume. Dennis ananyanyasika kwa kupatwa na hasira na kujuta kwa nini mwanzoni aliyakubali mapenzi ya Penina.

Katika hadithi ya 'Ndoto ya Mashaka' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba* tunamwona pia mhusika Mashaka akiaibikiwa na wazazi wa Waridi kwa kuwa yeye Mashaka alikuwa maskini:

> Ndoa yetu na Waridi ilitia toa na doa andikizi katika familia nzima ya Mzee Rubeya. Walikosa raha kweli. Mamwinyi wenye faka zao! Viweje tena hohehahe kama Mashaka? Huba zetu zikawa kichefuchefu kikubwa kwa mzee Rubeya na mkewe waridi. Aibu ilipowazidi, wakakimbilia Yemeni. (TL 3, uk.74)

Dondoo linaonyesha kuwa Mashaka ananyanyasika kwa sababu ya ndoa yake. Wazazi wa Waridi wanaaibikia ndoa yao kwa sababu ya umaskini na kuhamia Yemeni kwani mapenzi yake na Waridi yalikuwa kichefuchefu kikubwa kwa Mzee Rubeya na mkewe mama Waridi. Iliwabidi kukimbilia Yemeni kwa sababu ya kuaibikia umaskini wa Mashaka. Baadaye Mashaka anatorokwa na mke wake pamoja na watoto wao. Anawatafuta kwa siku nyingi bila mafanikio na hili linampa mawazo tele. Kipengele cha tabaka na matarajio ya kijamii vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Mashaka kwa mujibu wa Patricia (1990). Mashaka alikuwa maskini hivyo mkewe na wanawe wakamtoroka. Wazazi wa Mkewe walikuwa matajiri. Iliwalazimu wahamie Yemeni kwa kuaibikia umaskini wa Mashaka. Ni matarajio ya jamii kuwa mwanamume anafaa kuikimu familia yake. Wazazi wa Mashaka waliona kuwa mwanao aliolewa na mtu wa tabaka la chini kwa hivyo wakaikataa ndoa hiyo. Hapa kipengele cha tabaka na matarajio ya kijamii vinaungana katika unyanyasikaji wa Mashaka.

Mchango wa mtafiti ni kuwa, wazazi hawafai kuingilia ndoa za wanao na kuzikataa kwa misingi kuwa wanaolewa na wapenzi wa tabaka la chini. Hakuna anayechagua kuwa maskini. Wazazi wanafaa kuelewa kuwa wapenzi wote ni sawa wawe wa tabaka la chini au la juu. Pia wajue kuwa walio katika tabaka la chini waweza kuinuka siku zao za usoni. Katika ndoa hizi mbili, wazazi wote walikuwa na uwezo wa kiuchumi lakini wakaamua kutosaidia. Wa kulaumiwa hapa ni wazazi ambao hukataa wachumba wa wanao kwa misingi ya mali. Wazazi wanafaa kuelimishwa kuhusu madhara ya kuingilia ndoa za wanao na kutotumia kigezo cha fedha wanapowachagulia wanao wachumba.

### 4.3.4. Kutukanwa

Bandura (1990) alijadili jinsi matusi yanavyoathiri tabia ya watu, hasa watoto. Aliona kuwa matumizi ya matusi yanaweza kukuza tabia mbaya na kutengeneza mazingira ya fujo na vurugu kwa kuwa hakuna mtu hufurahi wakati anaelekezewa lugha ya matusi. Alisema kuwa lugha huathiri hali katika jamii.

Lenard (2025) anasema kuwa upyaro huwa na hasara zake. Upyaro huvuruga uhusiano mwema baina ya watu. Husababisha kuongezeka kwa chuki na hofu. Chuki husababisha watu kukosa furaha kuvuruga uhusiano wao na watu wanaowatukana.

Katika hadithi ya ‘Tulipokutana Tena’, katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, inadhihirika kuwa Bogoa ananyanyasika anapotukanwa na Bi Sinai. Mwandishi anasema:

> Hii ilikuwa furaha yangu, pumziko langu, utulivu wangu kutokana na misukosuko, matusi na masimbulio ya Bi Sinai. (TL, uk. 116)

Kauli hii inaonyesha kuwa Bogoa alikuwa akinyanyasika kwa matusi aliyopokea kutoka kwa Bi Sinai aliyefaa kuwa mlezi wake. Alikuwa amepelekwa kwake na wazazi wake aishi huko kwa kuwa wazazi wake walikuwa na watoto wengi hivyo hawangeweza kuwalea vizuri. Wakaamua kumpeleka Bogoa kwa Bi Sinai. Bogoa alikuwa anawasimulia marafiki zake mateso aliyopitia kwa mama huyo kiasi cha kusema kuwa “Pale palikuwa jehanamu kwake. Mara moja nikafahamu kwamba nilikuwa mtumwa nyumbani hiyo”. Alinyanyasika kwa njia nyingi akiwa pale kama vile kuchomwa viganja, kunyimwa chakula, kupigwa na kufanyishwa kazi za nyumba.

Kwa mujibu wa Audre (1984), kipengele cha kichumi, jinsia na utabaka vinashirikiana na kusababisha unyanyasikaji wa Bogoa. Bogoa ananyanyasika kwa kutukanwa na Bi Sinai. Kichocheo cha haya yote ni hali wa kiuchumi. Wazazi wake walitoka tabaka la chini. Hawangeweza kuwalea watoto wao wote vyema kwa sababu ya umaskini. Hivyo, wakaamua kumpeleka Bogoa kwa Bi Sinai kwa kuwa alikuwa wa jinsia ya kiume. Kule alikoenda kulikuwa kama jehanamu. Alinyanyasika kwa kuteswa na kutukanwa na Bi Sinai.

Katika hadithi ya 'Nizikeni Papa hapa' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Otii akinyanyasika kwa kutukanwa na mwenyeketi wa chama cha watu wa nyumbani.

> Anzeni mapema kuchangisha fedha ya kusafirisha maiti, alisema mwenyekiti wa Chama Cha Watu wa Nyumbani. Tunahitaji kuchangisha fedha za kununua jeneza, mavazi ya kumvisha maiti pamoja na fedha za kukodisha magari ya kuchukua maiti na waombolezaji kutoka hapa Kisumu Ndogo, Mombasa, hadi Sidindi karibu na Kisumu Kubwa, Kisumu asilia. (TL, uk. 97)

Kumwita mtu *maiti* ni kumtukana. Mkurugenzi wa Chama cha Watu wa Nyumbani anamtukana Otii na kumwita maiti. Ni kinaya kumtembelea mtu hospitalini kumjulia hali kisha kumwita maiti hata kabla hajaaga dunia. Wanapanga mazishi yake pia huku akiwasikia. Otii anapokuwa pale hospitalini, baadhi ya watu wanamtembelea. Jamaa na marafiki walikuwa wameambiwa wamrejeshe nyumbani kwani hakukuwa na matumaini ya kupata afueni. Mwandishi anaonyesha kuwa Otii anazidi kutukanwa.

> Baadhi ya watu waliozika imani na huruma zao, watu wenye kejeli zilizopindukia, wanamwita mbu. (TL, Uk. 96)

Otii anatukanwa na kuitwa mbu. Mbu huleta dhana ya unyonyaji. Mbu ni aina ya mdudu lakini watu wanamwita Otii mbu. Hili linamfanya kunyanyasika zaidi kwani wanamwita mbu akiwa anasikia. Si ubinadamu kumwita mtu mbu hasa akiwa mgonjwa. Kinaya zaidi ni kupanga mazishi ya mtu ambaye yu hai. Watu huenda hospitalini kuwapa wagonjwa matumaini lakini hawa walienda kupanga mazishi ya Otii akiwa hai. Ukweli ni kuwa Otii alinyanyasika na kuathirika kihisia. Alisalitiwa na watu wa jamaa yake pamoja na marafiki. Vilevile Otii alinyanyasika alipopata habari kuwa Wanjiru aliyekuwa mpenziwe ameaga dunia. Wanjiru mpenziwe ndiye

aliyemwambukiza maradhi. Otii ananyanyasika kama mtoto wa kiume. Mwanzoni alikuwa maarufu na mwenye pesa. Siku moja akiwa katika starehe zake anakutana na msichana mrembo aitwaye Wanjiru. Wanakuwa wapenzi. Wanjiru alijua kuwa alikuwa na ugonjwa wa ukimwi lakini hakumwambia Otii. Baada ya muda, Otii hakumwona Wanjiru tena. Alipoulizia habari zake, alielezwa kuwa Wanjiru aliaga kwa ugonjwa uliokuwa na dalili kama zile za ugonjwa wa Otii. Otii alinyanyasika zaidi kwa kujua kuwa pia naye angeaga dunia.

Utamaduni na matarajio ya kijamii zinasababisha kunyanyasika kwa Otii kwa mujibu wa nadharia. Utamaduni unamnyanyasa kwa kumtaka azikwe kwao kinyume cha mapenzi yake. Vilevile matarajio ya kijamii yanapelekea yeye kufanyiwa harambee ya mazishi na watu wa ukoo wake hata kabla hajafa. Huenda kilichomwua si maradhi bali ni shinikizo kutoka kwa jamaa zake.

Mtafiti anaeleza msimamo kwamba ni wajibu wa wazazi kupanga uzazi ili kuhakikisha kuwa idadi ya watoto wanaopata inalingana na uwezo wao wa kuwalea kwa hali bora. Kwa mantiki hii, anadokeza kwamba iwapo wazazi wa Bogoa wangekuwa na mpango madhubuti wa uzazi, huenda Bogoa asingekumbana na unyanyasikaji alioupitia mikononi mwa Bi Sinai. Aidha, mtafiti anasisitiza umuhimu wa jamii kuzingatia athari za maneno wanayowatamkia wengine, kwani matumizi ya lugha kali na ya kuudhi kama ilivyomkumba Otii hospitalini huweza kusababisha madhara ya kihisia. Kutokana na hayo, wazazi wa Bogoa wanawajibika kwa mateso aliyoyapata mtoto wao, sawa na jamii inayotumia lugha ya matusi. Suluhisho linaweza kupatikana kupitia elimu kwa wazazi kuhusu upangaji uzazi, na kampeni za kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwasiliana kwa heshima, kwa kuzingatia kuwa maneno yana uwezo wa kujenga au kubomoa utu wa mtu.

### 4.3.5. Kunyimwa Chakula

Katika hadithi ya ‘Mapenzi ya Kifaurongo, katika *Diwani* ya *Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Dennis akinyanyasika kwa kunyimwa chakula na mpenzi wake Penina:

> Penina: “Umepata kazi?” Anauliza bila shauku.
>
> Dennis: “La,” ninamjibu huku nikijipweteka kochini “Kuna chochote cha kutia tumboni?” Nauliza kwa sauti ya kunyong’onyea na kukata tamaa. Nimeuliza kama kuna chochote cha kutumbukiza tumboni?”

> Penina: "Mmmh!" Anaguna. Utakula chakula cha nani? Hujachangia chochote. Wacha ubwege. Mtu huvuna alichopanda. Hukuacha hata senti moja nyumbani hapa. Sikupika upepo. Hamna chakula wala uji. Penina anajibu kwa sauti ya ukali (TL, uk. 26).

Maneno haya yanaonyesha kuwa Dennis aliomba chakula kwa kuwa alikuwa na njaa lakini hakupewa. Dennis alikuwa amerudi nyumbani baada ya shughuli ya kusaka kazi. Hakika alikuwa amehisi njaa na pia alikuwa amechoka. Anapomwuliza Penina kama kuna chochote ambacho angeweza kula, Penina anamnyima chakula. Anamwambia kuwa hakuacha chochote cha kupika. Kilichosababisha yeye kutompa chakula ni kuwa hakufaulu kupata kazi. Hili linamfanya Dennis kusema kuwa amegundua kwamba kweli Penina amemdharau na kumuona kama kinyaa au matapishi.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho, unyanyasikaji wa Dennis unatokana na ushirikiano wa kipengele cha kiuchumi na tabaka, ubabedume, utamaduni na matarajio ya jamii. Jamii haitarajii mke kumlisha mume. Dennis alikuwa analishwa na mpenziwe Penina. Utamaduni humbeza mume asiye na uwezo wa kukidhi mahitaji ya mkewe na familia. Dennis hakuweza kukidhi mahitaji haya. Hata kodi ya nyumba alilipiwa na wazazi wa Penina na ubabedume hauruhusu mume kuishi kwa nyumba inayolipwa na mkewe. Haya yote yalimfanya Dennis kunyanyasika zaidi. Kushindwa kutekeleza majukumu haya kunamfanya Dennis kurushiwa maneno makali kama vile awache ubwege kwani hakuacha chochote cha kupikwa na mkewe hangepika upepo. Dennis ametoka katika tabaka la chini jambo linalosababisha mkewe kumdharau.

Katika hadithi ya 'Tulipokutana Tena' katika *Diwani ya Tumbo lisiloshiba,* tunamwona Mashaka akinyanyasika kwa kunyimwa chakula na Bi Sinai.

Mwandishi anasema:

> Hakujua maskini kwamba mimi nilikuwa nikila makoko ya vyakula au makombo ya watu waliyoacha baada ya chakula. Tena nikila wa mwisho wakati kila mtu ameshakula. Nilikula kwenye sufuria na vyungu wakati kila mtu alikula sahanini. (TL 2, uk. 17)

Bogoa alikuwa akinyimwa chakula. Chakula chake kilikuwa ni makoko au makombo ya watu waliyoacha baada ya kushiba. Huu ni ukatili kwa Bogoa kwa kuwa kazi za

nyumbani ni yeye aliyezifanya lakini chakula hakuruhusiwa kula. Huu ni ukiukaji wa haki za kibinadamu. Si haki kumnyima mtu chakula. Hii ni njia mojawapo ya kumdhalilisha mwanamume.

Unyanyasikaji wa Bogoa unatokana na ushirikiano wa kipengele cha uchumi, jinsia na tabaka lake kwa mujibu wa nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho. Bogoa ametoka tabaka la chini. Ananyanyasika kwa sababu ya umaskini wa wazazi wake ambao hawana ajira. Wazazi wake wanamchagua kwenda kuishi kwa Bi Sinai. Bogoa anateseka kwa kuwa mtoto wa kiume. Ananyimwa chakula licha ya kufanya kazi nyingi. Anakula mabaki ya chakula kilichobakishwa na wale walioshiba.

Mtafiti ana mtazamo kuwa wapenzi wote katika ndoa ni sawa, wanafaa kushirikiana na kusaidiana katika ndoa. Aliye na uwezo wa kifedha anafaa kugharamia mahitaji ya nyumba kama Hill na wenzake (2022). Penina alikuwa na uwezo wa kifedha lakini hakumsaidia Dennis. Mtafiti anasisitiza kwamba mienendo ya wahusika kama Penina inaakisi ukosefu wa uelewa kuhusu majukumu ya kifamilia na kijamii. Licha ya juhudi za mpenzi wake Dennis kutafuta ajira, Penina akamkosea heshima jambo linalosababisha kunyanyasika kwake. Vilevile, kitendo cha Bogoa kunyimwa chakula ni dhihirisho la ukatili anaotendewa. Wanaolengwa kwa lawama ni Penina, wazazi wa Bogoa, na Bi Sinai kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao kikamilifu. Kwa mujibu wa mtafiti, suluhisho linaweza kupatikana iwapo jamii itaelimishwa na kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa kushirikiana kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya nyumbani.

### 4.3.6. Kuchapwa

Wanaume hukabiliwa na unyanyasaji wa kupigwa. Unyanyasaji huu umekuwa na ugumu wa kukubalika na watu wengi kwa sababu kulingana na desturi za jamii nyingi, mwanamume alikuwa ameruhusiwa kumpiga mkewe ikiwa amekosa utiifu au ikiwa hafanyi majukumu yake ya kinyumba kama alivyotarajiwa Kimani (2003). Pia itikadi na mila zilimruhusu mwanamume kumpiga mkewe baada ya kipindi fulani ili asipotoke na kutenda yasiyotakikana. Kwa mujibu wa hadithi zilizoteuliwa, inadhihirika wazi kuwa wanaume hunyanyasika kwa kupigwa.

Katika ya hadithi ya ‘Tulipokutana Tena’ katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Bogoa akinyanyasika kwa kuchapwa. Mwandishi anasema:

> Alilia sana kwani hakutaka kwenda na kupiga kelele lakini babake alimshikia mkwaju kutishia kumchapa ikambidi afumbe midomo yake ikalazimu amfuate. (TL, uk.115)

Bogoa anaeleza jinsi alivyokataa kwenda kwa Bi sinai. Alilia sana na kukataa lakini babake akatishia kumchapa. Wazazi wake walikuwa maskini na walikuwa na watoto wengi. Wazazi hawa hawakuweza kuwalea hivyo wakampeleka kwa Bi Sinai rafiki yao kuishi huko.

Mwandishi anaendelea kuonyesha kuwa Bogoa alinyanyasika zaidi kwa kuchapwa anaposema:

> Alipochelewa kurudi, alimtafuta na alipompata alimpiga vibaya sana. (TL, uk. 116)

Kifungu *alimpiga vibaya sana* kinaonyesha kuwa Bogoa alinyanyasika zaidi kwa kupigwa na Bi Sinai. Anasema kuwa alipoenda palikuwa kama jehanamu kumaanisha kuwa alikuwa akipitia mateso mengi. Anaeleza kuwa kila wakati Bi Sinai akitoka kazini alikuwa akimpiga bila kufanya kosa lolote. Maoni ya mtafiti ni kuwa mwanamume au mtu mzima afanyapo kosa hafai kupigwa. Wanafaa kutumia njia mwafaka za kusuluhisha migogoro kama vile kutafuta ushauri kwa wataalamu.

Patricia (1990), alianzisha dhana ya matriki ya utawala ambayo inaeleza jinsi vipengele vya utambulisho kama jinsia, rangi, na tabaka vinavyoathiriana na kuunda mifumo ya ukandamizaji. Kipengele cha uchumi, jinsia na mamlaka vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Bogoa. Wazazi wa Bogoa ni maskini, jambo hili linasababisha wao kumpeleka kwa Bi Sinai ambaye ni tajiri ili amlee. Bogoa ana dada zake lakini yeye ndiye anatengwa kwa kuwa yeye ni wa jinsia ya kiume. Pale anapoenda ananyanyasika kwa kupigwa, kuchomwa na kutendewa unyama mwingi. Babake Bogoa pia alitumia mamlaka yake kama mzazi hivyo kuchangia unyanyasikaji. Anamchagua Bogoa kati ya watoto wake wote kumi na wawili na kutishia kumchapa alipokataa kwenda. Mwandishi anatuchorea hali ilivyo katika jamii. Bogoa ananyanyasika kwa sababu ya makosa yasiyo yake. Wazazi wanafaa kujukumika na kutekeleza majukumu yao. Vilevile jamii inafaa kuhamasishwa jinsi ya kupanga uzazi. Endapo wazazi wa Bogoa wangetekeleza mpango madhubuti wa uzazi kwa kuzingatia uwezo wao wa kimalezi na kiuchumi, huenda Bogoa asingekumbana unyanyasikaji uliomkumba.

Msimamo wa mwandishi ni kuwa watoto wote ni sawa wawe wa jinsia ya kiume au ya kike. Pia walio na majukumu ya kuwalea watoto wawe watoto wao kibiolojia au wa kupanga wanafaa kuwajika katika malezi. Walezi wanaowalea watoto kwa udhalimu wanafaa kulaumiwa pamoja na wazazi wanaokosa kuwajibika katika malezi ya wanao. Idadi ya watoto, iwe ndogo au kubwa, haipaswi kuwa msingi wa ubaguzi. Suluhisho linaweza kupatikana iwapo jamii itaelimishwa na kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa kuwatambua na kuwatendea watoto wote kwa usawa, bila kujali hali zao za kifamilia. Mtazamo huu wa usawa ni nguzo muhimu katika kuimarisha ustawi wa watoto na kudumisha mshikamano wa kijamii.

### 4.3.7. Kufanyishwa Kazi za Nyumba

Osore (2008) katika tasnifu ya uzamifu alifanya utafiti kuhusu kinaya katika riwaya za Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa, kutoka utotoni mafunzo katika jamii yalijikita katika uana. Wanaume walichukuliwa kuwa kichwa cha familia. Walipewa majukumu ya kutimiza mahitaji ya wake na watoto wao. Ili kutimiza haya, walijihusisha na kilimo na uvuvi. Majukumu ya wanawake yalikuwa ya kufagia boma, kupika, kuosha vyombo na nguo na kufuma mikeka.

Katika jamii ya Kiafrika, inajulikana kuwa kazi nyepesi nyepesi za nyumbani kama vile kupika, kufua, kufagia, usafi wa nyumba na kutunza watoto ni jukumu la mwanamke. Mwanamume anayefanya kazi hizi huonekana kama aliyedhalilishwa au kunyanyaswa. Kitamaduni, mwanamke anafaa kushughulika na kazi za nyumbani kwani haya ndiyo matarajio ya jamii. Hapo awali, ubabedume ulimfanya mwanamume kuwa mchangiaji wa kipekee wa uchumi wa familia, lakini katika maisha ya kisasa, mwanamke pia anatoa mchango mkubwa katika uchumi wa familia na jamii. Kwa kuwa mwanamke anachangia kwa kuleta pato nyumbani, anahisi kuwa anafaa kusaidiwa kazi za nyumba.

Katika hadithi ya ‘Masharti ya Kisasa’ katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, mhusika Dadi alikuwa akifanya kazi za nyumba na hili halikumfurahisha kamwe. Alikuwa ametia saini masharti aliyokuwa amepewa na Kidawa kabla ya kumwoa kwa papara. Hakuchukua muda wake kuyaelewa kwani alikuwa amefurahi sana Kidawa alimpokubali. Masharti haya yalimsababisha kufanya

asiyopenda kwani alipoyavunja au kuyasahau alikumbushwa kila wakati. Mwandishi anasema:

Mfano 1:

> Hebu fikiri wewe. Tokea lini kidume cha kweli, akune seruni na kukalia mbuzi kukuna nazi? Akishaikuna nazi, ainuke kwenda kuchuja nazi hiyo kuitia mboga *tuwi* kunoga? Itakuwaje mwanamume wa kupigiwa mfano aoshe vyombo au afagie nyumba? Au afue na kupiga pasi? Kweli mkewe anafanya kazi za nje pia. Kazi moja ikiwa ile ya ulinzi wa wanafunzi wa kike wanaoishi bwenini, yaani kazi ya umetroni. Yaani Kidawa hupita vijumbani kuuza kanzu, viatu na khanga kutoka Uarabuni. Na eti Kidawa kazi hizo huzipamba kwa maneno. (TL1, uk. 61)

Katika dondoo hili, sentensi *Itakuwaje mwanamume wa kupigiwa mfano aoshe vyombo au afagie nyumba, au afue na kupiga pasi* inaonyesha kuwa Dadi alikuwa akifanya kazi za nyumba. Kazi hizi ni kama vile: kufagia, kukuna nazi, kuosha vyombo, kupiga nguo pasi na nyinginezo. Mwandishi amechora kazi hizi kama za mwanamke kwa kuwa anasema kuwa kazi za ndani ni za mwanamke na za nje ni za mwanamume. Mhusika Dadi anasema kuwa anazifanya kazi hizi si kwa sababu anapenda ila tu amfurahishe mkewe. Dadi anahisi kuteswa kwa kufanya kazi hizi si kwa sababu ni vibaya bali ni kinyume na utamaduni na matarajio ya kijamii.

Mwandishi anasema kuwa:

Mfano 2:

> Kidawa humwambia asaidie kazi za nyumba, na yeye Dadi hajaacha kusaidia, lakini hatosheki kamwe mwanamke huyo. Na si hatosheki tu, hataki kukubali kuwa mwanamume kazi zake ni za nje si za ndani. Na yeye akishiriki kazi za nyumba ni kwa hisani tu (TL 2 uk. 60).

Katika nukuu hili, maneno *kazi za nyumba, mwanamume kazi zake ni za nje si za ndani* na *kwa hisani tu* yanaashiria kuwa kuna kazi ambazo mhusika Dadi alikuwa analalamika kuzifanya kama mwanamume akidai kuwa ni za mwanamke. Mwandishi anaonyesha kuwa Kidawa humwambia mumewe Dadi amsaidie kazi za nyumba na Dadi hufanya hivyo ila mkewe huwa haridhiki. Dadi anasema kuwa mkewe hatosheki

anapomsaidia na pia hataki kukubali kuwa mwanamume kazi zake ni za nje wala si za ndani. Vilevile anasema kuwa ingawa anafanya kazi hii, ni kwa hisani tu. Hivyo, anamsaidia mkewe kazi za nyumba kwa kuwa ni vyema kusaidia au anasaidia kwa kupenda tu lakini si kwa sababu zile ni kazi zake. Ubabedume unamsababisha kuhisi kuwa kuna kazi hafai kufanya kwa kuwa yeye ni mwanamume.

Katika dondoo hili inabainika wazi kuwa Dadi alifanya kazi za nyumba. Alipika, aliosha vyombo, alifagia, alifua na hata kupiga pasi. Haya anayafanya kwa kuwa mkewe Kidawa anafanya kazi za nje ambazo kulingana na mhusika Dadi zinafaa kufanywa na wanaume. Mwandishi pia anasema kuwa Dadi anafika nyumbani nyakati za saa kumi na mbili jioni hivi. Anavua nguo za kazini na kuingia msalani kukoga ili kujitoa vumba. Baada ya kukoga, anaingia chumbani na kuvaa seruni na fulana. Akiwa tayari kwenda kupata chajio.

Kipengele cha utambulisho wa uchumi, matarajio ya kijamii na jinsia vinashirikiana kumnyanyasa Dadi kwa mujibu wa Crenshaw (1989). Dadi alikuwa ametia saini masharti aliyokuwa amepewa na Kidawa kwa papara. Masharti haya yalimfanya Dadi kufanya kazi nyingi za nyumba. Dadi alianza kunyanyasika akisema kuwa kazi alizozifanya ni za mwanamke. Anasema kuwa kazi za mke ni za ndani ilhali za mume ni za ndani. Dadi alikereka kufanya kazi kama vile kuosha nyumba, kufagia, kukuna nazi na nyinginezo. Ni matarajio ya jamii kuwa majukumu ya kijinsia yanafaa kutekelezwa kwa misingi hiyo. Kuna kazi zilizotengewa wanaume na wanawake. Sababu za kiuchumi vilevile zinasababisha Dadi kutekeleza majukumu haya kwani mkewe anaenda kazini hivyo kumwachia Dadi kazi ya kulinda mtoto. Dadi anasema kuwa hizi kazi huzifanya lakini shingo upande kumaanisha kuwa alinyanyasika alipofanya kazi hizi. Ananyanyasika kwa sababu ya kuwa mwanamume.

Mtafiti ana msimamo kuwa ni vyema kusaidiana majukumu. Mwanamume pia anaweza kufanya hizi kazi iwapo anafanya kazi mbali na nyumbani kwake. Hata hivyo mwanamume akiwa nyumbani pamoja na mama na watoto, hafai kufanya kazi kama za kufagia na kuosha vyombo. Heshima ya mwanamume kama kiongozi wa familia inafaa kudumu.

### 4.4. Athari za Unyanyasikaji wa Wanaume

Sehemu hii imeangazia madhumuni ya pili ya utafiti ambayo ni kutathmini athari za unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi fupi teula za Kiswahili.

#### 4.4.1. Majuto

Kessy (2025) anasema kuwa majuto ni hisia za huzuni au uchungu zinazotokana na kutambua kuwa umefanya uamuzi au tendo ambalo linaonekana kuwa na madhara. Kila mtu anaweza kujuta kwa jambo alilofanya au alilokosa kufanya. Watu hujuta kwa sababu ya kufanya maamuzi yasiyofaa, kupoteza nafasi waliyokuwa nayo na kuwatendea wengine mabaya. Hata hivyo, kukwama kwenye majuto kunaweza kuathiri furaha yetu na kutuzuia kuishi kwa amani.

Katika hadithi ya 'Mapenzi ya Kifaurongo', katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, mhusika Dennis amesawiriwa akiwa katika hali ya kujuta. Mwandishi anasema: Dennis hakukubali mapenzi ya Penina mwanzoni Penina alipokuja kumshawishi awe mpenzi wake, alikataa kwa kuwa hali zao zilikuwa tofauti lakini baadaye Penina anapomfukuza nyumbani anajuta kwa kukubali mapenzi hayo. Msimulizi anasema:

> Najutia uchochole wangu. Kumbe ile falsafa yake inayochombeza kwa maneno makali ya mapenzi ni uongo mtupu. Muda unavyoenda ndivyo hali halisi ya falsafa hii inavyobainika. Nabaki nimesimama kama sanamu nikimtazama Penina kwa jicho la hasira iliyochanganyika na kite. Huyu ndiye Penina aliyeniambia kuwa mali na mapenzi ni vitu viwili vyenye asili tofauti? Ameghairi nia na kubadilika kama msimu. Ameambatanisha mali na mapenzi na kuvifanya kuwa kitu kimoja. (TL 1, uk. 27)

Katika fungu hili, maneno na sentensi *najutia*, *Nabaki nimesimama kama sanamu nikimtazama Penina kwa jicho la hasira iliyochanganyika na kite* yanaashiria Dennis alikuwa akijuta. *Kujutia* ni ile hali ya kusikitikia vitendo vya nyuma. Dennis anajuta kuyakubali mapenzi ya Penina. Aliyakubali baada ya kuyakataa kwa muda. Dennis hana ajira kwa hivyo uchochole wake umesababisha yeye kuachwa na mpenziwe Penina. Kwa kuzingatia muktadha wa kijamii na kiuchumi unaomkabili Dennis, awali alikataa kuingia katika uhusiano wa kimapenzi na Penina kutokana na tofauti zao za hali ya maisha; ambapo Dennis alikuwa akiishi katika mazingira ya umaskini huku Penina akiwa na uwezo mkubwa kifedha. Hata hivyo, kupitia ushawishi wa Penina ulioambatana na msukumo wa kihisia, Dennis hatimaye alikubali kuwa katika uhusiano huo licha ya mitazamo yake ya awali. Maneno *Nabaki nimesimama kama*

*sanamu nikimtazama Penina kwa jicho la hasira iliyochanganyika na kite* yanaonyesha kuwa Dennis anajutia kwa uchungu baada ya Penina kumfurusha kwa kisingizio kuwa yeye hawezi kutoa hela zozote za chakula na matumizi ya pale nyumbani. Dennis alipokosa kazi, alifukuzwa kwa sababu ya uchochole wake. Maneno ya Penina yanamwumiza Dennis. Penina anamwambia wazi kuwa hakuwa anampenda na aliolewa naye kwa kuwa alidhani kuwa angepata kazi. Anapotafuta kazi bila mafaniko, anafukuzwa nyumbani.

Kauli ya Penina inayomzuia Dennis kumwita mpenzi na kumkataza kumweleza mtu yeyote kuhusu uhusiano wao wa awali, inadhihirisha ukatili wa kihisia unaoathiri kwa kiasi kikubwa hadhi ya mtu. Aidha, kumtaka Dennis atafute mpenzi mwingine mwenye hali kama yake kunaleta taswira ya ubaguzi wa kijamii na kimapato. Tabia hii inaashiria, kuwa Penina alikuwa na nia ya kufaidika na mafanikio ya Dennis, na aliposhindwa kutimiza matarajio hayo, anakataa uhusiano huo bila kuzingatia hisia na hali ya Dennis. Matokeo yake, Dennis anabaki na majuto makubwa kutokana na dhuluma hiyo ya kihisia.

Kwa mujibu wa nadharia kipengele cha tabaka, uchumi na tofauti za hali ya maisha kati ya Dennis na Penina zilisababisha athari za kihisia kwa Dennis. Ingawa Dennis alikataa uhusiano huo awali kwa sababu ya umaskini wake, alishawishiwa na Penina kutokana na matarajio ya mafanikio ya baadaye. Hata hivyo, baada ya kuoana, hali ya Dennis ya kutokuwa na ajira ilisababisha Penina kumdharau na kumfukuza, jambo lililoibua majuto makubwa kwa Dennis na kunyanyasika kwingi.

Katika hadithi ya 'Masharti ya Kisasa' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* Dadi amesawiriwa na mwandishi akiwa na majuto. Aliyatia saini masharti aliyopewa na kidawa na kukubali kuyafuata yote bila kuyaelewa. Mwandishi anasema:

> Pamoja na hayo yote, Dadi hakufahamu uzito wa maneno yale ya Kidawa yaliyotonewa kama kito chenye thamani neno 'kisasa' hatua kwa hatua, kipembe baada ya kipembe. Kwa sababu hii hakufahamu maana wala uzito wa maneno yale, hakuweza kuyazingatia vyema. Alijaribu kuyapinduapindua, kuyapekua pekua na kuyabiruabirua ili apate asili iliyomfanya afungike na maneno yale ya masharti toka wakati ule yaliposhurutishwa na Kidawa. Ilikuwa kama vile katia saini

> ya kukubali kutiwa kitanzi bila kutambua vipengele vya sheria za utiaji huo wa kitanzi. (TL 2, uk. 59)

Katika dondoo hili, sentensi *Dadi hakufahamu uzito wa maneno yale ya Kidawa yaliyotonewa kama kito chenye thamani neno 'kisasa'* na. *Ilikuwa kama vile katia saini ya kukubali kutiwa kitanzi bila kutambua vipengele vya sheria za utiaji huo wa kitanzi* yanaashiria kuwa Dadi alikuwa akijuta kuyatia sahihi masharti aliyopewa na mkewe Kidawa. Dadi alikuwa amemwinda Kidawa kwa siku nyingi awe mpenzi wake lakini kidawa alikuwa akikataa. Mwishowe alimweleza Dadi kuwa iwapo anamhitaji awe mke wake, ni lazima atimize masharti yake. Baadaye mambo yalipoanza kwenda mrama, akaanza kujuta. Masharti haya yalimruhusu Kidawa kuongea na wanaume anaotaka, kuvalia fasheni, kufanya kazi na kusaidiana kazi za nyumbani. Hili lilisababisha Dadi kufanya kazi zote za nyumbani kama vile kufagia, kupika, kupiga nguo pasi, kuosha nyumba na kazi nyinginezo. Wanakijiji walianza kumkejeli Dadi na kumsema kuwa alikuwa amezungushiwa donga na mkewe na kuwa alikuwa anamdhibiti. Maneno haya ya wanakijiji yalimkera Dadi sana.

Mwandishi pia anasema kutia yale masharti sahihi *Ilikuwa kama vile katia saini ya kukubali kutiwa kitanzi bila kutambua vipengele vya sheria za utiaji huo wa kitanzi.* Masharti haya yalimnyima Dadi raha na kumfanya kujuta zaidi. Anajiona kama aliyejitia kitanzi. Alichekwa na watu. Akaanza kuona wivu kuwa mkewe ana mpango wa kando nje. Alijuta zaidi.

Audre (1984) alizungumza kwa kina kuhusu maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi na jinsi vinavyoathiri uzoefu wa ukandamizaji au ukosefu wa haki. Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho, Dadi anaathirika kwa sababu ya mwingiliano wa kipengele cha matarajio ya kijamii na kiuchumi. Dadi aliathirika kwa kujuta kwa nini aliyatia masharti ya mkewe Kidawa sahihi. Haya masharti yalimkubalia Kidawa kufanya kazi hivyo kuchangia katika kukuza uchumi. Mkewe alifanya kazi ya umetroni hivyo usiku hakuwa nyumbani. Dadi alianza kumshuku mkewe kuwa na mpango wa kando. Jamii pia ilianza kumsema Dadi kuwa amedhibitiwa na mke kwani alifanya kazi zote za nyumbani. Dadi alijuta kwa kutochukua muda kuyaelewa masharti ya mkewe. Aliona kama alijitia kitanzi mwenyewe. Kweli majuto ni mjukuu. Dadi alifurahi Kidawa alipokubali kuwa mkewe lakini baadaye anakumbana na matatizo mengi kwa sababu ya masharti ya Kidawa. Dadi anaathirika kwa kujuta.

Mtafiti ana maoni kuwa watu wanafaa kuchukua muda kutafakari athari ya jambo kama hawajalitenda. Tunamwona Dadi akiathirika kwa sababu ya kuyatia masharti ya Kidawa sahihi kama hajachukua muda kuyalewa.

Kessy (2025) anasema kukwama kwenye majuto kunaweza kuathiri furaha yetu na kutuzuia kuishi kwa amani. Kujuta kuna mwathiri mwanamume na kusababisha yeye kuishi maisha yasiyo na furaha. Vilevile humfanya mwanamume kuishi bila amani. Dennis anaishi bila furaha na amani anapofukuzwa na Penina kwa ajili ya kuwa maskini.

### 4.4.2. Kukata Tamaa

Seligman (1998) anasema kukata tamaa ni hali ya kupoteza matumaini kabisa kuhusu jambo fulani au kuamini kuwa hakuna tena uwezekano wa mafanikio au mabadiliko chanya. Anaendelea kusema kuwa ni hali ya kihisia ambayo inaweza kuathiri afya ya akili na tabia ya mtu. Wanaume wanaponyanyasika huwa wanaishia kukata tamaa. Dennis amesawiriwa akiwa ametamauka.

Katika hadithi ya ‘Mapenzi ya Kifaurongo’ katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* mwandishi anasema:

> Baada ya kusema machache na mhazili wa kike aliyeketi nyuma ya tarakilishi, anaingia ndani. Kidogo ninasikia kicheko kikubwa kikitokea katika ofisi ya ndani. Kicheko hicho nakijua vizuri. Ni kicheko cha Shakila. Mwanamke aliyeingia mwanzoni ni mamake, itakuwa muhali kupata kazi. Yamkini matumaini yameanza kudidimia. Sina matumaini. Hata hivyo, bora ningojee tamko la mwisho kutoka kwa wakurugenzi wa kampuni hii. (TL, uk. 23)

Katika dondoo hili, sentensi *Yamkini matumaini yameanza kudidimia* na *Sina matumaini.* zinaonyesha kuwa Dennis amekata tamaa. Mkewe alikuwa amemsukuma sana atafute ajira ndiyo aweze kumtimizia mahitaji yake yote kwani yeye hawezi kuishi na mwanamume asiye na kazi na mshahara mkubwa. Anaenda kutafuta kazi katika kampuni moja. Akiwa anasubiri, msichana waliyesoma naye aitwaye Shakila anakuja kutafuta kazi. Baadaye anang’amua hiyo kampuni ni ya kina Shakila na mwanamke aliyekuwa akicheka ndani ya ofisi ni mamake. Dennis anapoteza matumaini ya kupata ajira. Anasema hana matumaini kuwa atapata kazi lakini anasema asubiri tamko la mwisho la wakurugenzi wa kampuni. Wanapoitwa kupata

matokeo, nafasi inamwendea Shakila kisha wanamcheka. Dennis anarejea nyumbani akiwa ametamauka zaidi.

Mwandishi anasema:

Mfano 2:

> Penina: Umepata kazi? Anauliza bila shauku.
>
> Dennis: La, ninamjibu huku nikijipweteka kochini Kuna chochote cha kutia tumboni? Nauliza kwa kunyong'onyea na kukata tamaa.
>
> Penina: Mmmh! Anaguna. Utakula chakula cha nani? Hujachangia chochote. Wacha ubwege. Mtu huvuna alichopanda. Hukuacha hata senti moja nyumbani hapa. Sikupika upepo. Hamna chakula wala uji. Penina anajibu kwa sauti ya ukali Dennis: Ninabaki pale mlangoni kwa mshangao wa aibu. (TL 2, uk. 26)

Sentensi *Nauliza kwa kunyong'onyea na kukata tamaa* inaashiria kuwa Dennis alikuwa amekata tamaa. Alikuwa ametoka kutafuta ajira lakini hakufanikiwa. Akifika nyumbani alikuwa mnyonge na aliyekataa tamaa. Anamwuliza mkewe iwapo kuna chochote anaweza kula lakini badala ya kumjibu kwa upole, anamkemea kwa maneno makali huku akimtusi. Baadaye Penina anamfukuza nyumbani kwa kukosa ajira. Hili linamsababisha kutamauka zaidi.

Kwa mujibu wa Patricia (1990), vipengele vya uchumi na matarajio ya kijamii vinashirikiana katika kuathirika kwa Dennis. Dennis hakuwa na ajira. Siku moja anaenda kutafuta kazi katika kampuni ya utangazaji. Msichana waliyesoma naye pia anakuja kutafuta kazi. Wakati anasubiri matokeo, anamsikia yule msichana wakicheka sana mle ofisini. Baadaye anakuja kuelewa kuwa alikuwa mamake Shakila na hiyo kampuni ilikuwa yao. Dennis anaathirika na kupoteza matumaini ya kupata kazi. Vilevile katika dondoo la pili tunamwona Dennis akiathirika pia. Aliporejea kutoka kutafuta ajira, alikuwa amekataa tamaa. Anaingia nyumbani na kuomba chochote anaweza kula lakini badala ya kupewa chakula, anapokezwa maneno makali na mkewe. Ni wazi kuwa Dennis alikuwa amepoteza matumaini kwa sababu anasema kuwa aliomba chakula kwa sauti ya kunyong'onyea na kukataa tamaa. Hii inaonyesha kiwango ambacho Dennis alikuwa ameathirika. Kulingana na Seligman (1998), kukata tamaa kuna madhara kwa mwanamume. Hali ya utamaushi inaweza ikaathiri

afya yake ya kiakili na tabia yake. Anaweza kukosa tumaini katika maisha na kuanza kujidunisha.

Mtafiti ana msimamo kuwa watu hawafai kukata tamaa kwa sababu ya hali ngumu wanayopitia kwani mawimbi ni sehemu ya maisha. Wanafaa kuwa na imani kuwa mambo yatabadilika na kuwa mema baadaye. Hakuna hali ya kudumu. Jambo mbaya likitendeka haimaanishi kuwa mambo yataishi kuwa mabaya. Kukata tamaa kunaweza kusababisha mtu kutenda maovu, jambo ambalo halifai. Jamii inafaa kuelimishwa umuhimu wa kutokata tamaa maishani na madhara yake.

### 4.4.3. Ukosefu wa Amani

Olkayade (2014) anaeleza kuwa katika jamii ya kisasa, amani inafafanuliwa kama hali ya kutokuwepo kwa vita, vurugu na usumbufu mwingine, na uwepo wa sheria na utulivu ndani ya jamii. Anasema amani inahusisha usalama, uhuru na ulinzi dhidi ya hatari. Amani na usalama ni pande mbili za sarafu moja. Amani inaweza kupatikana tu pale ambapo pana usalama, na usalama unahakikisha kuwepo kwa amani.

Katika hadithi ya 'Haramu tamu' katika *Diwani ya Maskini Milionea na Hadithi Nyingine*, tunamwona mhusika Karisa akichorwa akiathirika kwa kukosa amani. Mwandishi anasema:

Mfano 1:

> Moyo ulimpapa Chaurembo alipojipenyeza nyumbani mwake jioni hiyo. Kulikuwa na kimya kikuu. Isipokuwa taa za nje, ndani mlikuwa giza. Chaurembo akaamini Karisa mumewe alikuwa usingizini. "Umechelewa, mpenzi. Itakubidi upunguze kazi. Huu mji siku hizi usiku una wenyewe." "Oh mpenzi, samahani. Hii mikutano inaweza kuendelea hadi usiku wa manane", alijibu akiangalia upande. (MM 1, uk 86.)

Sentensi, *Umechelewa, mpenzi. Itakubidi upunguze kazi. Huu mji siku hizi usiku una wenyewe* na *Kulikuwa na kimya kikuu. Isipokuwa taa za nje, ndani mlikuwa giza. Chaurembo akaamini Karisa mumewe alikuwa usingizini*. inaashiria kuwa Karisa alikuwa akiathirika kwa kukosa na amani kwa kuwa mkewe Chaurembo alikuwa akirejea nyumbani usiku wa manane. Aliathirika kiasi cha kukosa hata usingizi. Mkewe anasema kuwa ndani ya nyumba mlikuwa na giza akaamini kuwa mumewe

alikuwa kesha lala. Lakini anapoingia Karisa anamwonya dhidi ya kutembea usiku. Chaurembo alikuwa akishiriki mapenzi nje ya ndoa. Kila siku alikutana na mpenzi wake wa kando aliyekuwa akichupa naye kutoka hoteli moja hadi nyingine wakila haramu tamu. Hili lilimsababisha kurudi nyumbani usiku wa manane na kudanganya kuwa mikutano kazini ilikuwa mingi. Mumewe Karisa hakuwa na amani kwa sababu yake kurejea usiku kwani usiku ulikuwa na wenyewe. Alimweleza mkewe kuwa *Huu mji siku hizi usiku una wenyewe* kumaanisha kuwa kulikuwa na wahuni na ilikuwa hatari yeye kutembea usiku. Alihofia kuwa jambo mbaya lingemtendekea mkewe. Akamwonya dhidi ya kutembea usiku. Hili linaonyesha kuwa Karisa hana amani.

*Kulikuwa na kimya kikuu. Isipokuwa taa za nje, ndani mlikuwa giza. Chaurembo akaamini Karisa mumewe alikuwa usingizini*. Sentensi hii inaashiria kuwa Marasa hakuwa na amani. Mkewe anasema kuwa alipofika nyumbani taa za ndani zilikuwa zimezimwa akaamini kuwa mumewe alikuwa usingizini lakini hakuwa amelala. Vilevile hakuwa na amani kwa kuwa hakujua mkewe alikuwa wapi na siku hizo kulikuwa na visa vya wahuni.

Kulingana na nadharia, kipengle cha uchumi na jinsia vilisababisha kunyanyasika na kuathirika kwa Karisa. Alinyanyasika kwa kuwa mwanamume kwani mkewe alikuwa akirejea usiku wa manane akitoka kumwona mpenzi wake wa kando. Karisa anaathirika kwa kukosa amani na usingizi. Anazima taa za ndani lakini halali. Mkewe anaporudi anafikiria kuwa mumewe amelala lakini Karisa hakuwa amelala. Aliogopa kuwa mji ulikuwa na wahuni na mkewe alikuwa akirejea usiku. Anamwonya dhidi ya kutembea usiku. Hii inaonyesha kuwa karisa hakuwa na amani. Aliogopa kuwa mkewe angepatana na wahuni kwa barabara wamtendee mabaya.

Katika hadithi ya ‘Masharti ya Kisasa’ katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, mhusika Dadi amesawiriwa kama asiye na amani. Dadi alilazimishwa kutia saini kwenye masharti ambayo hakuchukua muda kuyaelewa. Masharti haya yanamfanya kukaa bila amani. Dadi anamshuku Kidawa kuwa na uhusiano wa nje ya ndoa na hili linamkosesha amani zaidi. Mwandishi anasema:

Mfano 2:

> Hakuna jambo linalomkeketa ndani kwa ndani Dadi kama kuonekana na wanawake na wanaume mtaani kuwa yeye si mwanamume tosha kwa sababu ametiwa maganjani na kudhibitiwa na mkewe.

> Anapojitazama na kujipekua, Dadi huona ndiyo kwanza sasa atambue kuwa amedhibitiwa kikwelikweli. Ingawa Kidawa humwambia asaidie kazi za nyumba, na yeye Dadi hajaacha kusaidia, lakini hatosheki kamwe mwanamke huyo. Na si hatosheki tu, hataki kukubali kuwa mwanamume kazi zake ni za nje si za ndani. Na yeye akishiriki kazi za nyumba anafanya hisani tu. Na zaidi ni kwa vile anavyotaka kutimiza masharti aliyoyalia yamini mbali na mapenzi yasiyo mfano anayompenda Kidawa. (TL1, uk 60).

Sentensi *Hakuna jambo linalomkeketa ndani kwa ndani Dadi kama kuonekana na wanawake na wanaume mtaani kuwa yeye si mwanamume tosha kwa sababu ametiwa maganjani na kudhibitiwa na mkewe* Sentensi hii ina maana kuwa Dadi hakuwa na amani hata kidogo. Kilichosababisha haya ni masharti aliyokuwa ameyatia sahihi bila kuyaelewa. Yalimsababisha kufanya kazi mpaka za jikoni. Wanakijiji waume kwa wake walianza kumwona kama yeye si mwanamume kamili na hili lilimsababisha kuungulika ndani. Anachorwa kama asiye na amani. Mwandishi anasema hakuna jambo linalomkeketa Dadi kama kuonekana na wanawake na wanaume mtaani kuwa yeye si mwanamume tosha kwa sababu amethibitiwa na kutiwa viganjani na mke. Dadi amekuwa akifanya kazi za nyumba ambazo anasema ni za mwanamke kwa sababu za mwanamume ni za nje. Hili linasababisha yeye kutokuwa na amani kwa kuwa watu wanamsema huko nje. *Na yeye akishiriki kazi za nyumba anafanya hisani tu.*

Vilevile sentensi hii inaonyesha kuwa Dadi hakuwa na amani. *Na zaidi ni kwa vile anavyotaka kutimiza masharti aliyoyalia yamini mbali na mapenzi yasiyo mfano anayompenda Kidawa.* Sentensi hii inamaanisha kuwa hata kama Dadi alisaidia kazi za nyumba, ilikuwa shingo upande. Alifanya hili kwa vile alikuwa ameyatia sahihi masharti aliyopewa. Dadi alikosa amani. Dadi pia anamshuku mkewe Kidawa kuwa na uhusiano wa nje. Hili linachangia zaidi yeye kutokuwa na amani. Dadi anasema kuwa Kidawa anampa fedheha kwa kuwa hachoki kusimama na wanaume.

Kulingana na Patricia (1990) mwingiliano wa vipengele vya utambulisho husababisha ukandamizaji wa mtu pamoja na kuathirika. Kulingana na nadharia, kipengele cha uchumi, jinsia na matarajio ya kijamii vinashirikiana na kusababisha kunyanyasika na kuathirika kwa Dadi. Dadi ananyanyasika kwa sababu ya hali yake kama mwanamume. Anashuku kuwa mkewe ana mpango wa kando. Mkewe anafanya kazi

ya umetroni usiku na hili linamsababisha kufikiri kuwa ana mpango wa nje ya ndoa. Dadi anaanza kuathirika. Mwandishi anasema kuwa hakuna jambo linalomkeketa ndani kwa ndani Dadi kama kuonekana na wanawake na wanaume mtaani kuwa yeye si mwanamume tosha kwa sababu ametiwa maganjani na kudhibitiwa na mkewe. Hili linamsababisha kukosa amani. Dadi pia anamshuku mkewe Kidawa kuwa na uhusiano wa nje. Hili linachangia zaidi yeye kutokuwa na amani. Dadi anasema kuwa Kidawa anampa fedheha kwa kuwa hachoki kusimama na wanaume.

Ukosefu wa ndani huweza kuwa na madhara kwa mwanamume kama vile utulivu wa ndani. Kwa mujibu wa Olkayade (2014), tunamwona Karisa akikosa utulivu wa ndani na hivyo kukosa usingizi. Anaingia kwa nyumba na kuzima taa ili alale lakini hapati usingizi mpaka wakati mkewe anarejea.

### 4.4.4. Majeraha ya Mwili

Katika hadithi ya 'Masharti ya Kisasa' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* Mhusika Dadi anapata majeraha ya kimwili alipoanguka kutoka juu ya paipu. Mwandishi anasema:

Mfano 1:

> Chini, upande ule wa ubavuni kwenye ile paipu, tayari kulikuwa na kundi la watu limemzunguka mtu fulani. Alikuwa kalala chini kwenye kokoto na kupoteza fahamu. Kidawa alipopiga tochi alimkuta mumewe Dadi damu imemwenea kichwani. Mwalimu mkuu hakusita hapo kamwe. Haraka alikwenda kupiga simu kuita ambulensi. (TL, uk.68)

Sentensi *Alikuwa kalala chini kwenye kokoto na kupoteza fahamu* inamaanisha kuwa Dadi alikuwa amepata majeraha na kuumia. Dadi alikuwa anashuku kuwa mkewe alikuwa na mpango wa kando. Anakosa utulivu na kuamua kutafuta ushahidi kuwa mkewe ana mpenzi mwingine. Mkewe anajitayarisha kama kawaida ili kwenda kazini. Alikuwa akifanya kazi ya umetroni. Dadi anaona kuwa amepata nafasi ya kwenda kuthibitisha shaka alizokuwa nazo. Anaamua kumfuata bibiye. Alipofika katika ofisi ya Mwalimu mkuu, mkewe Kidawa alikuwa pamoja na mwalimu mkuu. Alipanda juu ya paipu kisha akaanguka na kupata majeraha. Dadi alianguka juu ya kokoto, akaumia na kupoteza fahamu. Watu wengi waliokuja kuona aliyekuwa amepanda juu ya paipu walimzingira Dadi. Kidawa walipofika na mwalimu mkuu na

kumlika kwa tochi, waliona Dadi aliyeanguka na kupata majeraha kisha kupoteza fahamu. Walipiga simu kuita ambulensi iliyompeleka hospitalini. Iwapo hangemfuata mkewe ili kuthibitisha usaliti wake, Dadi hangeanguka na kupata majeraha.

Mifumo ya ukandamizaji hushirikiana na kuathiri watu kwa njia nyingi. Ukandamizaji hauwezi kuchambuliwa kwa kutenganisha vipengele vya utambulisho wa mtu, bali kwa kuzingatia jinsi vinavyoshirikiana na kuathiriana kulingana na Crenshaw (1989). Kipengele cha jinsia na uchumi vinashirikiana katika kumwathiri Dadi kwa kupata majeraha mabaya. Dadi anampa mkewe uhuru wa kufanya kazi ya umetroni usiku. Baadaye kwa sababu ya ile hali ya kuwa mwanamume, Dadi anaanza kumshuku mkewe kuwa ana mpango wa kando na mwalimu mkuu. Anaamua kufanya uchunguzi ili kubaini iwapo mkewe anashiriki mapenzi nje ya ndoa. Hivyo, wanandoa wanafaa kuaminiana. Dadi hakumwamini mkewe hata alipojaribu kumweleza kuwa hana mapenzi nje ya ndoa. Mkewe hakuwa na mpango wa kando. Hata alikuwa tayari kuacha kazi ili aondoe mashaka ya mumewe.

Katika hadithi ya 'Mapenzi ya Kifaurongo' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* Dennis pia anapatwa na majeraha ya moyo alipofukuzwa na Penina kutoka kwake. Kiini cha kumfukuza ni kuwa alikuwa amekosa kazi. Mwandishi anasema:

Mfano 2:

> Nimekosa kazi katika kampuni hii! Siamini. Moyo unadunda kiasi kwamba nilihisi utanidondoka. Ninatoka ofisini kama mgonjwa mahututi. Miguu haishiki. Nimeweweseka kama ubua unaopeperushwa na upepo mkali. Tamaa yangu ya kuwa mwanahabari haina wokovu. Maskini nitawalipaje wazazi wangu wema walionitendea? Nani atawafaidi nguvu na jasho lao lililowamwagika wakijikusuru kunisomesha? Je, watakuja kufurahia matunda ya uzazi wao? Najiuliza maswali mengi lakini sijui vipi ningeweza kuyajibu, au nani angenijibia maswali haya (TL, uk. 27*)*

Sentensi *Moyo unadunda kiasi kwamba nilihisi utanidondoka. Ninatoka ofisini kama mgonjwa mahututi.* na *Ninatoka ofisini kama mgonjwa mahututi. Miguu haishiki. Nimeweweseka kama ubua unaopeperushwa na upepo mkali* zinaonyesha kuwa Dennis alikuwa na majeraha ya moyo. Penina mkewe alikuwa amemwumiza moyoni

kwani alimfukuza kwa sababu ya kukosa ajira. Alimwambia kuwa yeye si mpenzi wake na asimwambie yeyote kuwa aliwahi kuwa mpenziwe. Dennis anaumia moyoni na kuanza kujutia ufukara wake na kujiuliza kwa nini alimkubali Penina kuwa mpenzi. Anasema ameachwa bila mpenzi, hana rafiki, kisomo chake hakikumsaidia, anahofia wazazi wake. Anawahurumia kwa kuwa ni yeye aliyekuwa tegemeo la kuwatoa katika lindi la umaskini. Dennis alikuwa mwingi wa fikira. Anaumia moyoni.

Vilevile sentensi *Ninatoka ofisini kama mgonjwa mahututi. Miguu haishiki. Nimeweweseka kama ubua unaopeperushwa na upepo mkali* inaonyesha kiwango ambacho Dennis alikuwa ameumia. Anasema kuwa alikuwa kama mgonjwa mahututi, miguu yake haikuwa na nguvu na angeperushwa na upepo. Hii inaonyesha kuwa Dennis anaumia mwili na moyo kwa sababu ya hali yake. Katika jamii, wanaume hujipata katika hali kama hizi ambapo wanaumizwa na kupata majeraha ya mwili na pia ya moyo.

Maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi huathiri uzoefu wa ukandamizaji au ukosefu wa haki. Haya ni kulingana na Audre (1984). Kulingana na nadharia, Dennis anaathirika kwa sababu ya mwingiliano wa kipengele cha uchumi, matarajio ya kijamii na tabaka. Dennis hana kazi na ametoka tabaka la chini. Dennis anaathirika kwa kupata majeraha ya moyo alipokosa kazi katika kampuni alipokuwa ameenda kusaka ajira. Anaathirika moyo. Anasema moyo wake unadunda kiasi kwamba anahisi ungemdondoka. Hii inaonyesha kiasi moyo wake uliumia. Dennis alihisi anajukumu la kumtunza mkewe. Anatia bidii lakini hafanikiwi.  Hili linamsababisha moyo wake kuumia.

Kwa mujibu wa IPP Media (2017), majeraha ya mwili huwa na madhara kwa mwanamume kama vile**:** kupoteza uwezo wa kufanya kazi; majeraha makubwa kama kuvunjika kwa mifupa huweza kumzuia mwanamume kufanya kazi za kawaida au za kipato hivyo kushindwa kufanya majukumu yake kama mkimu familia. Jambo hili huweza kusababisha msongo wa mawazo na huzuni. Kukosa uwezo wa kufanya shughuli za kawaida huweza kusababisha hisia za kutengwa. Vilevile mwanamume anaweza kupoteza kujiamini. Mabadiliko ya mwonekano au uwezo wa mwili huweza kuathiri jinsi mwanamume anavyojiona na kuhusiana na wengine.

Mtafiti ana msimamo kuwa wanandoa wanafaa kuaminiana. Inadhihirika wazi kuwa kutoaminiana kuna madhara yake. Dadi hakumwamini mkewe hata alipojaribu kumweleza kuwa hana mapenzi nje ya ndoa. Mwishowe anapata majeraha na kupelekwa hospitalini. Madhara mengine ni kuwa mkewe alikuwa tayari kuacha kazi kwa kutoaminiwa na mumewe. Hili lingeleta matatizo kwani alichangia katika kutafuta riziki. Jamii inafaa kuelimishwa faida na hasara za kutoaminiana katika ndoa.

### 4.4.5. Upweke

Upweke ni hali ya kukaa katika maisha peke yako bila ya mshirika, mke au mume. Upweke unasababishwa na kukanwa na watu au jamii iliyo karibu na mhusika. Hata hivyo upweke huweza kusababishwa wakati mwanya umetokea kati ya mhusika na mhusishwa au wahusishwa. Pia vitendo vya kikatili vilivyoshuhudiwa na mtu vinamfanya awe katika hali ya upweke kwa kuhofia kuwa chochote kinaweza kutokea kwa njia isiyomfurahisha.

Katika hadithi ya 'Ndoto ya Mashaka' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* tunamwona mhusika Mashaka akiwa na upweke baada ya familia yake kupotea. Mashaka siku moja alienda kazini lakini aliporudi hakuipata familia yake, mke wake na watoto wake. Alisubiri warudi lakini hawakurudi. Akawatafuta lakini hakufaulu. Mwandishi anasema kuwa:

Mfano 1:

> Niliwaza mengi zaidi. Nikawaza la laiti ningekuwa na maisha mazuri, mambo yote yangekuwa mazuri. Kwanza, Waridi mke wangu, angeniheshimu. Asingekuwa na wazo la kunikimbia na kuniachia ukiwa nilio nao leo. Ningekuwa na fedha za kumfurahisha yeye na Watoto wangu. Ningeweza kuuzima udhia ukitokea kuupenyezea rupia. Bila shaka ningekuwa mwanamume wa kukata na shoka, imara na mwenye kujiamini. Pili, mke wangu angezidi kunipenda nami ningezidi kufurahia mapenzi yetu. Hata mwenyewe ningejipenda. Na watoto wangu ningewapenda pia. Lakini wapi! Tangu lini maskini akapenda? Maskini kabisa hapendi! (TL 1 uk.78)

Sentensi *Asingekuwa na wazo la kunikimbia na kuniachia ukiwa nilio nao leo* inaonyesha kuwa Mashaka alikuwa na upweke. Mkewe alikuwa amemkimbia pamoja na watoto wao na kumwachia ukiwa. Hili lilisababisha yeye kuwaza mengi. Anawaza

kuwa angekuwa na pesa mkewe hangemtoroka. Angemwonyesha mkewe mapenzi azidi kumpenda pamoja na wanawe. Hili linaonyesha kuwa alikuwa na upweke. Mke wake na watoto wake walitoroka kwa sababu ya umaskini wake. Huku kuishi peke yake kunampa wingi wa mawazo. Anajutia umaskini unaomfanya kuishi pweke. Anasema iwapo alikuwa na pesa mkewe hangemtoroka. Kuwa angezidi kumpenda. Angejipenda pia lakini anashangaa na kujiuliza tangu lini maskini apende lolote. Katika jamii wanaume wengi hujipata katika hali ya ukiwa wanapoachwa na familia zao. Hakuna binadamu anayependa kuishi peke yake.

Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho, vipengele vya utambulisho hushirikiana na kuathiriana katika ukandamizaji wa mtu kwa mujibu wa Crenshaw (1989). Kulingana na nadharia, kipengele cha uchumi na tabaka vinashirikiana katika kuathirika kwa Mashaka. Mashaka hana kazi, yupo katika tabaka la chini. Mashaka anaathirika sana anapotorokwa na mkewe pamoja na wanawe. Anasema angekuwa na pesa mkewe hangemtoroka na kumwachia ukiwa alio kuwa nao. Hili linathibitisha kuwa aliathirika kwa kuhisi pweke. Jioni moja anaporejea nyumbani, anampata mkewe hayuko. Mashaka anawaza mengi kuwa iwapo angekuwa na pesa hangemtoroka kwani angeweza kumfurahisha pamoja na wanawe. Anawatafuta kwa siku nyingi lakini hawapati. Anaishia kuishi peke yake jambo ambalo linamhuzumisha sana. Anaathirika kwa kuhisi upweke mwingi.

Katika hadithi ya ‘Mapenzi ya Kifaurongo’ katika *Diwani ya Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, tunamwona Dennis akiwa katika hali ya upweke anapofukuzwa na mpenziwe Penina. Mwandishi anasema kuwa:

Mfano 2:

> Sasa nayakumbuka maneno ya mhadhiri wetu Dkt Mabonga kwamba binadamu mwenyewe amegeuka kuwa kupe. Analaza damu usiku na mchana… sijui kama mimi ndiye kupe mlazadamu anayetegemea Penina au Penina ndiye kupe anayenitegemea mimi. Kukosa kazi kwangu kumeyafifisha mapenzi yake ya kifaurongo. Nimeachwa mchege. Sina kazi sina bazi. Sina mpenzi sina rafiki. Mama na baba wanakula mwata nyumbani. Elimu niliyoisoma haileti matumaini lakini sasa nimeanza kuuelewa ulimwengu. (TL 2 uk.28)

Sentensi *Kukosa kazi kwangu kumeyafifisha mapenzi yake ya kifaurongo. Nimeachwa mchege. Sina kazi sina bazi. Sina mpenzi sina rafiki* zinaonyesha kuwa Dennis anajihisi pweke. Anasema kuwa ameachwa mchege, hana kazi hana bazi, hana mpenzi hana rafiki. Rafiki husaidia mtu anapojisikia pweke. Kuzungumza na mtu wa karibu hufanya mtu ajihisi kuwa matatizo aliyokuwa nayo au mawazo yamepungua. Mambo ni tofauti kwa Dennis kwa kuwa anasema hana mpenzi tu bali pia rafiki hana. Anaona amepoteza kila kitu hii ni baada ya kuachwa na mpenziwe kwa sababu ya kukosa kazi. Alipoteza matumaini. Anaanza kuwahurumia wazazi wake ambao wamemsomesha kwa kujikaza kwingi lakini hajaweza kuwasaidia. Anasema hajui kesho yake itakuwa vipi. Akijaliwa kumpata mke atakayeridhi uchochole wake atafurahia, lakini akikosa atashukuru. Hii inaonyesha kuwa amekuwa mpweke mpaka anatamani ajaliwe kumpata mke mwingine. Huu ni ukweli wa mambo kuwa wanaume wengi huachwa na familia zao na kujihisi pweke. Hili hutendeka mwanamume anaposhindwa kuikimu familia yake.

Patricia (1990) alianzisha dhana ya matriki ya utawala ambayo inaeleza jinsi vipengele vya utambulisho kama jinsia, rangi, na tabaka vinavyoathiriana na kuunda mifumo ya ukandamizaji. Kulingana na nadharia, kipengele cha uchumi na tabaka vinashirikiana na kumwathiri Dennis. Dennis alikuwa na mpenzi Penina anayemfukuza baada ya kukosa kazi. Dennis hakuwa na kazi na alikuwa maskini sana. Mwanzoni, Penina aliyagharamia mahitaji ya nyumba kwa kuwa wazazi wake walimtumia pesa ya mahitaji kila mwisho wa mwezi. Dennis naye alitia bidii sana katika kutafuta ajira. Baadaye hafanikiwi na anafurushwa nyumbani. Dennis anaathirika kwa kupata upweke mwingi. Anakiri haya kwa kusema kuwa ameachwa mchege. Hana kazi hana bazi. hana mpenzi hana rafiki. Hili linadhihirisha kuwa ana upweke mwingi kwani anasema kuwa hana mpenzi hana rafiki.

Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na ya Ernest na wenzake (2021) walioonelea kuwa upweke huwa na madhara kwa mwanamume. Madhara haya ni kama vile: msongo wa mawazo, wasiwasi na matatizo ya kisaikolojia. Pia unaweza kuwa na madhara kama fikra za kujitoa uhai. Wanaume wanaokumbwa na upweke wa muda mrefu wako katika hatari kubwa ya kupata fikira za kujitoa uhai, hasa katika jamii ambazo kujieleza kihisia huonekana kama udhaifu na hukataliwa kijamii.

### 4.4.6. Kusambaratika kwa Asasi ya Ndoa

Udhalilishaji unaotendewa wanaume husababisha ndoa kukosa lengo kwa wawili waliooana ili waishi kwa pamoja. Ndoa inakosa ladha na kuwatawanya wapenzi wasiwe na mshikamano.

Katika hadithi ya 'Mapenzi ya Kifaurongo' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, tunaona ndoa kati ya Dennis na Penina ikisambaratika Dennis anapokosa kazi na Penina kumfukuza. Mwandishi anasema:

Mfano 1:

> Wazazi wangu walikuwa wamenionya dhidi ya kuchumbiwa nawe. Nikawapuuza. Sasa nimekuja kujua walichomaanisha. Maneno yao yamenisibu. Kwa sababu hii, sioni haja yoyote ya kuishi nawe. Naomba tafadhali uchukue chochote unachokiona chako na ujiendee zako (TL 1, uk. 26)

Katika dondoo maneno*, walikuwa wamenionya dhidi ya kuchumbiwa nawe, sioni haja yoyote ya kuishi nawe, Naomba tafadhali uchukue chochote unachokiona chako na ujiendee zako*, yanaonyesha kuwa ndoa kati ya Penina na Dennis ilisambaratika. Wazazi wa Penina walikuwa wamemuonya dhidi ya kuchumbiwa na Dennis kumaanisha kuwa hawakuwa wameibariki ndoa hiyo. Walikataa kuikubali ndoa hii kwa kuwa Dennis alikuwa maskini. Wao walikuwa tajiri. Walimpa Penina pesa za kila mwezi na kuwalipia kodi ya nyumba pia. Penina alipowaeleza kuwa amepata mchumba, wanamkataza kuchumbiwa naye kwa madai kuwa yeye ni maskini. Penina anapogundua kuwa matamanio yake hayakufaulu, anamfukuza. Anamweleza pia kuwa wazazi wake walikuwa wamemwonya kuchumbiwa naye. Kwa hivyo Dennis anapokosa kazi, anamfukuza. Anamwomba Dennis achukue kilicho chake ajiendee. Anamweleza kuwa haoni haja ya kuishi naye hivyo anamfukuza na kuisambaratisha ndoa yao. Hili linasababisha Penina kumfukuza nyumbani kwa madai kuwa hata wazazi wake hawakumkubali. Ndoa yao inaishia kusambaratika kwa sababu ya Penina kukosa ustahimilivu. Angemstahimili mumewe mpaka wakati atakapofanikiwa katika kupata ajira.

Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho iliyoasisiwa na Crenshaw (1989), vipengele vya tabaka na matarajio ya kijamii vinashirikiana katika kumwathiri Dennis. Dennis ametoka tabaka la chini naye Penina ametoka tabaka la juu. Kulingana

na jamii, mwanamume ana jukumu la kuilisha familia yake. Kwa kuwa Dennis alitoka tabaka la chini, wazazi wa Penina waliona kuwa Dennis ni maskini hivyo hangeweza kumtunza Penina. Wakamwonya Penina dhidi ya kuolewa na Dennis. Hili linasambaratisha ndoa yao na Dennis anaathirika sana kwa kujuta hali yake umaskini na kuyakubali mapenzi ya Penina. Penina anamfukuza na kumweleza kuwa anajuta kuwa mpenzi wake kwani wazazi wake walimwonya dhidi ya kuolewa naye. Penina anamfukuza kwa kumwambia achukue chochote kilicho chake ajiendee. Dennis anaathirika kwa sababu ya ndoa yake kuvunjika. Anashangaa iwapo huyo ni Penina aliyemwendea awali na kushawishi wawe wapenzi.

Katika hadithi ya 'Ndoto ya Mashaka' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, mhusika Mashaka pia anaumia. Ndoa yake ilikuwa imesambaratika na akaachwa na mpenzi wake Waridi pamoja na watoto wake.

Mfano 2:

> Katika maisha hayo siku zilijisotora zikapita kama hazitaki. Sura zetu zilitosha kuwa kurasa za kusomea. Dhiki ilikuwa ndiyo nguo na harufu yetu. Siku moja lakini nilishangaa nilipotoka kazini. Waridi sikumkuta mle chumbani mwetu. *Sikuona ndudu ya mtu!* Sikumwona yeye wala watoto wake. "Wamekwenda wapi watu hawa?" Nilijiuliza lakini sikupata jibu. Nilisubiri sana hawakutokea. Waridi mwenyewe hakuniaga. Niliendelea tu kuwasaka lakini wapi! Juhudi zangu za kuwasaka, mke na watoto wangu, ziligonga mwamba hatimaye. Na sikujua vipi. (TL, uk. 76)

Sentensi *Siku moja lakini nilishangaa nilipotoka kazini. Waridi sikumkuta mle chumbani mwetu, Sikumwona yeye wala watoto wake, Nilisubiri sana hawakutokea, Niliendelea tu kuwasaka lakini wapi! Juhudi zangu za kuwasaka, mke na watoto wangu, ziligonga mwamba hatimaye* zinaonyesha kuwa mkewe Mashaka pamoja na watoto walikuwa wamepotea na ndoa yake kusambaratika Tunamwona Mashaka akiwa mwingi wa mawazo. Ndoa yake ilikuwa imesambaratika na mke wake kupotea. Anasema kuwa aliwatafuta kwa siku nyingi bila kuwapata. Kilichosababisha yeye kutorokwa na mke na ndoa yake kusambaratika ni umaskini wake. Mashaka alikuwa maskini sana. Hakuweza kuilisha familia yake. Mpaka wazazi wa mkewe walikuwa wameondoka walikoishi na kwenda kuishi Yemeni kwa sababu ya ufukara wa

Mashaka. Ufukara huu ulimletea matatizo na kuisambaratisha ndoa yake. Hili lilimhuzunisha. Mashaka anasema angekuwa na pesa mkewe angempenda, naye angempenda. Hili halitendeki mpaka anaishia kusema kuwa maskini hapendwi. Ni uhalisia wa mambo kuwa ndoa nyingi zinasambaratika kwa sababu ya wanaume kushindwa kulisha familia zao.

Kulingana na Audre (1984) maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi husababisha ukandamizaji. Kulingana na nadharia, Mashaka anaathirika kwa sababu ya kipengele cha tabaka na uchumi. Mashaka ni maskini. Anafanya kazi za kijungujiko. Siku moja anaporejea nyumbani anampata mkewe kesha toroka pamoja na wanawe. Mashaka ananyanyasika na kuathirika. Anasema kuwa siku moja alishangaa alipotoka kazini. Waridi hakumkuta mle chumbani mwao. Hakumwona yeye wala watoto wake. Alishangaa wamekwenda wapi watu hao. Alijiuliza maswali mengi lakini hakupata jibu. Aliwasubiri sana hawakutokea. Waridi mwenyewe hakumuaga. Aliendelea tu kuwasaka lakini wapi! Juhudi zake za kuwasaka, mke na watoto wake, zikagonga mwamba hatimaye. Na hakujua vipi. Mashaka anaonekana kuathirika kwa sababu ya familia yake kutoroka. Aliwatafuta siku nyingi hakuwapata na hili lilisambaratisha ndoa yao.

Kusambaratika kwa ndoa huweza kuwa na madhara kwa mwanamume. Huweza kusababisha msongo wa mawazo na hisia za kukosa mamlaka. Jamii pia huwazuia wanaume kutafuta msaada wa kihisia, jambo linaloongeza athari za kiakili kutokana na mgogoro wa kifamilia kwa mujibu wa (Hine na wengine, 2025).

Mtafiti ana msimamo kuwa wanajamii wanafaa kuhamasishwa kuwa wanaume ni binadamu kama wengine. Jamii ihamasishwe kuwa wanaume wanaponyanyasika pia huathirika kihisia, kimwili na hata kisaikolojia. Jamii ielimishwe kuwa kunyanyasika na kuathirika huku huweza kusambaratisha asasi ya ndoa wanaume wanapoathirika.

### 4.4.7. Msongo wa Mawazo

Msongo wa mawazo husababishwa na jambo au kitu chochote ambacho kinaleta usumbufu kwenye mawazo ya binadamu. Kuna dalili ambazo huonekana kwenye mtu anapokuwa na msukumo wa mawazo. Dalili hizi ni pamoja na kulia, huzuni, ukali, unyonge, kutomakinika katika ulifanyalo, mabadiliko katika mavazi na namna ya kuongea miongoni mwa dalili zingine.

Katika hadithi ya 'Ndoto ya Mashaka' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba* na *Hadithi Nyingine,* Mashaka anaonekana akiwa mwingi wa mawazo. Siku moja akitoka kazini alipata mkewe Waridi amepotea pamoja na watoto wake. Aliwasubiri hawakurudi. Akawatafuta juhudi zake zikagonga mwamba. Mwandishi anasema kuwa hali hii ya utengano na familia yake ilimfanya mnyonge na kumyong'onyeza. Mashaka aliwaza mengi.

Mfano 1:

> Niliwaza mengi zaidi. Nikawaza la laiti ningekuwa na maisha mazuri, mambo yote yangekuwa mazuri. Kwanza, Waridi mke wangu, angeniheshimu. Asingekuwa na wazo la kunikimbia na kuniachia ukiwa nilio nao leo. Ningekuwa na fedha za kumfurahisha yeye na Watoto wangu. Ningeweza kuuzima udhia ukitokea kuupenyezea rupia. Bila shaka ningekuwa mwanamume wa kukata na shoka, imara na mwenye kujiamini. Pili, mke wangu angezidi kunipenda nami ningezidi kufurahia mapenzi yetu. Hata mwenyewe ningejipenda. Na watoto wangu ningewapenda pia. Lakini wapi! Tangu lini maskini akapenda? Maskini kabisa hapendi! (TL 1, uk. 78)

Sentensi *Niliwaza mengi zaidi,* na *Nikawaza la laiti ningekuwa na maisha mazuri, mambo yote yangekuwa mazuri.* zinaonyesha kuwa Mashaka alikuwa na msongo wa mawazo. Mkewe na wanawe walipotea kwa kuwa alikuwa maskini. Anasema kuwa angekuwa na pesa mke wake angemheshimu na hangekimbia na kumwacha. Anasema angeweza kumfurahisha pamoja na wanawe angekuwa na fedha. Anasema angekuwa mwanamume wa kukata na shoka na angejiamini kumaanisha kuwa sasa amejidharau na hajiamini. Mashaka pia hajipendi. Anasema angekuwa na pesa angejipenda. Anawaza kiasi kwamba yeye anajiita maskini. Anasikitikia hali yake inayomnyima furaha. Familia yake kupotea inamfanya kuwa na msongo wa mawazo. Mwandishi anaendelea kusema:

Mfano 2:

> Nilizidi kuwaza na kuwazua. Niliwaza juu ya mashaka yangu mwenyewe kwanza-mimi Mashaka kisha nikajiuliza kuna Mashaka wangapi Tandale nilipo? Sote tulikuwa mashaka watupu, Tandale nzima. Na je, kuna Tandale ngapi katika Tanzania? Kuna Mashaka

> wangapi Kenya na Uganda na Afrika nzima na duniani kote. Na hatimaye kwa nini jamiiza kimataifa zinalifumbia jicho kina Mashaka na Tandale? Kwa nini hazitaki kuukemea mfumo huu wa maisha? Mfumo wa mwenye nacho kuendelea kupata na msinacho kuendelea kukosa? Labda si bure, iko namna! Je, jamii hizo zina mkono wake katika hili? Kwa nini…Kwa nini…kwa nini lakini? Nilipokuwa nikiwaza haya, nafsi yangu iliniambia, *Subira ni ufunguo wa heri*. (TL 2, uk. 78)

Katika nukuu hili Mashaka anazidi kuwaza mengi. Sentensi *Nilizidi kuwaza na kuwazua* na *Niliwaza juu ya mashaka yangu mwenyewe kwanza-mimi Mashaka kisha nikajiuliza kuna Mashaka wangapi* zinaonyesha kuwa mawazo hayakumwishia Mashaka. Alifikiria kuhusu shida zake kisha akaanza kujiuliza kuna Mashaka wangapi wanaopitia hali kama hiyo yake. Alijiuliza kwa nini walizo nazo wanazidi kupata na wasio nazo kuzidi kukosa. Moyo wake hautulii. Mawazo haya yote yalimfanya Mashaka kuwa mnyonge sana. Wanaume wengi katika jamii hujipata katika hali kama hii pale ambapo wanashindwa kuzikimu familia zao hivyo wanatorokwa.

Crenshaw (1989) alieleza jinsi mifumo ya ukandamizaji inavyoshirikiana na kuathiri watu kwa njia nyingi. Alisema kuwa ukandamizaji hauwezi kuchambuliwa kwa kutenganisha vipengele vya utambulisho wa mtu, bali kwa kuzingatia jinsi vinavyoshirikiana na kuathiriana. Kulingana na nadharia, Mashaka anaathirika kwa sababu ya mwingiliano wa kipengele cha matarajio ya kijamii na tabaka. Mashaka alikuwa na jukumu la kuilisha familia yake lakini hakuweza kufanya hivyo kwa kuwa alikuwa maskini. Alikuwa akifanya kazi lakini zilikuwa kazi za kijungu jiko. Hili linasababisha kutorokwa na familia yake na anapata msongo wa mawazo. Anasema kuwa aliwaza mengi zaidi. Akawaza ya laiti angekuwa na maisha mazuri, mambo yote yangekuwa mazuri. Anasema angeweza kumfurahisha mkewe pamoja na wanawe na hivyo hawangemtoroka. Mashaka alizidi kuwaza mengi. Anasema alizidi kuwaza na kuwazua. Aliwaza juu ya mashaka yake mwenyewe kisha akajiuliza kuna Mashaka wangapi Tandale alipo wanaopitia madhila kama aliyopatana nayo. Hili linaashiria kuwa Mashaka alikuwa na msongo wa mawazo. Mwanzo aliwaza mengi kujihusu kisha akaanza kuwaza ya wengine. Kuwaza ya wengine hakungemsaidia kwa lolote isipokuwa kumwongezea matatizo zaidi.

Kulingana na (Schön na wengine 2025), msongo wa mawazo huweza kuwa na madhara kwa mwanamume kama kupata mawazo ya kujiua. Kulingana na takwimu, wanaume wana uwezekano mkubwa wa kufariki kwa kujiua mara nyingi kutokana na ukosefu wa matibabu. Vilevile wanaweza kujidhalilisha kwa kuona kama wamefeli maishani. Pia wanaweza kukasirika na kuwa na hasira. Badala ya kuonyesha huzuni ya moja kwa moja, wanaume mara nyingi huonyesha dalili za unyogovu kupitia hasira au kukasirika kupita kiasi.

### 4.5. Mbinu Wanazotumia Wanaume Kupambana Dhidi ya Unyanyasikaji

Sehemu hii imeongozwa na madhumuni ya tatu ambayo ni kubainisha mbinu wanazotumia wanaume kupigana dhidi ya unyanyasikaji wanaopitia.

#### 4.5.1. Kuvumilia au Ustoa

Kulingana na Grych (2020) kuvumilia ni kustahimili hali ngumu au yenye maumivu bila kuvunjika moyo, kukata tamaa au kuchukua hatua mbaya. Wanaume wanapokabiliwa na unyanyasikaji wa aina mbalimbali huweza kuvumilia na kunyamaza. Kunyamaza huku kunaletwa na hali walimokulia iliyowatengea nafasi ya juu katika familia na hadhi yenye mamlaka. Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho, ubabedume huathiri mwanamume kwa kuwa humfanya ajichukulie kama mtu anayepaswa kujitegemea katika jamii. Kulingana na matarajio ya kijamii mwanamume anapaswa kuwa mkakamavu katika kukabiliana na changamoto anazozipitia bila kudhihirisha udhaifu wowote. Jamii hutarajia kwamba mwanamume hapaswi kudhihirisha hisia kama vile kulia hasa anapopitia magumu. Kwa sababu ya matarajio haya ya kijamii, mwanamume hunyamaza na kuvumilia shida zake na kujipa matumaini.

Katika hadithi ya ‘Mapenzi ya Kifaurongo’, tunamwona mhusika Dennis akipatana na hali ngumu ya kukosa kazi. Lakini anaamua kuvumilia na kupambana na hali ngumu ya maisha. Msimulizi anasema:

> Mimi na Penina tunaishi katika mtaa wa New Zealand. Huu ni mtaa wa watu wenye mapato ya kadri. Hatujaoana. Lakini kodi yetu hulipwa na wazazi wa Penina kwa kuwa bado hatujapata kazi. Mara nyingi naona aibu, lakini najipa matumaini, moyo wa kuvumilia na kupigana. Penina naye ni mvumilivu kwelikweli. Kusema kweli si vyema kuendelea kuishi pamoja bila kuwa tumeoana. Hata hivyo mipango

> ingalipo. Nina tamaa kubwa ya kupata kazi na anayenipa msukumo huu ni mchumba wangu Penina. Penina anasema hawezi kuolewa na mwanamume asiye na kazi yenye mshahara mkubwa. Hilo hunishangaza sana ingawa hunimakinisha katika tafutatafuta zangu. (TL 1, uk. 22)

Sentensi *naona aibu, lakini najipa matumaini, moyo wa kuvumilia na kupigana*. na *Hilo hunishangaza sana ingawa hunimakinisha katika tafutatafuta zangu* yanaonyesha kuwa kuna jambo ambalo linamsumbua Dennis lakini anaamua kuvumilia. Anasema kuwa anaona aibu kwa kuwa kodi ya nyumba yao inalipwa na wazazi wa Penina kwa kuwa wao hawana kazi. Bila shaka jambo hili linamsumbua kwa kuwa mwanamume hutarajiwa kuwa kiongozi wa boma hivyo anafaa kushughulikia mahitaji ya familia yake. Jambo hili linampa wasiwasi lakini anaamua kuvumilia na kujipa matumaini. Vilevile ana wasiwasi kwa kuwa mpenziwe Penina alisema kuwa hawezi kuolewa na mwanamume asiye na kazi yenye mshahara mkubwa. Dennis anasema kuwa jambo hili humshangaza  ingawa linamfanya makini katika kutafuta kazi. Dennis hakati tamaa kwa kuwa hana kazi. Anavumilia na kujiaminia kuwa mambo yatakuwa shwari. Ingawa Dennis anavumilia, baadaye anaishia kufukuzwa nyumbani na Penina kwa kukosa kazi.

Kulingana na Crenshaw (1989), kipengele cha uchumi na tabaka vinashirikiana na kusababisha kunyanyasika kwa mwanamume. Kwa mfano, Dennis ameathirika kiuchumi na kusawiriwa kama aliye katika tabaka la chini ambalo linamsababishia kudhalilishwa na mkewe. Ili kukabiliana na udhalilishwaji huu, anavumilia yale yote anayopitia. Anasema kuwa mara nyingi huona aibu, lakini anajipa matumaini, moyo wa kuvumilia na kupigana. Anafanya jitihada za kujitafutia ajira lakini mkewe haelewi kikamilifu changamoto anazozipitia kama mwanamume. Badala ya kutambua juhudi zake anamfurusha nyumbani. Hivyo kuvumilia na kujipa matumaini si suluhu kamili bila kutafuta msaada wa kudumu kama vile ushauri nasaha.

Katika hadithi ya ‘Ndoto ya Mashaka’, katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, Mashaka vilevile anayavumilia masaibu yanayompata. Siku moja anaenda kazini lakini anaporudi kutoka kazini, anapata kuwa mke wake pamoja na watoto wamemtoroka. Anawasubiri lakini hawarudi. Anawatafuta kwa muda lakini juhudi zake zinagonga mwamba. Anamua kuvumilia yanayompata. Mwandishi anasema:

> Nikaona fikra za nafsi yangu zimeendana na zile za moyo wangu uliokwisha kutamauka. Nilizaliwa kichanga, nikawa mtoto koroto kisha nikakua na kuota ndoto. Barobaro zima nikawa. Nikaoa na kuishi ndani ya uzio wa ndoa. Nikazaa kama nilivyozaliwa mimi, tena watoto si haba. Nikakaa na mke wangu mpaka pale aliponiacha. Mangapi hayo? Na yote katika mashaka na dhiki kubwa. Nikavumilia na kuendelea kusubiri kesho mambo huenda yakawa mazuri. Lakini mawe! Kila uchao ikawa afadhali ya jana ambayo haikuwa na afadhali kitu. (TL, uk. 79)

Sentensi *Nikavumilia na kuendelea kusubiri huenda kesho mambo yakawa mazuri* inaonyesha kuwa Mashaka alivumilia aliyoyapitia huku akijipa matumaini. Mashaka anajiliwaza kuwa amepitia mengi na pia kufanya mengi. Shida alipatana nazo lakini akavumilia na hata sasa anajipa moyo na kusubiri iwapo mke wake na watoto wake wangerejea. Anajiambia atazidi kuvumilia kwani huenda mambo yakawa mazuri siku moja.

Kulingana na Audre (1984), vipengele vya matarajio ya kijamii, uchumi na tabaka vinaingiliana na kusababisha kunyanyasika na kuathirika kwa Mashaka lakini anaamua kuvumilia. Mashaka yuko katika tabaka la chini. Anafanya kazi za kijungujiko hivyo kutotimiza mahitaji ya familia yake vizuri. Jambo hili linasababisha kusambaratika kwa ndoa yake kwani mkewe Waridi na wanawe wanamtoroka na kumsababishia upweke mwingi. Mashaka anawatafuta kwa siku nyingi bila mafanikio. Hata hivyo Mashaka anaamua kuvumilia yote aliyoyapitia. Kulingana na msimulizi kuvumilia si suluhu dhabiti ya kutatua unyanyasikaji na kuathirika kwa wanaume kwani alizidi kusema kuwa baada ya kuvumilia, mambo yalizidi kuwa mawe. Kila uchao hali ilizidi kuzorota. Hivyo badala ya kuvumilia, ni muhimu kutafuta msaada kutoka kwa wanasaikolojia. Kulingana na Mtazamo wa Afya wa Adena (2025) kutafuta ushauri wa kisaikolojia si udhaifu kama inavyodhaniwa bali ni hatua ya kishujaa na ya kujitahidi katika kupigana dhidi ya unyanyasikaji wa wanaume.

Kulingana na msimulizi, mbinu hii ya kuvumilia na ustoa ina udhaifu wake. Si suluhu dhabiti ya kutatua unyanyasikaji na kuathirika kwa wanaume kwani Mashaka alizidi kusema kuwa baada ya kuvumilia, mambo yalizidi kuwa mawe. Kila uchao hali ilizidi kuzorota. Kwa hivyo badala ya kuvumilia, ni muhimu kutafuta msaada kutoka kwa

wanasaikolojia. Kulingana na Mtazamo wa Afya wa Adena (2025) kutafuta ushauri wa kisaikolojia si udhaifu kama inavyodhaniwa bali ni hatua ya kishujaa na ya kujitahidi katika kupigana dhidi ya unyanyasikaji wa wanaume. Wanaume wanaponyanyasika hawafai kuvumilia na kunyamaza tu kwani tatizo lao bado huwa halijasuluhishwa. Jambo hili huweza kuleta msongo wa mawazo. Wanahitajika kutafuta ushauri nasaha kutoka kwa wataalamu.

### 4.5.2. Kuchunguza na Kuchukua Hatua Hatari

Berlyne (1960) alieleza kuchunguza kama hisia ya kimsingi inayosaidia kugundua, kujifunza na kuachana na msisimko wa kisaikolojia. Vilevile, ni kile kitendo cha kutafiti kuhusu jambo ili kuweza kubaini ukweli. Baadhi ya wanaume wanaponyanyasika huchukua hatua ya kuchunguza lile wanaloshuku kabla ya kuchukua hatua yoyote. Kwa mfano:

Katika hadithi ya ‘Masharti ya Kisasa’, mhusika Dadi ana shaka kuwa mkewe Kidawa anamwendea kinyume. Dadi anaamua kuchunguza ili aweze kujua ukweli wa mambo. Mwandishi anasema:

> Lakini Dadi alikwisha amua. Vyovyote itakavyokuwa, lazima autekeleze mpango wake. Na liwe liwalo. Alipotoka Kidawa tu, Dadi aliingia ndani akavaa nguo na kumfuata mkewe. Kwanza alipanga apite nyumbani kwa mwalimu mkuu, amtazame kama yuko kwake au la. (TL, uk.66)

Sentensi *Lakini Dadi alikwisha amua. Vyovyote itakavyokuwa, lazima autekeleze mpango wake*. *Na liwe liwalo..*. zinaonyesha kuwa Dadi alikuwa ameamua kuwa lazima amchunguze mkewe Kidawa. Alichukua hatua ya kimaksudi kuonyesha kufanya uamuzi usioyumbishwa. Dadi alikuwa akimshuku Kidawa kuwa hakuwa mwaminifu na alikuwa na uhusiano na mwalimu mkuu. Siku moja mkewe alipoenda kazini, Dadi aliamua kumfuata. Alijisemea kuwa, kwanza angepitia nyumbani kwa mwalimu mkuu ajue iwapo yupo. Kama hangekuwepo basi angemfuata shuleni. Dadi alipofika kwa mwalimi mkuu, hakumpata. Akaamua kwenda shuleni. Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho uamuzi wa Dadi hauchochewi tu na hisia binafsi bali pia na vipengele vya kijinsia, ubabedume na matarajio ya kijamii. Kutokana na ubabedume anaona ni wajibu wake kufuata mkewe popote alipo. Hivyo, hali hii inamchochea kuchukua hatua hatari kwa madai kuwa anailinda nafasi yake

katika jamii. Maamuzi hayo yanamsababishia maumivu makali baadaye hali inayomlazimu kupelekwa hospitalini kwa ajili ya matibabu. Mwandishi anasema:

> Dadi alikwisha 'talii' zamani wepesi wa kuipanda paipu ile, lakini alihofia jambo moja kubwa. Ijapokuwa upande ule ni wa kichochoroni na kwa hivyo si mno kupitapita watu, kama ingetokezea kupita na kumwona anaparamia paipu ile, angefikiriwaje? Aaaa, hilo halitokei. Wacha kuitaita bahati mbaya Dadi. Alijiambia mwenyewe kwa mwenyewe. Atawahi kupanda ile paipu mpaka juu achungulie vituko vinavyoendelea baina ya mkewe na mwalimu mkuu. (TL, uk. 69)

Katika kifungu hiki, sentensi inayosema *"Dadi alikwisha 'talii' zamani wepesi wa kuipanda paipu ile, lakini alihofia jambo moja kubwa…kama ingetokezea kupita na kumwona anaparamia paipu ile, angefikiriwaje?"* inadhihirisha mgongano wa ndani unaomsumbua. Sentensi hii inaibua taswira ya unyanyasikaji wa kihisia na kimfumo unaotokana na matarajio ya kijamii, hasa katika jamii zenye misingi ya ubabedume. Dadi anajitahidi kupambana na hali ya kudhalilishwa, lakini anajikuta amenaswa katika mtego wa matarajio ya kijamii yanayomwelekeza kuona aibu kutekeleza kitendo cha kujikomboa hadharani. Hofu ya kuonekana akiparamia paipu inaonyesha namna anavyojitambua kulingana na nafasi yake ya kijinsia, hadhi ya ndoa, na matarajio ya heshima ya kitamaduni.

Kwa mujibu wa Patricia (1990), hali ya Dadi ni zao la mwingiliano wa vitambulisho mbalimbali kama vile: jinsia, nafasi ya kifamilia, na matarajio ya kijamii vinaunda mazingira ya kimya kinachomzuia Dadi kuonyesha udhaifu au kuomba msaada. Ubabedume unaomzingira unamsababisha Dadi kuteseka kihisia kwani mfumo huo hauwaruhusu wanaume kuonyesha hisia zao waziwazi. Badala yake, analazimika kudhibiti maumivu yake kimyakimya, jambo linalompeleka kuchukua hatua ya hatari inayozua madhara makubwa kwake. Kwa hivyo, kifungu hiki kinaeleza kwa kina jinsi miundo ya kijamii na kitamaduni inaweza kushinikiza mtu kujinyima uhuru wa kujieleza na kujiokoa.

Kwa hivyo, ni muhimu kufanya maamuzi yanayozingatia heshima binafsi na ustawi wa kiakili, badala ya kujiingiza katika hatua za haraka au zenye hatari kwa sababu ya shinikizo la kijamii. Bandura (1997) alieleza kuwa mtu anapaswa kuwa na uwezo wa kujitathmini na kuchukua hatua na kufanya maamuzi sahihi kulingana na mazingira

yake. Katika muktadha wa Dadi, tunashuhudia mgongano wa ndani unaotokana na matarajio ya kijamii dhidi ya mahitaji ya kibinafsi. Hali hii inaweza kusababisha msongo wa mawazo, aibu, au hata kujihatarisha, jambo ambalo linapingwa na wataalamu wa afya ya kiakili kama (Leake, 2018) ambaye katika utafiti wake kuhusu jinsia na ushirikiano wa kitaaluma alionyesha kuwa miundo ya kijamii inayodhibiti hisia na maamuzi ya mtu huweza kuathiri vibaya ustawi wa kiakili.

Mtazamo wa kijamii unaodhani kuwa mwanamke na mwanamume hawawezi kushirikiana kazini usiku bila kuwa na uhusiano wa kimapenzi ni changamoto kwa usawa wa kijinsia na haki za kitaaluma. Kwa mujibu wa UN Women (2024), mtazamo huu unapaswa kubadilika ili kuunda mazingira ya kazi yenye usawa, salama, na yanayowezesha ushirikiano wa kitaaluma bila ubaguzi wa kijinsia. Ushauri wa kitaalamu ni kuwa: watu wafanye maamuzi yanayoendana na heshima yao na afya ya kiakili, jamii ibadili mitazamo ya kijinsia inayozuia ushirikiano wa kitaaluma na taasisi ziunde mazingira salama na ya usawa kwa kazi za usiku.

Mbinu anayotumia Dadi ya kuchunguza na kuchukua hatua hatari si mbinu njema ya kupigana dhidi ya unyanyasikaji kwa kuwa inamletea madhara. Dadi anaumia na kupelekwa hospitali hivyo kukatiza shughuli zake za kiuchumi. Mbinu mwafaka ambayo wanaume wanafaa kuchukua ni kuondoa ubabedume wa kuamini kuwa wanaume hawafai kumdhibiti mwanamke. Wanaume wanafaa kuhamasishwa kuwa mwanamume na mwanamke wanaweza kufanya kazi katika ofisi moja na pia usiku bila kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Ushauri wa kitaalamu ni kuwa: watu wafanye maamuzi yanayoendana na heshima yao na afya ya kiakili, jamii ibadili mitazamo ya kijinsia inayozuia ushirikiano wa kitaaluma na taasisi ziunde mazingira salama na ya usawa kwa kazi za usiku.

### 4.5.3. Kujipa Matumaini na Kuomba kuwa Hali Itabadilika

Matokeo ya utafiti huu yamebainiisha wanaume wanapopatwa na changamoto, aghalabu hujipa moyo na kutumaini kuwa hali itabadilika. Wanaamini kuwa huenda mambo yakabadilika na kuwa mazuri. Mhusika Dennis anatumaini kuwa akiimarika kiuchumi mambo yake yatakuwa shwari. Anatia bidii katika kusaka kazi.

Katika hadithi ya ‘Mapenzi ya Kifaurongo’ mhusika Dennis amesawiriwa na mwandishi akiwa mwingi wa matumaini. Mwandishi anasema:

> Mimi na Penina tunaishi katika mtaa wa New Zealand. Huu ni mtaa wa watu wenye mapato ya kadri. Hatujaoana. Lakini kodi yetu hulipwa na wazazi wa Penina kwa kuwa bado hatujapata kazi. Mara nyingi naona aibu, lakini najipa matumaini, moyo wa kuvumilia na kupigana. Penina naye ni mvumilivu kwelikweli. Kusema kweli si vyema kuendelea kuishi pamoja bila kuwa tumeoana. Hata hivyo, mipango ingalipo. Ninatamaa kubwa ya kupata kazi na anayenipa msukumo huu ni mchumba wangu Penina. Penina anasema hawezi kuolewa na mwanamume asiye na kazi yenye mshahara mkubwa. Hilo hunishangaza sana ingawa hunimakinisha katika tafutatafuta zangu. (TL, uk. 22)

Katika dondoo hili imebainishwa taswira ya mwanamume ambaye anakumbwa na hali ya kihisia ya kukosa heshima kwa sababu hana ajira wala kipato cha kumwezesha kujitegemea. Hali hii inamfanya aishi kwa kutegemea misaada ya wazazi wa mchumba wake Penina jambo linalomletea aibu na hisia za kutothaminiwa kama mwanamume katika jamii. Sentensi *Mara nyingi naona aibu, lakini najipa matumaini, moyo wa kuvumilia na kupigana* inaonyesha kuwa Dennis alikuwa anajipa matumaini kuwa mambo yangekuwa mema. Anasema kuwa, kwa sasa wanalipiwa kodi na wazazi wa Penina na anaona aibu lakini anajipa matumaini, moyo wa kuvumilia na kupigana.

Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho, unyanyasikaji wa Dennis unaonekana kupitia shinikizo la kijamii na matarajio ya kijinsia yanayomfanya kuhisi kuwa si mwanamume kamili kwa kuwa hana kazi. Penina anampa sharti kwa kumwambia kuwa hataolewa naye hadi awe na kazi yenye mshahara mkubwa. Kauli hii ni kashfa ya moja kwa moja inayomwumiza mumewe kisaikolojia na kumlazimu ajitahidi ili kudhibiti thamani yake kama mwanamume anayestahili ndoa. Matokeo haya yanalingana na manoni ya Kolaweska na Vital (2023) waliosema kuwa wanaume wanaoishi katika ndoa ambapo mke ndiye aliye na kipato kikubwa zaidi huwa na kiwango cha chini cha kuridhika katika maisha. Kwa sababu hii, Dennis anajaribu kujinasua kutokana na hali hii ya unyanyasikaji kwa kujipa matumaini, moyo wa kuvumilia na dhamira ya kupambana.

Kwa mujibu wa wataalamu wa usawa wa kijinsia, United Nations Development Programme (2022), Equimundo (2023) na García (2019) wanaume wanaweza kujitambua na kuchochea mabadiliko. Wanaweza kujitambua na kuchunguza nafasi yao na kujitathmini binafsi kuhusu jinsi mitazamo ya kijinsia waliyofundishwa tangu utotoni na athari zake kwa mahusiano ya kijamii na kikazi. Pia, wanafaa kuwa washirika wa usawa wa kijinsia kwa kuchukua hatua za wazi kupinga lugha ya kibaguzi, unyanyasaji, au vitendo vinavyodumisha mfumo dume. Vilevile wanafaa kushiriki katika juhudi za kubadilisha tamaduni za shirika zinazodumisha ubaguzi wa kijinsia, kwa mfano kwa kuunga mkono sera za usawa wa mishahara na likizo kwa wazazi wote na kujifunza kutoka maeneo ya kazi, familia, na jamii pana. Isitoshe, wanaume wanapaswa kujifunza kutoka kwa mashirika husika yanayotoa miongozo ya jinsi wanaume wanaweza kuwa sehemu ya suluhisho.

Dennis anatumia mbinu ya kujipa matumaini na kuomba kuwa hali itabadilika. Mbinu hii ilikuwa dhaifu kwa kuwa haikusuluhisha matatizo yake kwani mwishowe alifukuzwa nyumbani na mpenziwe Penina kwa kukosa ajira. Mwanamume anaponyanyasika, hafai kuvumilia tu na kuomba kuwa hali itabadilika. Wanafaa kuwa washirika wa usawa wa kijinsia kwa kuchukua hatua za wazi kupinga lugha ya kibaguzi, unyanyasaji, au vitendo vinavyodumisha mfumo dume. Wanastahili kupigana dhidi ya matarajio ya kijamii ambayo humtengea mwanamume jukumu la kukidhi mahitaji yote ya familia yake. Jamii inafaa kuhamasishwa kuwa mwanamume pia anaweza kumtegemea mwanamke kwani Mungu ndiye huchagua wa kubariki katika familia.

### 4.5.4. Kunyamaza au kutojali

Baadhi ya wanaume wengi wanapokabiliwa na tatizo, huwa si wepesi wa kuzungumza. Wakati mwingine wao hunyamaza na kuzidi kuumia moyoni kwa sababu ya kuhofia kukejliwa na jamii kuwa ni wanaume bwege. Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho, hili ni suala la ubabedume, utamaduni na ustoa.

Katika hadithi ya ‘Haramu Tamu’ katika *Diwani ya Maskini Milionea*, mhusika Chaurembo alimpenda sana mumewe Karisa. Hata hivyo, alikuwa akimwendea kinyume. Alikuwa ameolewa kwa miaka kumi na kujaliwa watoto watatu. Mumewe Karisa alikuwa mkurugenzi wa kampuni yake mwenyewe na aliitunza familia yake

vyema. Wengi walitamani maisha ya Chaurembo. Fauka ya haya, alimtafuta mpenzi wa kando aitwaye, Marasa. Walikubaliana kupatana katika sehemu za faragha. Chaurembo alirudi nyumbani usiku akiwa amechelewa na kumdanganya mumewe kuwa kazi zilikuwa nyingi. Karisa alijua kuwa mkewe alikuwa akienda kukutana na mpenzi wake wa kando.

"Niliyajua tangu mwanzo. Yote, Chaurembo" (MM, uk. 91)

Kauli kuwa *Niliyajua tangu mwanzo. Yote…*inaashiria kuwa Karisa alijua kuwa mkewe alikuwa na mapenzi nje ya ndoa lakini akamua kunyamaza. Karisa alikuwa amempa Chaurembo gazeti lililokuwa limeandikwa kuwa tapeli sugu alipata ajali ya barabara. Katika gari lake kulikuwa na picha za wanawake tajika akiwemo Chaurembo. Wakati Chaurembo alisoma hilo gazeti, makamasi na jasho zilimtoka. Mikono ikaanza kutetemeka kama ajuza wa miaka mia. Machozi yakamtoka kama maji kwenye chemchemi. Karisa alipoona hivyo, alimkumbatia mkewe kama vile hajawahi kufanya maisha yake yote. Chaurembo aliomba msamaha kwa kugugumiza. Naye mumewe akamwambia kuwa amekuwa akijua kutoka kitambo kuwa mkewe alikuwa na mpango wa kando. Ni wazi kuwa Karisa aliyajua yote yaliyokuwa yakiendelea lakini hakuthubutu kumwuliza mkewe. Aliamua kunyamaza. Hata katika jamii kuna baadhi ya wanaume ambao huamua kunyamaza hata wanapoona kuwa mambo hayaendi sawa. Hii ni kwa sababu katika baadhi ya tamaduni, wanaume wanapokuwa wazi na kuonyesha hisia zao, huonekena kuwa dhaifu na kuchukuliwa kama ishara ya kutokuwa na nguvu (Ingerson 2024).

Kulingana na nadharia, vipengele vya uchumi na jinsia vinashirikiana katika kunyanyasika na kuathirika kwa Karisa lakini anaamua kunyamaza anapojua kuwa mkewe anamwendea kinyume. Karisa anampa mkewe uhuru wa kufanya kazi ili kuchangia katika uchumi. Mkewe Chaurembo anaitumia nafasi hii vibaya na kuwa na mapenzi nje ya ndoa. Anaanza kurejea nyumbani akiwa amechelewa sana. Akiulizwa na mumewe amechelewa wapi anasema kuwa mikutano kazini imekuwa mingi. Anamdanganya mumewe kuwa alikuwa mikutano ya kikazi ilhali alikuwa na mpenzi wake wa kando wakichupa kutoka hoteli moja hadi nyingine. Mumewe karisa ananyanyasika kwa kukosa usingizi mkewe anapochelewa. Hana amani pia. Anasubiri mkewe arudi akiwa amezima taa za nyumbani. Mkewe anadhani kuwa mumewe kesha lala. Muda huu wote Karisa alielewa vyema yaliyokuwa yakiendelea ila aliamua kupingana na unyanyasikaji huu kwa kunyamaza.

Pia katika hadithi ya ‘Masharti ya Kisasa’ katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, tunamwona Bi. Zuhura akija kwa Dadi kununua samaki. Bi Zuhura alikuwa na tabia ya kuwapiga vijembe wanamtaa wenzake. Hivyo alipomwita Dadi, Dadi aliamua kutojibu swali lake. Mwandishi anasema:

> “Bwana Dadi,” aliita kwa sauti mwanamke mmoja aliyetaka kununua samaki. Alikuwa Bi. Zuhura, anayependa mafumbo na kuwapiga vijembe wanamtaa wenzake. Dadi alitamani kumwepuka bibi huyu sasa, ingawa angefurahi kwamba wale samaki wawili waliobaki wangemalizika kununuliwa. Alifunga breki za baiskeli yake. Akasimama ubavuni pa Bi. Zuhura. Dadi aliona huo ni upuzi mtupu. Hapo hapo akachupia baiskeli yake huku akimwambia Bi Zuhura “Wewe hutaki samaki, unataka umbeya na kujua mambo ya watu. (TL, uk. 62)

Sentensi *Dadi alitamani kumwepuka bibi huyu sasa*, na *Dadi aliona huo ni upuzi mtupu. Hapo hapo akachupia baiskeli yake huku akimwambia Bi Zuhura “Wewe hutaki Samaki, unataka umbeya* zinaashiria kuwa Dadi aliamua kumnyamazia Bi Zuhura. Bi Zuhura alimwita Dadi na kumsimamisha ili anunue samaki lakini haja yake haikuwa kukua samaki. Alitaka tu kumkejeli Dadi kuwa, alidhibitiwa na mkewe Kidawa. Alimwuliza Dadi kama alikuwa na samaki au walibaki tu wa kumkaangia Kidawa. Maneno haya hayakumfurahisha Dadi akaamua kunyamazia na kufanya biashara. Dadi alipomwambia wamebaki wawili, alianza kuwatomasatomasa kisha akamwuliza Dadi kwani wameoza. Dadi alikasirika naye sana. Kisha akamwuliza iwapo atamparia kwa kuwa hana mtu wa kumparia nyumbani. Dadi akasema atamparia lakini kwa bei. Tena, Bi Zuhura akamwuliza kwani ni yeye tu anayelipishwa kupara. Dadi alikasirika sana na kumwacha hapo. Dadi aliamua kumnyamazia kwa kuwa alijua kuwa haja yake haikuwa kununua samaki bali alitaka kumpiga vijembe. Dadi anaona kuwa kunyamaza ndio njia mwafaka ya kusuluhisha mgogoro kati yake na Bi Zuhura.

Kulingana na Audre (1984), ni matarajio ya jamii kuwa kuna kazi zinazotengewa wanaume na zingine wanawake. Jamii iliona kuwa Dadi alitekeleza majukumu yaliyofaa kuwa ya Kidawa kama vile: kufagia, kuosha vyombo, kupiga nguo pasi na kadhalika. Bi Zuhura alipomsimamisha Dadi alikuwa anataka kumkejeli lakini Dadi aliamua kumnyamazia.

Athari za kunyamazia changamoto au kutojali katika mazingira ya kijamii ni kubwa kwa wahusika wote wawili; mtenda na mtendewa. Kwa mtenda, hali hii huweza kusababisha msongo wa mawazo, kujihisi mnyonge, na kupoteza udhibiti wa kihisia. Kwa mtendewa, hujenga hisia za kutothaminiwa, aibu, na kujitenga kijamii. Kwa mujibu wa García Johnson na Otto (2019), uelewa wa kihisia na ushirikiano wa wazi huongeza uwezo wa mtu kushiriki katika jamii kwa kujiamini, na huchochea mazungumzo yenye kujenga katika mazingira ya kitaaluma na ya kifamilia.

Wanaotoa ushauri nasaha wanapendekeza mbinu mbalimbali za kusaidia mtu kujikomboa kutoka hali ya kimya kinachoumiza. Njia hizi zinajumuisha mawasiliano ya heshima, uthibitisho wa hisia, ushauri wa kitaalamu na elimu ya kihisia inayolenga kuongeza uelewa wa mtu juu ya hisia zake binafsi. Hatua hizi huimarisha uwezo wa mtu kufanya maamuzi ya busara, kudhibiti hisia, na kushiriki kikamilifu katika kujenga jamii yenye usawa, heshima, na fursa kwa wote. Mwanamume akitumia njia hizi anaweza kupambana dhidi ya unyanyasikaji.

### 4.5.5. Hatua ya Kujisaka na Kutafuta Suluhu

Rogers (1961), anasema kujisaka ni hatua ya kiini cha kujitambua ambapo mtu hujichunguza, kutafakari hali za ndani, na kutambua athari za mazingira katika maendeleo yake binafsi. Hili huweka msingi wa kupambana na vikwazo vya kijamii vinavyoweza kusababisha maumivu ya kihisia.

Kufuatia hatua ya kujisaka, mtu huingia katika awamu ya kutafuta suluhu, ambapo anaweza kutumia mbinu mbalimbali za kukabiliana na changamoto alizotambua. Beck (1976) anaeleza kuwa hatua hii hutegemea uwezo wa mtu wa kufanya tathmini ya mantiki juu ya hali yake na kuchagua njia zinazojenga ustawi wa kiakili, ikiwemo mawasiliano ya wazi, ushauri nasaha, au mabadiliko ya mtazamo wa kijamii.

Binadamu katika jamii za Kiafrika hawezi kuishi peke yake. Haya ni kulingana na Mbiti (1989). Katika jamii hizi mtoto alishirikishwa katika jamii yake kikamilifu, akafundishwa umuhimu wa ushirikiano kwa sababu ni kupitia kwa watu wengine mtu binafsi huweza kuhisi nafsi yake, madaraka yake na majukumu yake mwenyewe na majukumu yake kwa mwingine.

Katika hadithi ya 'Ndoto ya Mashaka' katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* mhusika Mashaka anatorokwa na mkewe pamoja na wanawe lakini anaamua kuwasaka walikopotelea. Mwandishi anasema:

> Katika maisha hayo siku zilijisotora zikapita kama hazitaki. Sura zetu zilitosha kuwa kurasa za kusomea. Dhiki ilikuwa ndiyo nguo na harufu yetu. Siku moja lakini nilishangaa nilipotoka kazini. Waridi sikumkuta mle chumbani mwetu. *Sikuona ndudu ya mtu!* Sikumwona yeye wala watoto wake. "Wamekwenda wapi watu hawa?" Nilijiuliza lakini sikupata jibu. Nilisubiri sana hawakutokea. Waridi mwenyewe hakuniaga. Niliendelea tu kuwasaka lakini wapi! Juhudi zangu za kuwasaka, mke na watoto wangu, ziligonga mwamba hatimaye. Nasikujua vipi. (TL, Uk. 76)

Sentensi *Nilisubiri sana hawakutokea. Waridi mwenyewe hakuniaga. Niliendelea tu kuwasaka lakini wapi! Juhudi zangu za kuwasaka, mke na watoto wangu, ziligonga mwamba hatimaye. Nasikujua vipi.* zinaonyesha wazi kuwa Mashaka aliisaka familia yake ilipotoroka. Siku moja Mashaka aliporejea kutoka kazini, alishangaa kupata kuwa mkewe Waridi na wanao hawakuwepo. Aliwaza kujihusu na kuanza kutafuta suluhu. Akaanza kuwasaka lakini anasema hakuwapata. Kulingana na nadharia, Mashaka alinyanyasika na kuathirika kwa sababu ya kipengele cha tabaka na uchumi. Mkewe Waridi na wanawe walitoroka kwa sababu Mashaka alikuwa maskini. Mashaka alijukumika kuisaka familia yake ili kupigana dhidi ya unyanyasikaji ule. Hata kama alidhihirisha juhudi za kupigana na tatizo lake, mbinu aliyotumia haikutosha kwa kuwa hakuwa ameshughulikia tatizo lilimtorosha bibiye pamoja na wanawe. Kwa hivyo, ikiwa wangerudi hali hiyo ingejirudia kwa kuwa hakuwa amejiimarisha kiuchumi.

Katika juhudi za mtu kuondokea athari za kihisia zinazotokana na kutengwa, mchakato wa kujitambua na kujithamini unakuwa msingi katika kujenga upya heshima na utu binafsi. Mashaka angeanza kwa kujisaka kwanza, aelewe hali yake ya kiuchumi na vile ilivyomwathiri yeye binafsi pamoja na familia yake. Tafiti za kitaaluma, kama zile za Rogers (1961) na Beck (1976), zinaonyesha kuwa kujitambua kisaikolojia ni hatua muhimu katika kuponya majeraha ya kihisia na kuanzisha mabadiliko ya kudumu. Baada ya kujisaka, Mashaka angeweza kujitambua na kuponya majeraha ya kihisia aliyokuwa nayo baada ya kutorokwa na familia yake.

Kisha angechukua hatua za kujiboresha kwa kujenga uhuru wa kifedha kupitia ajira na kuimarisha uthibitisho wa kijamii kwa kujihusisha na watu wanaomtambua na kumthamini. Baada ya kuimarika kiuchumi, angeanza safari ya kuisaka familia yake sasa. Mwanamume anapokabiliwa na hali ngumu inayomwathiri kisaikolojia, ni muhimu kwake kwanza kujisaka, kujitambua kisha kutafuta suluhisho la changamoto anayokabiliana nayo.

**4.6 Hitimisho**

Sehemu hii imeangazia uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kulingana na madhumuni. Madhumuni ya kwanza yameonyesha mwanamume hunyanyasika kwa njia kama vile: wake zao kushiriki mapenzi nje ya ndoa, kutenganishwa na familia, kukataliwa uchumba, kutukanwa, kunyimwa chakula, kuchapwa na kufanyishwa kazi za nyumba.

Katika madhumuni ya pili, athari za unyanyasikaji wa wanaume zimebainika kama vile: kujuta, kukata tamaa baada ya kutofaulu, kukosa amani na hata usingizi, kupata majeraha ya mwili, upweke baada ya kuachwa na familia zao, kusambaratika kwa asasi ya ndoa na kupatwa na msongo wa mawazo. Mwishowe, mbinu ambazo wanaume hutumia kupambana dhidi ya unyanyasikaji zimeshughulikiwa kama vile: kuvumilia au ustoa, kuchunguza na kuchukua hatua hatari, kujipa matumaini na kuomba kuwa hali itabadilika, kunyamaza au kutojali na kuchukua hatua ya kujisaka na kutafuta suluhu.

# SURA YA TANO

# MAJADILIANO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1. Utangulizi

Sura hii imeangazia majadiliano ya matokeo ya utafiti, hitimisho na kutoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## 5.2. Majadiliano

Majadiliano ya matokeo ya utafiti huu yamepangwa kulingana na madhumuni ya utafiti ambayo ni: namna za wanaume hunyanyasika, athari za unyanyasikaji huo na mbinu wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji. Mtafiti ameonyesha namna madhumuni haya yalifanikiwa katika sehemu ifuatayo:

### 5.2.1. Namna Wanaume Hunyanyasika

Madhumuni ya kwanza yalibainisha namna wanaume hunyanyasika katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Ilibainika kuwa wanaume hunyanyasika wenzi wao wanaposhiriki mapenzi nje ya ndoa au wanaposhuku kuwa wake zao wana mpango wa kando. Ukosefu wa uaminifu wa wanawake unapojitokeza katika ndoa, wanaume huhisi kuwa heshima na hadhi yao ya kiume imeshushwa na kusababisha unyanyasikaji wao wa kihisia. Katika jamii, jambo hili huwa ishara ya wanaume hao kutokuwa na mamlaka katika ndoa zao. Hii ni kwa sababu jamii huwatarajia wanaume kuwa na uwezo wa kuwadhibiti wake zao (Sikweyiya na wenzake, 2020). Kulingana na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho Crenshaw (1989), kipengele cha kiuchumi ndicho kilisababisha kunyanyasika huku. Matokeo haya yanakubaliana na Budyningrum na Ariana (2023) waliogundua kuwa wanaume wanaosalitiwa kwenye ndoa hunyanyasika kihisia na kupatwa na msongo wa mawazo.

Isitoshe, wanaume hunyanyasika kwa sababu ya kutenganishwa na familia zao. Kulingana na nadharia, kipengele cha utambulisho kinachosababisha utengano huu ni uchumi na matarajio ya jamii. Katika jamii za Kiafrika mke huhisi kuwa mume anastahili kuikimu familia yake (Stoebenau na wenzake, 2023). Itokeapo kuwa mwanamume hawezi kugharamia mahitaji haya, yeye hutorokwa na familia yake kama ilivyowafanyikia Mashaka na Dennis. Wengine hunyanyasika kwa kukataliwa uchumba. Wanaume wanakataliwa uchumba kwa misingi ya tabaka kulingana na nadharia ya utafiti. Itokeapo kuwa wachumba wametoka matabaka tofauti, baadhi ya

wazazi hukataa mahusiano yao. Matokeo haya yanakubaliana na ya Kagitcibasi (2017) aliyegundua kuwa wazazi wengi huwazuia watoto wao kuanzisha uhusiano wa kimapenzi na watu kutoka tabaka la chini, hasa kwa sababu ya kutaka kudumisha hadhi ya kiuchumi ya familia. Jambo hili huwaathiri wanaume kwani wengi wanatorokwa na wake zao wanaposhindwa kugharamia mahitaji ya familia.

Utafiti ulibainisha kuwa wanaume hunyanyasika kutokana na kutukanwa. Baadhi ya wanaume huelekezwa matusi kwa makosa wasiyoyafanya. Wengine hunyimwa chakula na wake zao iwapo hawakidhi mahitaji ya familia zao kikamilifu kwa sababu ya changamoto za kiuchumi. Vilevile wanaume wengine hunyanyasika kwa kuchapwa. Crenshaw (1989) anaeleza kuwa kipengele hiki cha kiuchumi kinapoathiriana na matarajio ya kijamii husababisha mwanamume kunyanyasika.

### 5.2.2. Athari za Unyanyasikaji wa Wanaume

Katika kutathmini athari za unyanyasikaji wa wanaume katika diwani teule, ilibainika kuwa wanaume huathirika kwa njia mbalimbali. Baadhi ya athari hizo ni kama vile: kujuta, kukata tamaa baada ya kutofaulu, kukosa amani na hata usingizi, kupata majeraha ya mwili, upweke baada ya kuachwa na familia zao, kusambaratika kwa asasi ya ndoa na kupatwa na msongo wa mawazo. Kulingana na matokeo ya utafiti, unyanyasikaji wa wanaume husababisha athari hasi zinazoathiri afya yao ya akili, heshima ya kibinafsi na nafasi yao katika jamii. Ilibainika kuwa kutokana na matarajio ya kijamii, wanaume hunyanyasika na kuathirika kihisia jambo ambalo huwasababishia mafadhaiko na huzuni (Tsui na wenzake, 2010). Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na Mahmood na wenzake (2023) waliogundua kuwa unyanyasikaji huu huathiri uwezo wa wanaume wa kushiriki kikamilifu katika jamii. Hali hii hujenga hisia za kutengwa, kudhalilishwa na hata kukata tamaa maishani. Hivyo, ilibainika kuwa unyanyasikaji wa wanaume ni changamoto ya kijamii iliyopuuzwa na ambayo inahitaji hatua madhubuti za kitaasisi kuchukuliwa ili kuitatua. Utatuzi wake una umuhimu katika kuwezesha maendeleo ya kijamii, usawa wa kijinsia na ustawi wa jamii kwa jumla. Vilevile unaweza ukasaidia katika kuvunja mifumo kandamizi ya kijinsia ambayo huwalazimisha kufuata viwango visivyofaa vya “mwanamume kamili”, hivyo kuwezesha maisha yenye utu, heshima na usawa kwa wote (Tsui na wenzake, 2010). Pia, hatua ya kutatua changamoto ya unyanyasikaji wa wanaume

itasaidia katika ujenzi wa jamii jumuishi inayoheshimu haki za bianadamu bila kujali jinsia.

### 5.2.3. Mbinu Wanazotumia Wanaume Kupambana Dhidi ya Unyanyasikaji

Katika madhumuni ya tatu utafiti ulibainisha mbinu wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji katika diwani teule. Ilibainika kuwa wanaume wanaponyanyasika hupambana dhidi yake kwa kutumia mbinu kama vile: kuvumilia au ustoa, kuchunguza na kuchukua hatua hatari, kujipa matumaini na kuomba kuwa hali itabadilika, kunyamaza au kutojali na kuchukua hatua ya kujisaka na kutafuta suluhu. Hata ingawa wengi wa wanaume walitumia mbinu hizi, hazikudhihirika kuwa madhubuti kwani hazikutatua changamoto ya unyanyasikaji wao kikamilifu. Badala yake, huongeza matatizo. Kwa mfano, wanaume wanaonyamaza baada ya kunyanyaswa na wake zao huishia kukumbwa na msongo wa mawazo, huzuni ya muda mrefu, na heshima yao ya kibinafsi kupotea kutokana na ukosefu wa msaada wa kijamii na kitaasisi (Mahmood na wenzake, 2023). Hivyo, kukaa kimya hakuondoi tatizo mbali hulea tatizo hilo kimyakimya hadi kufikia hatua hatari kama vile: kujitenga kijamii na hata kuwaza kujitia kitanzi.

Hali ya kuogopa kutafuta msaada kwa sababu ya hofu ya kudhalilika au kutoaminika katika jamii ni jambo linalowaweka wanaume katika mzunguko wa mateso yasiyoisha (Tsui na wenzake, 2010). Kwa hivyo suluhu dhabiti, ni wanaume kuhamasishwa kutafuta msaada, kujieleza kwa uwazi kuhusu wanayoyapitia, na kutafuta huduma za kitaalamu badala ya kuvumilia kimya kimya kwani ni mbinu hatari ya kufungia mateso ya muda mrefu bila kuchukua mwelekeo wa uponyaji.

## 5.3. Hitimisho

Utafiti huu umefaulu kwa kuwa umeonyesha wanaume hunyanyasika na kuathirika kwa njia mbalimbali katika diwani teule za Kiswahili. Umeonyesha wanaume wananyanyasika kwa njia kama vile: wake kushiriki mapenzi nje ya ndoa, kutenganishwa na familia zao, kukataliwa uchumba, kutukanwa, kunyimwa chakula, kuchapwa na kufanyishwa kazi za nyumba.

Wanaume wanaponyanyasika wanaathirika kwa njia kama vile: majuto, kukata tamaa, ukosefu wa amani, majeraha ya mwili, upweke, kusambaratika kwa ndoa, na msongo wa mawazo.

Utafiti umeonyesha kuwa wanaume wanaponyanyasika wanatumia mbinu mbalimbali za kupambana dhidi ya unyanyasikaji kama vile: kuvumilia au ustoa, kuchunguza na kuchukua hatua hatari, kujipa matumaini na kuomba kuwa hali itabadilika, kunyamaza au kutojali na kuchukua hatua ya kujisaka na kutafuta suluhu. Hata ingawa wanaume hujaribu kupigana na tatizo kwa kutumia mbinu hizi, utafiti huu ulibainisha kuwa si mbinu bora Hii ni kwa sababu, baadhi ya mbinu hizo hupalilia na kuzalisha mateso zaidi. Hivyo, ili kupata suluhu la kudumu wanaume wanapaswa kutafuta msaada wa kitaalamu kutoka taasisi husika, kuwa jasiri katika kueleza matatizo yao, kuchukua hatua ya kujisaka na kutafuta suluhu na kutokubali kukandamizwa na misimamo ya kijamii isiyo na misingi.

Utafiti huu una umuhimu kwani unahamasisha umma kuhusu matatizo wanayopitia wanaume na athari za unyanyasikaji wa wanaume. Vilevile, waandishi wa fasihi watanufaika na utafiti huu kwa kuwawezesha kutambua aina mbalimbali za unyanyasikaji wa wanaume. Isitoshe, waandishi wa fasihi watahamasishwa pia kuhusu nafasi ya fasihi kama chombo cha kuyafichua maovu yanayoiathiri jamii na kupendekeza suluhu. Pia, utakuwa wenye manufaa kwa wanaharakati wa haki za wanaume nchini na kimataifa kuwasaidia kuelewa mchango wa fasihi ya Kiswahili katika kuangazia suala la unyanyasikaji wa wanaume. Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho imechangia katika matokeo ya utafiti huu kwani imesaidia kuelewa vipengele vya utambulisho vinavyoshirikina na kusababisha unyanyasikaji wa wanaume. Vilevile matokeo ya utafiti huu yamechangia nadharia hii kwani yamethibitisha kweli kuwa vipengele vya utambulisho vya nadharia hii vinashirikiana katika kunyanyasika kwa wanaume.

## 5.4. Mapendekezo

Utafiti huu unapendekezea watetezi wa haki za binadamu waelimishe wanajamii kuhusu suala la unyanyasikaji wa wanaume na mbinu bora za kupambana dhidi yake. Jamii ihamasishwe kuwa wanaume ni binadamu kama wengine, wana hisia kama wanawake na huathirika kisaikolojia, kimwili na kihisia wanaponyanyasika. Mtafiti anapendekeza utafiti wa baadaye uzingatie:

1. Utanzu wa tamthilia na ushairi ili kubaini jinsi waandishi wameangazia suala la unyanyasikaji wa wanaume kwani utafiti huu ulijikita tu katika utanzu wa hadithi fupi
2. Suala la unyanyasikaji wa wanaume kwa kuongozwa na msingi tofauti wa nadharia.
3. Kuchunguza jinsi tamaduni za Kiafrika zinakuza na kuhimili unyanyasikaji wa wanaume.

**5.5. Hitimisho la sura**

Sehemu hii iliwasilisha majadiliano ya matokeo ya utafiti. Majadiliano ya matokeo yameelezwa kulingana na madhumuni ya utafiti ambayo yalikuwa: kubainisha namna wanaume hunyanyasika katika diwani teule, kutathmini athari za unyanyasikaji huo katika diwani teule na kufafanua mbinu wanazotumia wanaume kupambana dhidi ya unyanyasikaji katika diwani teule. Isitoshe, hitimisho lililotokana na matokeo ya utafiti lilitolewa. Baadaye mapendekezo ya tafiti za baadaye yaliorodheshwa.

## MAREJELEO


Adena Health Focus. (2025, April 22). *Breaking the Stigma: Why Seeking Counseling is a Sign of Strength*. Adena Health Focus. https://www.adena.org/health-focus/adena-health-focus/2025/04/22/breaking-the-stigma--why-seeking-counseling-is-a-sign-of-strength

Alberta, G. (2011) Men Abused Women Swahili Infosheet. https://www.family violence.alberta.ca.

Allen, E. S., Rhoades, G. K., Stanley, S. M., & Markman, H. J. (2015**.** Premarital Financial Expectations and Marital Outcomes: The Role of Economic Pressure and Communication**.** *Journal of Family Psychology*, 29(4), 433–443. https://doi.org/10.1037/fam0000093

Amadiume, I. (1987). *Male Daughters, Female Husbands: Gender and Sex in an African Society*.London: Zed Publishers Ltd.

APA (1892). Unyanyasaji Wanaume. https://www.apa.org.

Audre, L. (1984) *Sister Outsider: Essays and Speeches.* The Crossing Press. California

Bahemu, E. (2021) Wanaume Hunyanyaswa ila Hawasemi. https://www. Mwananchi .co.tz.

Beck, A. T. (1976). *Cognitive Therapy and the Emotional Disorders*. International Universities Press.

Berlyne, D. E. (1960). *Conflict, Arousal, and Curiosity*. McGraw-Hill.

Canadian Men's Health Foundation. (2025). *Men's Mental Health Research: Social Connection and Help-seeking in Canadian Men*. https://menshealthfoundation .ca/research/2025-mens-mental-health-research/

Chaterji, S. A. (2004). *Signs of Change in Patriarchal Ideas about Men and Women's Status and Role in Indian Society.* Katika Gender and Conflict Transformation.Irenees.net

Chokocho, A., & Kayanda D (Wah) (2016).*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* .Nairobi: Longhorn Publishers limited.

City News. (2025, June 26). *Gachagua's full statement on how Ruto and Sakaja Reportedly Hired Goons to Loot and Destroy Businesses Belonging to Kikuyus in Nairobi CBD*.https://citynews.co.ke/gachaguas-full-statement-on-how-ruto-and-sakaja-reportedly-hired-goons-to-loot-and-destroy-businesses-belonging-to-kikuyus-in-nairobi-cbd/

Crouse, M. L. (2005). *Presentation of Masculinity in a Selection of Male-Authored Post Apartheid Novels*, University of Stellenbosch.

Crenshaw, K. (1989). *Demarginalizing the Intersection of Race and Sex.* University of chicago Legal Forum

Crenshaw, K. (1989). *Demarginalizing the Intersection of Race and Sex.* University of Chicago Legal Forum

Creswell, J. W. (2014). *Research design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches* (4th ed.). SAGE Publications.

Derry-Vick, H. (2023, July 11). *Descriptive Research in Psychology*. Verywell Mind. https://www.verywellmind.com/descriptive-research-in-psychology-8551840

Equimundo. (2023). *State of the World's Fathers 2023*. https://www.equimundo.org/resources/state-of-the-worlds-fathers-2023/

Gagiano, A. (2002). *Achebe, Head, Marechera: On Power and Change in Africa*. Boulder: Lynne Rienner.

García Johnson, C. P., & Otto, K. (2019). Better together: A model for women and LGBTQ equality in the workplace. *Frontiers in Psychology, 10*, Article 272. https://doi.org/10.3389/fpsyg.2019.00272

Gitau, E. N. (2005). Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume Katika Fasihi Andishi ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Haslanger, S. (2024). *Feminist Perspectives on Sex and Gender*. Stanford

Encyclopedia of Philosophy. https://plato.stanford.edu/entries/feminism-gender/

Hill, E. J., LeBaron, A. B., Marks, L. D., & Rosa, C. M. (2022). Shared Financial Decision-making and Relationship Satisfaction: The Role of Economic Equality and Mutual Goals. *Family and Consumer Sciences Research Journal, 50*(3), 219–234. https://doi.org/10.1111/fcsr.12400

Hine, B., Roy, E., & Burhai, L. (2025). Father's Experiences of Family Breakdown and Domestic Abuse. *Psychology of Men & Masculinities*, 26(2), 265–274. https://doi.org/10.1037/men0000506

Ingerson, R. (2024, June 10). *Men are not sure how they're viewed – and if they are even required anymore*. Adelaide Now. https://www.adelaidenow.com.au/news/opinion/men-are-not-sure-how-theyre-viewed-and-if-they-are-even-required-anymore-robyn-ingerson/news-story/75827e26cfc9cb29dac9ac69040f71a0

IPP Media. (2017, Julai 27). *Jeraha la Moto na Namna ya Kulidhibiti*. https://legacy.ippmedia.com/sw/makala/jeraha-la-moto-na-namna-ya-kulidhibiti

IRC (2020).Unyanyasaji Wakijinsia. https:// gbvrespondrs.org./wp content/uploads/.

John, A., & Brown, B. (2018). *Reflective Practices and Coping Strategies Among Abused Men: A psychological perspective*. Nairobi: Wellness Press.

Kagitcibasi, C. (2017). *Family, Self, and Human Development Across Cultures: Theory and Applications* (2nd ed.). New York, NY: Routledge.

Karina, O. (2021). Ukandamizaji wa Wanaume. https: //doi .org/ 10.5 840/socphi/today202192988

Kausi, B. (2021). Dhuluma.za Kitabaka katika Riwaya ya Kiswahili. (Tasnifu ambayo Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi.

Kimani, C. W. (2003).Suala la Dhuluma dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili. (Tasnifu ambayo haijachapishwa).Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Kimani N. &Wafula R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Sai Industries Limited.

Kenya National Bureau of Statistics. (2022). *Women and Men in Kenya: Facts and Figures 2022*. https://www.knbs.or.ke/download/women-and-men-in-kenya-facts-and-figures-2022-report/

Kevin, C. (2019) Kwa nini Wanaume Hukaa Kimya Wanapofanyiwa Unyanyasaji wa Kijinsia. https://www.bbc.com/ Swahili habari-48211124

Khaisie, J. W., Simwa, S. W., & Gwachi, J. M. (2018). *Fear Mongering and Appeal to the Name of God as Propaganda Techniques in the Kenyan 2013 Presidential Debate*. *2*(2017), 1–6.

Kingei K. & Amata K. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacian Stan Text Publishers.

King'ei, K. (2002). *Suala la Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Uhakiki wa Tafiti kutoka Kenya.* Kiswahili Juzuu.65, Tuki Daresalam.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology; Methods and Technique*. New Delhi, New Age International (P) Limited.

Kowalewska, H., & Vitali, A. (2023). *Men's life Satisfaction is Lower when their Female Partner is the Main Earner*. *European Sociological Review*. (Imechapishwa)

Laititi, (2005) *Retrenchments & Domestic Violence*. A cause effect of Analysis

Leake, P. J. (2018). *Nursing, Power, and Gender in Interprofessional Collaboration* (Master's thesis, University of Toronto). TSpace Repository. https://hdl.handle.net/1807/91458

Mahmood, R., Otieno, M., & Kamau, J. (2023). *Psychosocial Impacts of Abuse on Male Participation in Community Development*. Nairobi: Centre for Gender and Social Research.

Matei, K. (2017).*Chozi la heri*.Nairobi: One planet Publishing and Media Services limited.

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text books and Graphics and Publishing Limited.

Mboya, M. (2018). Dhuluma kama Kichocheo Cha Mzinduko wa wanawake katika Riwaya ya Kiswahili.Internatinal journal Of Social Sciences and Information Technology.Vol 4. Nairobi

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi* .Nairobi. : East African Educational Publishers Ltd.M. Press.

Mwita, B. & Mutwiri F.(2018).*Usawiri wa Wahusika wa Jinsia ya kiume katika Riwaya ya Chozi La Heri* Chuo Kikuu cha Mashariki mwa Afrika, Baraton na Chuo kikuu cha Chuka.

Njogu, S. K. (1985). *Wanawake na mabadiliko ya kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi

Nyangweso, M. (2017). *Nafasi ya Mwanamke na Athari ya Kiongozi wa Kike katika Tamthilia Teule za Kiswahili*.Chuo Kikuu cha Masai Mara.

Nzonga, P. S. (2020). *Mgao wa Kazi za Wanaume katika Hadithi Fupi za Kiswahili*.( Tasnifu ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi.

Ortiz-Hernández, L., & Mendoza-Pérez, J. C. (2021). Association between Overt and Subtle Experiences of Discrimination and Violence and Mental Health in Homosexual and Bisexual Men in Mexico. *Journal of Interpersonal Violence, 36*(5-6), NP2654–NP2681. https://doi.org/10.1177/0886260519898423

Okiror, S. (2023, October 22). *The silent Mental Health Crisis among Men in Uganda*. BMJ Global Health Blogs. https://blogs.bmj.com/bmjgh/2023/10/22/the-silent-mental-health-crisis-among-men-in-uganda/

Palomino-Suárez, C., & Aparicio, M. E. (2025). Gender Stereotypes and their Impact on Social Sustainability: A Contemporary View of Spain. *Social Sciences*, *14*(5), Article 292. https://doi.org/10.3390/socsci14050292

Parhiala, P.(2021).Ukatili wa Kijinsia. Dignity kwanza Community salutions. https://www.dignity.org.2021

Rafiki, H. (2012) Vitendo vya Unyanyasaji kwa Wanaume Kupigwa na wake. https://www.rfi.RFI>Habari>RF-ki.

Rogers, C. R. (1961). *On Becoming a Person: A Therapist's view of Psychotherapy*. Houghton Mifflin

Ruto, M. (2015). *Matatizo ya Mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi.Nairobi

Samritha, V. (2025). Revisiting Men's Rights: Addressing Societal Pressure on Men and Men's Mental Health. *Shanlax International Journal of Arts, Science and Humanities*, *12*(S1), 75–79. https://doi.org/10.34293/sijash.v12is1-apr.8944

Schön, E., Ehlert, U., Schneeberger, M., Zimmermann, D., & Walther, A. (2025). Effects of diagnosing major depressive disorders in men on externalizing depression symptoms and conformity to traditional masculinity ideologies. *Psychology of Men & Masculinities*. Advance online publication. https://doi.org/10.1037/men0000518

Sikweyiya, Y., Addo-Lartey, A. A., Alangea, D. O., Dako-Gyeke, P., Chirwa, E. D., Coker-Appiah, D., Adanu, R. M. K., & Jewkes, R. (2020). *Patriarchy and Gender-inequitable Attitudes as drivers of intimate partner violence against women in the Central Region of Ghana*. BMC Public Health, 20(1), 682. https://doi.org/10.1186/s12889-020-08825-z

Taylor, C. (2023) Mauaji ya AKA: Kengele ya Kuiamsha Afrika Kusini. https://trtafrika. com/sw/africa/mauaji-ya-aka-kengele-ya-kuiamsha-afrika-kusini-133

Tsui, A., Mwangi, J., & Njoroge, P. (2010). *Mitazamo ya Kijamii na Changamoto za Wanaume katika Kutafuta Msaada wa Kisaikolojia*. Nairobi: Taasisi ya Maendeleo ya Jamii.

UNESCO. (2023). *Gender equality guidelines: Concepts and definitions.* United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000385896

United Nations Development Programme. (2022). *Gender Equality Strategy 2022–2025*. https://genderequalitystrategy.undp.org/

UN Women. (2024). *Generation Equality accountability report 2024*. United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women. https://knowledge.unwomen.org/en/digital-library/publications/2024/09/generation-equality-accountability-report-2024.

Vogel, D. L., Wester, S. R., Hammer, J. H., & Downing-Matibag, T. M. (2014). Referring Men to Seek Help: The Influence of Gender role Conflict and Stigma. *Psychology of Men and Masculinity*, *15*(1), 60–67. https://doi.org/10.1037/a0031761

Zhaksylyk, A. (2023). Research Integrity: Where we are and what we Need. *Journal of Korean Medical Science*, *38*(1), e1. https://doi.org/10.3346/jkms.2023.38.e1

# KIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Idhini ya NACOSTI



REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 315215

Date of Issue: 30/June/2025

**RESEARCH LICENSE**

**This is to Certify that Ms.. Elizabeth Wanjiru Waithaka of University of Embu, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Embu on the topic: UNYANYASAJI WA WANAUME KATIKA DIWANI ZA TUMBO LISILOSHIBA NA MASKINI MILIONEA NA HADITHI NYINGINEZO for the period ending : 30/June/2026.**

License No: **NACOSTI/P/25/4175862**

**315215**

Applicant Identification Number

Deputy Director

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**